# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

**Kikao cha Tano - Tarehe 2 Februari, 2019**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2018.

**MHE. ZAYNAB M. VULU (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2018.

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2018 na Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2018**

**MWENYEKITI:** Tunaanza na Mwenyekiti wa Kudumu ya Bunge ya Bajeti, karibu kwa kuwasilisha taarifa ya Kamati.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu taarifa yetu ni ndefu, hii nitakayosoma hapa ni *summary* tu ya taarifa yetu na hivyo ninaomba taarifa rasmi iliyowekwa mezani ndiyo iingie kwenye *Hansard* kama taarifa kamili ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2016, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa ya Mwaka kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Bunge ya Bajeti katika kipindi cha mwezi Januari, 2018 hadi Januari, 2019 pamoja na tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2018/2019 katika kipindi cha nusu mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati katika kipindi cha mwaka 2018, ilitekeleza shughuli zake kama zinavyoonyeshwa katika vipengele (a) hadi (p) vya taarifa ya Kamati. Tathimini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali inakwenda sambamba na kuangalia mwenendo wa viashiria mbalimbali vya uchumi. Kwa muhtasari, mwenendo wa viashiria hivyo vya ukuaji wa uchumi vimetathmiwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha uchumi wa Taifa ulikua kwa wastani wa 7% kwa kipindi cha miaka tatu mfululizo, yaani 2015 - 2017. Aidha, katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2018 pato la Taifa lilikua kwa 7% ikilinganishwa na asilimia 6.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango cha ukuaji wa uchumi kimechochewa na kuendelea kuongezeka kutokana na kuimarika kwa miundombinu, upatikanaji wa uhakika wa nishati wa umeme pamoja na kuongezeka kwa utolewaji wa huduma za jamii na bidhaa. Aidha, sekta zilizokua kwa kasi zaidi katika kipindi hicho ilikuwa ni Ujenzi (5.7%), Uzalishaji Viwandani (12%), Habari na Mawasiliano (11.2%) na Uchukuzi na Uhifadhi Mizigo (8.2%).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta zilizoendelea kutoa mchango mkubwa katika pato la Taifa kwa Januari hadi Juni, 2018 ni Kilimo (4.5%), Ujenzi (16.8%) na biashara (10.1%). Aidha, kasi ya ukuaji ya Sekta ya Kilimo imeendelea kuwa ndogo kwa asilimia 3.6 kwa kipindi hicho, licha ya kutoa mchango katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali katika kusimamia Sera ya Kodi na kudhibiti mfumko wa bei kupungua kutoka wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2018 hadi kufukia kiwango cha chini kabisa cha 3% mwezi Novemba, 2018, ambapo lengo la kipindi cha muda wakati ni 5%. Hatua hii imefikiwa baada ya mwenendo wa bidhaa na huduma za jamii kuwa imara kwa kipindi chote cha mwaka kutoka Januari hadi Desemba, 2018 pamoja na kutengemaa kwa bei ya mafuta katika Soko la Dunia na utekelezaji madhubuti wa Sera ya Fedha na za Bajeti. (Rejea Jedwali Na.1 ambalo limeonyeshwa katika ukurasa wa sita wa taarifa yetu).

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kuwa kwa kipindi cha Julai hadi Novemba, 2018, Dola ya Marekani imebadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,276/= ilikilinganishwa na shilingi 2,235/= katika kipindi cha Julai hadi Novemba, kwa mwaka uliopita 2017. Hii inaonesha Shilingi ilipungua thamani

dhidi ya Dola *(depreciation)* kwa asilimia 1.8. Kamati inatoa angalizo kuwa:-

(1) Serikali iongeze jitihada ya mauzo ya bidhaa na huduma nje; na

(2) Viwanda vizalishe zaidi bidhaa ambazo zinaagizwa nje kwa wingi. Hatua hizi zitasaidia kupunguza nakisi ya urari wa biashara na hivyo kuongeza upatiakanaji wa fedha za kigeni na thamani ya Shilingi *(appreciation).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonyesha kuwa Deni la Serikali limeendelea kukua. Deni hili linajumuisha fedha zilizokopwa na Serikali kutoka katika vyanzo vya ndani na nje; na sekta binafsi kutoka nje ya nchi kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Novemba, 2018, Deni la Taifa limekuwa likikua taratibu hadi kufikia shilingi trilioni 61.8. Ukuaji wa deni umetokana na mahitaji ya uwekezaji kwenye miradi ya maendeleo na kijamii nchini kwa ajili ya kukuza uchumi. Kielelezo Na.1 kinaonesha mwenendo wa ukuaji wa deni la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, pamoja na sababu nzuri za ukopaji na kwamba bado deni ni himilivu, Kamati inaendelea kuishauri Serikali iangalie uwiano uliopo kati ya mwenendo wa upatikanaji wa mapato ya ndani pamoja na ulipaji wa wa deni la Serikali na athari zake katika bajeti na uchumi.

Mheshimiwa Spika, tathmn zinaonesha kuwa Serikali kwa sasa imelazimika kujielekeza zaidi kukopa mikopo yenye masharti ya kibiashara *(Non Concessional Loans)* kuliko yenye masharti nafuu *(Concessional Loans).* Hii inatokana na ugumu wa upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu. Kamati bado inaona mikopo yenye masharti ya kibiashara *(Non Concessional Loans)* ina riba kubwa na hivyo kuwepo kwa mzigo mkubwa wa ugharamiaji wa mikopo kupitia mapato ya ndani. Kielelezo Na. 2 kinaonesha mwenendo wa mikopo ya masharti ya kibiashara na masharti nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 94 Bunge lilijadili mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2018/2019 uliowasilishwa Bungeni na Waziri wa Fedha na Mipango. Kamati imeridhishwa na hatua ya utekelezaji wa mapendekezo mbalimbali yanayotolewa na Kamati kwa Serikali. Baadhi ya mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2018/2019 ambao Serikali inayafanyia kazi ni kama yafuatayo:-

(1) Uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji kwa sekta binafsi;

(2) Urasimishaji wa sekta isiyo rasmi;

(3) Diplomasia ya kiuchumi. Hapa Kamati imeridhishwa na hatua ambazo Serikali imeanza kuzichukua ikiwa ni pamoja na kutoa maelekezo kwa Waheshimiwa Mabalozi wote kuanza kutafuta masoko ya bidhaa za Tanzania pamoja na kuvutia wawekezaji wapya kuja nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati imeridhishwa na hatua ya Serikali kuzitumia taasisi zake kama vile *TANTRADE, TANAPA, TAWA, NGOROGORO Consavation authourity TNBC* na *TAC* katika kuitangaza nchi yetu kwenye masuala ya utalii, biashara na uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miswada iliyoshughulikiwa na Kamati kwa mwaka 2018; wa kwanza ni wa Sheria ya Fedha ya Mwaka, 2018 *(The Finance Bill, 2018);* Muswada wa pili ni wa Huduma Ndogo za Fedha kwa Mwaka, 2018 *(Microfince Act, 2018);* Muswada wa tatu ni Muswada wa Sheria wa Ubia Baina ya Serikali na Sekta Binafsi *(The Public Private Patnership Admentment Bill, 2018);* na azimio moja lililoshughulikiwa na Bunge la Kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika *(The African Charter on Statistics).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa pamoja na Mwongozo wa Kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2019/

2020; kwa upande wa Bajeti ya Serikali, makisio yanaonesha kuwa kwa mwaka 2019/2020 jumla ya shilingi trilionI 3.5 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika katika kipindi cha mwaka 2019/2020 ikiwa ni ongezeko la asilimia 3.2 ukilinganisha na shilingi trilioni 32.47 kwa mwaka 2018/2019. Kati ya fedha hizo shilingi trilioni 23.2, sawa na asilimia 99.25 ya bajeti yote, zinatokana na mapato ya ndani ambapo mapato ya Halmashauri zinatakiwa shilingi bilioni 795.68 na mapato ya kodi shilingi trilioni 20.12 na mapato ya siyo ya kodi, shilingi trilioni 2.28.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali inategemea kupata kiasi cha shilingi trilion 3.38 ikiwa ni msaada wa mkopo nafuu kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la asilimia 26.3 ikilinganishwa na shilingi trioni 2.67 kwa mwaka 2018/2019. Ni mategemeo ya Kamati kuwa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati kwenye taarifa yake iliyowasilishwa hapa Bungeni kuhusu mwongozo na maandalizi ya mpango wa bajeti kwa mwaka 2019/2020 yamechukuliwa na Serikali na watayafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti imepewa jukumu la kuchambua hoja zitakazojitokeza kwenye Kamati za Bunge za Kisekta wakati wa kujadili Bajeti za Wizara kwa ajili ya kuishauri Serikali. Kamati ya Bajeti ilitekeleza jukumu hilo katika kipindi cha mwezi Machi hadi Juni, 2018 kwa kupokea maombi mbalimbali ya nyongeza za fedha za bajeti zilizoombwa na Kamati za Kisekta kwa ajili ya Wizara ambazo Kamati hizo zinasimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokea jumla ya hoja 23. Kimsingi Serikali imeweza kuzifanyia kazi hizo hoja zote 23 na kwa kadri iliyowezekana kulingana na upatikanaji wa fedha wamejaribu kuzitekeleza. Hata hivyo, inaendelea kuishauri Serikali kutekeleza ahadi zake kama tulivyokubaliana kwenye mashauriano kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2018 kwa kipindi cha nusu mwaka. Kamati

imefanya uchambuzi wa utekelezaji wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2018/2019 kama ifuatavyo: Kodi ya Mapato *(Income Tax)*, marekebisho yalifanyika ili kupunguza kiwango cha Kodi ya makampuni kutoka asilimia 30 hadi asilimia 20 kwa viwanda vya madawa na uzalishaji wa bidhaa za ngozi wapya kwa kipindi cha miaka mitano. Hatua hii imewezesha viwanda vitano vipya vya madawa kufunguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kupanua punguzo hili kwa viwanda vingine vya kimkakati pamoja na viwanda vilivyopo katika sekta hizo ili kuwe na ushindani ulio sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura Na. 148 yalilenga kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye taulo za kike zinazozalishwa nchini. Hatua hii mpaka sasa imepunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 38.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii imeathiri wazalishaji wa ndani wa taulo hizo kwa kuwa hivi sasa hawawezi kuomba marejesho ya *VAT* walizozilipia katika ununuzi wa mali ghafi kutoka nje na uzalishaji. Hivyo taulo zinazozalishwa ndani zimekuwa na bei ya juu ukilinganisha na zinazoingizwa kutoka nje. Kamati inaishauri Serikali kutoa msamaha maalum *(special relief)* ili taulo za ndani ziweze kushindana na zinazoagizwa kutoka nje kwa nia ya kulinda uzalishaji wa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia ilitoa msamaha wa kodi kwa miradi ya Serikali inayotekelezwa kwa mikopo ya kibiashara na mikataba ya miradi ya utekelezaji kati ya Serikali na Taasisi za Fedha. Kamati inashauri kuwa, ni vyema miradi ya nyuma nayo ikanufaika na kukwamuliwa kutokana na msamaha huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya uchambuzi kwenye Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura Na. 147 na kuona kuwa marekebisho ya viwango maalum vya kodi *(specific duty rates)* kwa bidhaa zisizo za petroli

zinazotoka nje kwa kiwango cha mfumuko wa bei 5% yamesaidia upatikanaji wa kiasi cha shilingi bilioni 1.464 kati ya shilingi bilion 3.462 ya lengo ya ukusanyaji wa kodi hiyo kwa mwaka mzima, yaani sawa na asilimia 42 tu. Changamoto hii ya upungufu wa mapato imesababishwa na upungufu wa uagizwaji wa bidhaa hizo toka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya uchambuzi kwenye marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147 na kuona kuwa marekebisho ya viwango maalum vya kodi yaani *specific duty rates* kwa bidhaa zisizo za petroli zinazotoka nje kwa kiwango cha mfumuko wa bei wa asilimia tano yamesaidia upatikanaji wa kiasi cha shilingi bilioni 1.464, kati ya shilingi bilioni 3.462 ya lengo la ukusanyaji wa kodi hiyo kwa mwaka mzima, yaani sawa na asilimia 42 tu. Changamoto hii ya upungufu wa mapato imesababishwa na upungufu wa uagizwaji wa bidhaa hizo toka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura 41; marekebisho yaliyofanyika katika kiwango cha kodi kinachotozwa kwenye michezo ya kubahatisha na matokeo ya michezo yamesaidia upatikanaji wa mapato ya kiasi cha shilingi bilioni 14.851 kati ya shilingi 29.7202 zilizotarajiwa kupatikana kwa mwaka mzima. Kwa hiyo umefikia asilimia 50 mwenendo huu unaonesha kuwa kodi hii imefanya vizuri na itaweza kufikia lengo la ukusanyaji kwa mwaka kama ilivyokusudiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilifanya marekebisho kwenye Sheria ya Usimamizi wa Kodi na kuanzisha utaratibu maalum wa kusamehe kodi yaani *tax amnesty* hatua hii imeisaidia kupokea maombi ya 9,070 yenye kiasi cha kodi ya shilingi trilioni 1.21 na kiasi cha riba ya adhabu ya shilingi bilioni 806.166 mpaka sasa kiasi cha shilingi bilioni 201.901 kimekusanywa kama kodi ya msingi yaani *principle tax*. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii nakuhamasisha ulipaji wa kodi kwa hiari na ni vema Serikali ikafikiria tena kuongeza muda ili kuruhusu maombi zaidi kwa walipa kodi ambao bado wanasita kutumia fursa hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki *(The East Africa Community Customs Management Act)* pamoja na viwango vya ushuru vya pamoja vya forodha zilifanyiwa marekebisho ili kuendelea kulinda viwanda vinavyozalisha mafuta ya kula nchini. Hata hivyo, katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2018 kiasi cha mafuta ghafi ya kula yaliyoingizwa nchini yalikuwa na thamani ya jumla ya shilingi bilioni 4.9 ikilinganishwa na thamani ya jumla ya shilingi bilioni 262.3, kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2017/ 2018 sawa na upungufu wa asilimia 98.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kudhibiti mafuta yaliyokuwa yanaingia kama ghafi yaani *crude oil* ilhali ni mafuta yaliyosafishwa *refined oil* na ndio maana uingizaji wa mafuta ghafi umeshuka na wakati huo huo uingizaji wa mafuta yaliyosafishwa umeongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa *Stamp* za Kodi za Kielektroniki *(Electronic Tax Stamps)*. Serikali imeanzisha mfumo wa *stamps* za kodi za kielektroniki yaani *ETS* ulioanza kutumika tarehe 1 Septemba, 2018 kwa lengo la kutumia teknolojia ya kisasa kupata taarifa sahihi ya uzalishaji viwandani na kwa wakati. Takribani mitambo 37 yaani 15 kwenye viwanda vya bia na 22 kwenye sigara na pombe kali imefungwa. Kamati inaipongeza hatua hii nzuri ya Serikali ya kutumia mfumo huu, hata hivyo, inaendelea kuishauri Serikali kwa sasa kutumia mfumo huu kwenye bidhaa kama vile bia, sigara na pombe kali na kufanya tathmini ya mafanikio yake kabla ya kutumia mfumo huu kwenye bidhaa nyingine kama vile maji, soda na *juice*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi; takwimu zinaonesha kuwa katika kipindi cha mwezi Julai hadi Disemba, 2018, makusanyo ya kodi ya majengo kwa halmashauri zote yalikuwa ni kiasi cha shilingi bilioni 8.41, sawa na asilimia 28 tu ya lengo la ukusanyaji wa mapato hayo kwa mwaka mzima. Kwa upande wa makusanyo ya kodi ya mabango yaani *Billboards* kwa halmashauri zote yalifikia shilingi bilioni 12.3 sawa na asilimia

62.65 ya lengo la ukusanyaji wa kodi hiyo kwa mwaka mzima. Kamati inaona kuwa kiwango cha ukusanyaji wa kodi ya majengo kimeshuka kwa asilimia 44.5, wakati ukusanyaji wa kodi za mabango umeongezeka kwa asilimia 64.6. Kamati inaishauri Serikali kuongeza bidii ya ukusanyaji wa kodi ya majengo kwa kushirikiana na halmashauri husika. Jedwali namba mbili linaonesha ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa bajeti wa Serikali katika kipindi cha nusu ya mwaka wa fedha 2018/2019 na mwelekeo hadi Juni 2019; mwenendo wa makusanyo ya mapato. Takwimu zinaonesha kuwa katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali ilipanga kukusanya jumla ya shilingi trilioni 32.475, kati ya fedha hizo shilingi trilioni 20.158 yalikuwa ni mapato ya ndani, shilingi bilioni 735.5 mapato ya halmashauri na shilingi trilioni 8.905 ni mikopo ya ndani kwa ajili ya kudumisha deni yaani *roll over* na mikopo ya kibiashara kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, Serikali inatarajia kupokea jumla ya shilingi trilioni 2.13 kutoka kwa washirika wa maendeleo ambayo inajumuisha misaada ya kibajeti na misaada ya mikopo ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Disemba, 2018, jumla ya mapato yote ambayo Serikali imekusanya ni shilingi trilioni 12.839 ambayo ni sawa na asilimia 80.4 ya lengo la nusu mwaka la kukusanya shilingi trilioni 15.974. Kiasi hiki kilichokusanywa ni sawa na asilimia 39.5 tu ya lengo la ukusanyaji wa kiasi shilingi 32.475 kwa mwaka. Kutofikiwa kwa makusanyo haya katika kipindi cha nusu mwaka kwa kiasi kikubwa kumechangiwa na kutopokelewa kwa wakati misaada na mikopo ya kutoka nje iliyokuwa imeahidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jedwali namba tatu linaonesha mwenendo wa ukusanyaji wa katika kipindi cha nusu mwaka yaani Julai – Disemba, 2018. Uchambuzi wa Kamati unaonesha kuwa ukusanyaji wa mapato ya ndani kodi ya ushuru wa forodha imeongezeka kwa kukusanya shilingi trilioni 3.143 ikifuatiwa na walipaji wakubwa kiasi cha shilingi trilioni 2.980 na mwisho kodi za ndani kiasi cha shilingi

trilioni 1.594. Kwa takwimu hizi inaonesha kwamba kwa kiasi kikubwa mapato yetu yanategemea biashara za kimataifa *(International trade)* na wafanyabiashara wakubwa hivyo ni lazima Serikali kuhakikisha kwamba inachukua hatua za makusudi ili kuongeza mauzo yetu nje ya nchi pamoja na kuweka mazingira wezeshi kwa nchi jirani kuendelea kutumia bandari zetu ili kupata mapato mengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenendo wa matumizi; Serikali inatumia mfumo wa *cash budget* ambapo kiasi cha fedha kinachokusanywa ndio kiasi ambacho kinatumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya maendeleo. Katika kipindi cha nusu mwaka Serikali ilitumia kiasi jumla ya shilingi trilioni 12.839 kati ya shilingi 20.468 zilizoidhinishwa na Bunge kwenye matumizi ya kawaida. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 62.72.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hatua hizi nzuri ya utolewaji wa fedha, Kamati imebaini kuwa, kuna baadhi ya Mafungu yamepokea zaidi ya malengo yaliyopangwa katika kipindi cha nusu mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinganisho wa sura ya bajeti ya Serikali kwa mwaka 2018/2019 na utolewaji wa fedha katika kipindi cha nusu mwaka 2018/2019; Kamati imebaini kuwa katika kipindi cha nusu mwaka 2018/2019 kiasi cha shilingi trilioni 12.839 ya mapato yote yaliyokusanywa na kiasi cha shilingi trilioni 4.77 sawa na asilimia 37.1 yalitumika katika kugharimia ulipaji wa deni la Taifa pamoja na riba ya madeni yaliyoiva. Aidha, kiasi cha shilingi trilioni 3.311 kilitumika katika kulipia mishahara sawa na asilimia 25.6. Mwenendo huu unaonesha kuwa kiasi cha fedha shilingi trilioni 8.08 kimetumika katika ulipaji wa deni la Taifa na mishahara tu na kinachobakia shilingi trilioni 4.749 kimetumika katika matumizi mengineyo na maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika inaonesha kuwa kwa vigezo vyote deni la Taifa ni himilivu ukilinganisha na nchi nyingine za jirani ambazo ama zinakaribia ukomo au zimevuka vigezo vilivyowekwa. Kamati inaona kuwa mwenendo wa utolewaji wa fedha kwenye

matumizi mengineyo na miradi ya maendeleo siyo wa kuridhisha. Mathalani kati ya Mafungu 92 ya Serikali ni Mafungu 14 tu yaliyopata fedha za maendeleo zaidi ya asilimia 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo ya jumla:-

KWA KUWA Serikali ilikubali kutoa shilingi bilioni 38.9 kwa ajili ya miradi ya afya na shilingi bilioni 29.7 kwa ajili ya umaliziaji wa miradi ya elimu yaani maarufu kwa jina la maboma;

NA KWA KUWA hatua hii imekuwa ya mafanikio kwa kupande wa sekta ya afya wakati miradi ya elimu imekwama utekelezaji na endapo ahadi ya Serikali haitatekelezwa itawakatisha tamaa wananchi kuchangia katika miradi ya maendeleo kwa siku zijazo;

HIVYO BASI Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kuhakikisha inatoa kiasi kilichobaki ili kufikia shilingi bilioni 251 ambazo zilikuwa zinahitajika kwa ajili ya kukamilisha maboma hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, KWA KUWA Serikali bado haijaweza kufanya vizuri katika utolewaji wa fedha za ndani kwenye matumizi ya maendeleo kutokana na upungufu wa mapato;

NA KWA KUWA fedha za nje za wahisani wa maendeleo zinatolewa kwa asilimia 13.16 tu ya fedha zote zilizoahidiwa;

HIVYO BASI Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutekeleza mwongozo wa ushirikiano wa wahisani yaani *DCF – Development Cooperation Framework* ili kuimarisha uhusiano utakaosaidia upatikanaji wa fedha hizo kwa sababu bado kama Taifa tunazihitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, KWA KUWA Serikali imeweka utaratibu wa kutoza amana ya asilimia 15 pindi wamiliki wa viwanda wanapoagiza sukari ya viwandani kutoka nje;

NA KWA KUWA fedha hizo zitatakiwa kurejeshwa kwa wamiliki wa viwanda pindi uhakiki wa sukari unapomalizika;

HIVYO BASI Kamati inaishauri Serikali kutumia *Escrow Account* ambayo tayari imekwishafunguliwa kwa ajili ya kuhifadhi amana hizo ili pindi uhakiki unapokamilika fedha hizo ziweze kurejeshwa kwa wahusika.

KWA KUWA katika utekelezaji wa bajeti katika kipindi cha nusu mwaka, sekta ya kilimo, uvuvi na ufugaji zimepata fedha za maendeleo chini ya asilimia 40;

NA KWA KUWA sekta hizi zinazoajiri takribani asilimia 70 ya Watanzania na ndizo zinazozalisha malighafi ya viwandani;

HIVYO BASI Kamati inaishauri Serikali kuelekeza fedha hizo kwenye sekta hizo ili kuchochea ukuaji wa uchumi wa viwandani na kupanua fursa ya ajira na kuboresha miundombinu ya uchumi na kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, KWA KUWA Kamati imebaini kwamba hatua ya Serikali ya kusamehe riba na adhabu zinazotokana na makosa ya kodi *(tax amnesty)* imeonesha mafanikio makubwa sana. Serikali imefanikiwa kukusanya zaidi ya shilingi bilioni 200, hatua hii ni ya kuipongeza Serikali;

HIVYO BASI, kamati inaishauri yafuatayo ili kiasi cha shilingi bilioni 720.6 ziweze kupatikana katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka 2018/2019:-

(1) Kuharakisha kushughulikia maombi 3,371 yaliyobaki; na

(2) Kuharakisha kusikiliza kesi za kodi ambazo ziko kwenye ngazi za bodi na rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, KWA KUWA michezo ya kubahatisha imekuwa ikikua kwa kasi sana nchini. Aidha michezo hii kwa asili yake si ya kiuzalishaji hivyo haina mlolongo wa thamani yaani *value chain;*

NA KWA KUWA michezo nchini inaendeshwa kwa mujibu wa sheria michezo hii ina madhara makubwa sana kwa Taifa

HIVYO BASI Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuongeza kodi kwenye mapato yanayotokana na michezo yaani *tax on winning* ili kupata mapato zaidi na wakati huo huo kupunguza ushiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa yote iingie kwenye *Hansard*. Pia naomba nichukue nafasi hii nihitimishe kwa kukushukuru wewe, Mheshimiwa Mwenyekiti kwa niaba ya Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa miongozo yenu. Aidha, napenda nimshukuru Waziri Mheshimiwa Dkt, Mpango na Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Ashatu kwa Ushirikiano walioonesha pamoja na wataalam wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano waliotuonesha. Aidha, niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati na kwa sababu ya muda sitawataja majina yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kipekee kabisa kutoa shukrani kwa Ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake katika kipindi chote. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Mkurugenzi Ndugu Lina Kitosi na Naibu Mkurugenzi wa Kamati ndugu Michael Kadebe na wataalam wengine katika Kamati hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa na Kamati pamoja na uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti katika kipindi cha nusu mwaka, naomba Bunge lako lipokee lijadili na kuidhinisha maoni na mapendekezo yaliyotolewa katika taarifa hii ambayo mengi yake sikuyasoma bali yako kwenye taarifa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, hoja imeungwa mkono. Nakushuru sana Mwenyekiti wa Bajeti, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene.

**TAARIFA YA MWAKA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KATIKA KIPINDI CHA JANUARI, 2018 HADI JANUARI, 2019 PAMOJA NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA KIPINDI CHA NUSU MWAKA 2018/2019 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**(Imetolea chini ya Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016)**

## 1.0. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2016, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa ya Mwaka kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Bunge ya Bajeti katika kipindi cha mwezi Januari 2018 hadi Januari 2019 pamoja na tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2018/19 katika kipindi cha nusu mwaka.

## 2.0. UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2018, Kamati ya Bajeti ilitekeleza majukumu yake kwa kuzingatia majukumu yaliyoanishwa katika kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 Mwaka 2015, Kanuni za Bunge Toleo la 2016, Sheria ya Fedha na Sheria nyingine, taratibu na miongozo mbalimbali iliyopo inayohusiana na masuala ya fedha, kodi na bajeti. Katika kutekeleza shughuli hizo, Kamati ilikutana na Serikali, Taasisi, Mashirika na Sekta binafsi pamoja na wadau mbalimbali ili kuwasikiliza pamoja na kupokea Taarifa na maoni mbalimbali ambayo Kamati ilitumia wakati

ikitekeleza majukumu yake na hatimaye kutoa maoni na ushauri kwa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, zifuatazo ni kazi zilizotekelezwa na Kamati ya Bajeti katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari 2018 hadi Januari 2019: -

a) Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2017/2018;

b) Kupitia na kujadili utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa katika kipindi cha Mwaka 2017/2018;

c) Kutathmini na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa kipindi cha Mwaka 2018/2019 yatokanayo na vyanzo vya kodi na vyanzo vingine visivyo vya kodi;

d) Kupitia na kujadili kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa kipindi cha Mwaka 2019/2020;

e) Kupitia na kujadili utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2017/2018; pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019;

f) Kuchambua na kushauri kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2018 *(The Finance Act, 2018*);

g) Kuchambua na kushauri kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (The Public Private Partneship (Amendment) Bill, 2018));

h) Kuchambua na kushauri kuhusu Muswada wa Sheria ya Huduma ndogo za Fedha wa mwaka 2018 (The Microfinance Act, 2018);

i) Kuchambua na kushauri kuhusu Azimio la Bunge la kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika *(The African Charter on Statistics);*

j) Kupitia na kujadili kuhusu Mwongozo wa kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/ 2010

k) Kupitia na kujadili utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa katika kipindi cha mwaka 2018/2019;

l) Kushiriki mafunzo mbalimbali yenye lengo la kuwaongezea wajumbe wa Kamati uwezo na ujuzi katika kuchambua Sera za kodi, fedha na za kiuhasibu zilizopendekezwa na Serikali;

m) Kukutana na wadau mbalimbali wa masuala ya kodi na kujadili changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika utekelezaji wa sheria mbalimbali za kodi na sizizo za kikodi zinazoathiri sekta binafsi;

n) Kufanya utafiti na uchambuzi wa vyanzo mbalimbali vya mapato na kutoa mapendekezo kuhusu hatua za kupunguza utegemezi wa kibajeti;

o) Kutoa ushauri wa jumla kuhusu bajeti ya Serikali kwa Bunge na Kamati za Kudumu za Bunge; na

p) Kuchambua hoja zilizojitokeza kwenye Kamati za Bunge za Kisekta wakati wa kujadili Bajeti za Wizara kwa mwaka 2017/2018 kwa ajili ya kuishauri Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatoa shukrani kwa Serikali na wadau wote waliowezesha kukamilika kwa shughuli hizi.

## 2.1. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali inakwenda sambamba na kuangalia mwenendo wa viashiria mbalimbali vya uchumi. Kwa muhtasari mwenendo wa viashiria hivyo vya ukuaji wa uchumi vimetathminiwa kama ifuatavyo:

### 2.1.1. Pato la Taifa

**Mheshimiwa Spika,** takwimu za Serikali zinaonesha uchumi wa Taifa ulikua kwa wastani wa **asilimia 7.0** kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo (2015-2017). Aidha, katika kipindi cha Januari hadi Juni 2018, Pato la Taifa lilikuwa kwa **asilimia 7.0** ikilinganishwa na **asilimia 6.3** katika kipindi kama hicho mwaka 2017. Kiwango cha ukuaji wa uchumi kimechochewa na kuendelea kuongezeka na kuimarika kwa miundombinu, upatikanaji wa uhakika wa nishati ya umeme pamoja na kuongezeka kwa utolewaji wa huduma za jamii na bidhaa. Aidha, sekta zilizokua kwa kasi zaidi kwa kipindi hicho ilikuwa ni ujenzi **asimilia 15.7**, uzalishaji viwandani **asilimia 12.0,** habari na mawasilino **asilimia 11.2** na uchukuzi na uhifadhi mizigo **asilimia 8.2.**

**Mheshimiwa Spika,** Sekta zilizoendelea kutoa mchango mkubwa katika Pato la Taifa (Januari – Juni, 2018) ni kilimo **asilimia 34.5**. Ujenzi **asilimia 16.8** na Biashara **asilimia 10.1.** Aidha, kasi ya ukuaji wa sekta ya kilimo imeendelea kuwa ndogo **(asilimia 3.6)** kwa kipindi hicho licha ya kutoa mchango mkubwa katika Pato la Taifa.

### 2.1.2. Mfumuko wa Bei

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali katika kusimamia sera za kodi na kudhibiti mfumuko wa bei kupungua kutoka wastani wa **asilimia 4.3** mwaka 2017/2018 hadi kufikia kiwango cha chini kabisa cha **asilimia 3.0** mwezi Novemba, 2018 ambapo lengo la kipindi cha muda wa kati ni asilimia 5. Hatua hii imefikiwa baada ya mwenendo wa bidhaa na huduma za jamii kuwa imara kwa kipindi chote cha mwaka kutoka Januari hadi Desemba , 2018 pamoja na kutengamaa kwa bei ya mafuta katika soko la Dunia na utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha na za bajeti. (Rejea Jedwali namba 1).

**Jedwali Namba 1: Mwenendo wa bei za bidhaa na huduma za jamii na mfumuko wa bei kutoka mwezi januari hadi desemba, 2018 (des. 2015=100)**

| Mwezi | Fahirisi za Bei za Taifa | Mfumuko wa Bei wa Taifa (%) | Mfumuko wa Bei wa Bidhaa za Vyakula (%) | Mfumuko wa Bei wa Bidhaa Zisizo za Vyakula (%) | Mfumuko wa Bei ambao Haujumuishi Vyakula na Nishati (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| Jan-18 | 110.13 | 4.0 | 6.7 | 2.8 | 1.4 |
| Feb-18 | 111.33 | 4.1 | 5.8 | 3.3 | 1.7 |
| Mar-18 | 112.70 | 3.9 | 5.0 | 3.5 | 1.6 |
| Apr-18 | 113.20 | 3.8 | 4.0 | 3.9 | 1.4 |
| May-18 | 113.24 | 3.6 | 3.2 | 4.5 | 1.6 |
| Jun-18 | 112.81 | 3.4 | 3.8 | 4.0 | 1.6 |
| Jul-18 | 112.44 | 3.3 | 3.0 | 4.2 | 1.6 |
| Aug-18 | 112.01 | 3.3 | 3.2 | 4.6 | 2.0 |
| Sep-18 | 112.12 | 3.4 | 3.1 | 4.8 | 2.2 |
| Oct-18 | 111.83 | 3.2 | 2.5 | 5.0 | 2.3 |
| Nov-18 | 112.17 | 3.0 | 2.0 | 5.3 | 2.6 |
| Dec-18 | 112.76 | 3.3 | 2.6 | 5.4 | 3.1 |
| **Wastani 2018** | **112.23** | **3.5** | **3.7** | **4.3** | **1.9** |
| **Wastani 2017** | **108.42** | **5.3** | **9.6** | **3.2** | **2.0** |

***Chanzo:*** *Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2018*


## 2.1.3. Mwenendo wa Thamani ya Shilingi

**Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonesha kuwa kwa kipindi cha Julai hadi Novemba 2018, Dola ya Marekani imebadilishwa kwa wastani wa Shilingi 2,276 ilikilinganishwa na Shilingi 2,235 katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2017. Hii inaonesha Shilingi ilipungua thamani dhidi ya Dola (depreciation) kwa asilimia 1.8. Kamati inatoa angalizo kuwa, Moja; Serikali iongezee jitihada ya mauzo ya bidhaa na huduma nje, Pili; Viwanda vizalishe zaidi bidhaa ambazo zinaagizwa nje kwa wingi. Hatua hizi zitasaidia kupunguza nakisi ya urari wa biashara na hivyo kuongeza upatiakanji wa fedha za kigeni na hivyo kuongeza thamani ya Shilingi (appreciation)

### 2.1.4. Deni la Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Takwimu zinaonyesha kuwa Deni la Serikali limeendelea kukua. Deni hili linajumuisha fedha zilizokopwa na Serikali kutoka katika vyanzo vya ndani na nje , pia na Sekta Binafsi kutoka nje ya nchi kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Novemba 2018, Deni la Taifa limekuwa likikua taratibu hadi kufikia Shilingi 61.8 trilioni. Ukuaji wa deni umetokana na mahitaji ya uwekezaji kwenye miradi ya maendeleo na kijamii nchini kwa ajili ya kukuza uchumi.

**Kielelezo Namba 1: Mwenendo wa ukuaji wa Deni la Serikali (Deni la Ndani na Nje).**





**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua kuwa Serikali hukopa kwa sababu ya kupata fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kupata fedha za kigeni kwa ajili ya kulinda urari wa malipo wa kimataifa, kukopesha taasisi za ndani za umma kutekeleza miradi ya kimkakati na pia kuendeleza soko la ndani la mitaji ili kujenga uwezo wa soko kuwezesha Serikali na sekta binafsi kukopa zaidi siku zijazo (Domestic debt market development). Hata, hivyo pamoja na sababu nzuri za ukopaji ikiwemo ukizingatia kwamba deni kuwa himilivu, Kamati inaendelea kuishauri Serikali iangalie uwiano uliopo

kati ya mwenendo wa upatikanaji wa mapato ya ndani pamoja na ulipaji wa Deni la Serikali na athari zake katika bajeti na uchumi.

### 2.1.5. Mikopo ya Kibiashara

**Mheshimiwa Spika,** tathmnini zinaonesha kuwa Serikali kwa sasa imelazimika kujielekeza zaidi kukopa mikopo yenye masharti ya kibiashara (Non Concessional Loans) kuliko yenye masharti nafuu (Concessional) kama ilivyokuwa awali. Kutokana na ugumu wa upatikanaji wa mikopo hii, Kamati bado inaona mikopo yenye masharti ya kibiashara (Non Concessional Loans) ina riba kubwa na hivyo kuwepo kwa mzigo mkubwa wa ugharamiaji wa mikopo kupitia mapato ya ndani na hivyo kuathiri utekelezaji wa Bajeti hasa kwa upande wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo na utoaji wa huduma za maendeleo.

**Kielelezo Namba 2: Mwenendo wa mikopo ya masharti ya Kibiashara na masharti nafuu.**



## 2.2. UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 94 Bunge lilijadili mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2018/2019 uliowasilishwa Bungeni na Waziri wa Fedha na Mipango. Kamati ilipata fursa ya kufanya tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendelo wa Mwaka 2017/2018, kuchambua na baadaye kutoa maoni na mapendekezo kuhusu Mpango wa mwaka 2018/2019, kupitia Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni. Bunge lilitoa maoni na mapendekezo na hatimaye Mpango huo kuidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2017/18 ulikuwa wa kuridhisha. Changamoto iliyojitokeza ni ile ya kutopokea kiasi cha fedha za nje kutoka kwa wahisani zilizotarajiwa kutekeleza baadhi ya miradi. Changamoto hii imepelekea Kamati kuendelea kuishauri Serikali kupanga Bajeti yake ya Maendeleo kwa kutegemea mapato yake ya ndani na mikopo ya ndani ambayo upatikanaji wake ni wa uhakika. Aidha, Kamati inapenda kutoa angalizo kwa Serikali kuhakikisha kuwa ukopaji wake katika vyanzo vya ndani hauathiri upatikanaji wa mikopo kwa Sekta binafsi.

**Mheshimiwa Spika,** kamati imeridhishwa na hatua ya utekelezaji wa mapendekezo mbalimbali yanayotolewa na Kamati kwa Serikali. Baadhi ya mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2018/19 ambayo Serikali imeyafanyia kazi ni yafuatayo: -

### 2.2.1. Uboreshaji wa Mazingira ya Uwekezaji kwa Sekta Binafsi

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuweka mikakati na mipango mbalimbali ya kuboresha Mazingira ya Ufanyaji Biashara na Uwekezaji Nchini. Serikali iliandaa na kuanza kutekeleza Mwongozo wa Mapinduzi ya Kuboresha Mazingira ya ufanyaji biashara Tanzania “*Blueprint*” ambayo endapo itasimamiwa vizuri italeta maboresho katika mazingira ya

ufanyaji biashara na uwekezaji nchini. Pamoja na hatua hii muhimu, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kufanya mabadiliko ya baadhi ya Sheria ili Blueprint iweze kutekelezeka pamoja na kuweka muda maalumu wa utekelezaji wa muongozo huo. Aidha, mwongozo huu utafsiriwe katika lugha ya Kiswahili ili uweze kuleta uelewa wa pamoja kwa wadau.

### 2.2.2. Urasimishaji wa Sekta Isiyo Rasmi

**Mheshimiwa Spika**, bado kuna idadi kubwa ya biashara na wafanyabiashara wadogo wanaojihusisha na shughuli mbalimbali za kiuchumi katika mfumo usio rasmi, hivyo kutochangia katika mapato ya Serikali. Shughuli hizi zinaonekana katika pato ghafi la Taifa na kuonyesha kwamba pato la taifa linakua lakini hazionekani katika uchangiaji wa kodi. Hali hiyo inasababisha wigo wa kodi kuwa mdogo *“narrow tax base”*.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua kwamba Serikali imeanza kuwatambua na kuwasajili baadhi ya wafanyabiashara wadogo kwa kutoa vitambulisho na kuwapa namba ya mlipa kodi (TIN Number) ikiwa ni jitihada ya kuwajumuisha kwenye mfumo rasmi. Vilevile, Serikali inaandaa utaratibu wa kuwatambua na kuwasajili wakulima wote nchini ili waweze kupewa vitambulisho. Hatua hizi zitasaidia Serikali kuwa na takwimu sahihi za wajasiliamali na wakulima na hivyo kuweza kupanga mipango yake kwa ufasaha pamoja na urasimishaji wa sekta isiyo rasmi ili iweze kutoa mchango wake kwenye mapato ya kodi.

### 2.2.3. Diplomasia ya kiuchumi

**Mheshimiwa Spika,** Diplomasia ya kiuchumi ni eneo muhimu katika kusaidia Serikali kukuza uchumi na kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato Mafanikio yake yanategemea kwa kiasi kikubwa utangazaji wa vivutio vilivyopo ili kuvutia wawekezaji wa kigeni kwenye sekta mbalimbali kama vile kilimo, uvuvi, utalii, miundombinu, biashara na huduma. Kamati imeridhishwa na hatua ambazo Serikali imeanza

kuzichukua ikiwa ni pamoja na kutoa maelekezo kwa Waheshimiwa Mabalozi wote kuanza kutafuta masoko ya bidhaa za Tanzania pamoja na kuvutia wawekezaji wapya kuja nchini. Kamati imeona kuwa ni vema Balozi zeu zikashirikiana na mamlaka mbalimbali na Taasisi za Serikali kama vile TANTRADE, TANAPA, TAWA, Ngorongoro Conservation Authority, TNBC na TIC katika kuitangaza nchi yetu kwenye masuala ya utalii, biashara na uwekezaji

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kutekeleza maoni na mapendekezo yenye lengo la kuboresha utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Serikali. Baadhi ya maoni hayo ni;-

i. Kuongeza kasi ya kuweka mazingira mazuri yatakayowezesha utekelezaji wa Miradi ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi;

ii. Kupitia upya gharama za ujenzi wa barabara nchini kwani baadhi ya barabara zimeonekana kujengwa kwa gharama kubwa sana;

iii. Kuona umuhimu wa kukusanya yenyewe mapato yake (kodi, tozo) katika maeneo mengi badala ya kutumia kampuni binafsi kukusanya mapato (outsource);

iv. Kuboresha maeneo na mifumo ya ukusanyaji wa mapato katika vituo vya mabasi, maegesho ya magari, masoko, kumbi za starehe na viwanja vya michezo;

v. Kuweka muda maalum ambao kila Halmashauri italazimika kupitia Sheria zake za ukusanyaji kodi kwa lengo la kuhuisha kulingana na mabadiliko ya wakati na mazingira;

vi. Kuhuisha mifumo ya utambuzi wa wananchi kwa kutumia aina moja ya kitambulisho. Mfano kuhuisha taarifa za Vitambulisho vya Taifa (NIDA), usajili wa vizazi na vifo unaofanywa na RITA, vitambulisho vya mpiga kura, pamoja na kusajili anuani za makazi.

## 2.3. MISWADA ILIYOSHUGHULIKIWA NA KAMATI KWA MWAKA 2018

**Mheshimiwa Spika**, Kwa nyakati tofauti Kamati ya Bajeti ilipitia na kujadili miswada mbalimbali iliyoelekezwa kwake na hatimaye kutoa ushauri na mapendekezo kwenye vifungu mbalimbali vya Miswada hiyo. Kwa muhtasari Kamati ilipitia na kujadili miswada ifutayo: -

### 2.3.1. Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2018 (The Finance Bill, 2018).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipitia na kujadili Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2018 uliokuwa na lengo la kufanya mabadiliko ya vifungu mbalimbali vya sheria kwa kuondoa, kuongeza na kusamehe, ushuru, kodi, ada na tozo mbalimbali. Shughuli hii ilifanyika kwa kupitia kifungu kwa kifungu pamoja na kupokea maoni kutoka kwa wadau (Public Hearing). Baada ya kujiridhisha na maudhui yake, Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Serikali kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya Sheria mbalimbali zilizopendekezwa.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Sheria hizi umefafanuliwa kwa kina kwenye uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2018/19 kwa kipindi cha nusu.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, Kamati ilikamilisha jukumu lake kwa kuwasilisha Bungeni maoni na mapendekezo yake kuhusu Muswada huo na hatimaye Sheria hii iliidhinishwa na kuanza kutumika na Serikali tarehe 1 Julai, 2018.

### 2.3.2. Muswada wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018 *(The Microfinance Act, 2018)*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti ilifanya uchambuzi na kutoa maoni ya Muswada wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018. Kwa mara ya kwanza Sheria hii imetungwa nchini ili kukidhi mabadiliko ya kasi yanayotokea katika sekta ya fedha kutokana na kuongezeka kwa watoa

huduma ya fedha ukijumuisha ushiriki wa taasisi zisizo za kifedha kutoa huduma za kifedha na kuongezeka kwa teknolijia ya kutoa huduma ya fedha na kuongezeka kwa mahitaji ya mitaji na mikopo.

**Mheshimiwa Spika**, Kutungwa kwa Sheria hii kutasaidia kuleta usimamizi mzuri wa sekta ndogo ya fedha pamoja na upatikanaji wa huduma ya fedha nchini (*financial inclusion)*.

### 2.3.3. Muswada wa Sheria ya Ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi *(The Public Private Partnership Amendment Bill, 2018)*

**Mheshimiwa Spika,** lengo la Muswada huu lilikuwa ni kuimarisha mfumo wa kitaasisi na kisheria katika usimamizi wa miradi ya ubia na pia kutatua changamoto zilizopo katika utekelezaji wa miradi ya ubia ili kurahisisha uibuaji, uidhinishaji na utekelezaji wa miradi ya husika.

## 2.4. AZIMIO LILILOSHUGHULIKIWA NA KAMATI KWA MWAKA 2018

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (6)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Bunge ya Bajeti ilichambua na kuwasilisha maoni na ushauri kuhusu Azimio la Bunge la kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika (The African Charter on Statistics).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua, kutathmini na kujiridhisha na sababu za msingi zilizopelekea kuwepo na haja ya kuwa na Mkataba wa Takwimu wa Afrika. Malengo ya Mkataba huo ni pamoja na Afrika kuwa na mfumo bora wa kuratibu upatikanaji na usambazaji wa takwimu bora za kiuchumi, kijamii na mazingira zitakazotumika katika kupanga na kutolea maamuzi mbalimbali ya kisera katika ngazi ya Taifa, Kanda na Bara zima la Afrika.

**Mheshimiwa Spika,** kuridhiwa kwa Mkataba huu kutakuwa na faida mbalimbali kwenye sekta nyingine za kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni. Nchi zote duniani zinazopiga

hatua za maendeleo ya kiuchumi na kijamii zinategemea upatikanaji wa takwimu sahihi ambazo uchakataji wake unasaidia watunga sera na wataalamu wa mipango kushauri ipasavyo kuhusu maendeleo ya nchi kiuchumi na kijamii.

## 3.0. MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA PAMOJA NA MWONGOZO WA KUTAYARISHA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2019/ 2020.

**Mheshimiwa Spika,** mwezi Novemba 2018, Kamati ya Bajeti ilipitia na kujadiliana na Serikali kuhusu Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2019/2020. Kimsingi Mwongozo huu umeelekeza masuala ya msingi ya kuzingatiwa katika uandaaji wa Mpango na Bajeti ikiwemo kuandaa mipango inayozingatia mahitaji halisi ya rasilimali fedha, udhibiti wa matumizi yasiyo ya lazima, matumizi ya mifumo ya kieletroniki katika ukusanyaji wa mapato na malipo ya mtandao (GePG), uingizaji wa takwimu za Bajeti ya Serikali kwenye mifumo ya CBMS na PlanRep, miradi ya kimkakati ya kuongeza mapato ya Halmashauri (SGRP) pamoja na ulipaji na udhibiti wa ulimbikizaji wa madeni.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Bajeti ya Serikali, makisio yanaonesha kuwa kwa Mwaka 2019/2020 jumla ya **Shilingi trilioni 33.5** zinatarajiwa kukusanywa na kutumika kwa kipindi cha mwaka 2019/2020 ikiwa ni ongezeko la **asilimia 3.2** ukilinganisha na **Shilingi trilioni 32.47** kwa mwaka 2018/2019. Kati ya fedha hizo **Shilingi trilioni 23.20** sawa na **asilimia 69.25** ya Bajeti yote zitatokana na mapato ya ndani ambapo mapato ya Halmashauri yanatarajiwa kuwa **Shilingi bilioni 795.68,** mapato ya kodi **Shilingi trilioni 20.12** na mapato yasiyo ya kodi **Shilingi trilioni 2.28.**

**Mheshimiwa Spika**, aidha, Serikali inategemea kupata kiasi cha **Shilingi trilioni 3.38** ikiwa ni misaada na mikopo nafuu kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo, kiasi hiki ni sawa na ongezeko la **asilimia 26.3** ikilinganishwa na **Shilingi trilioni 2.67** kwa mwaka 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, ni mategemeo ya Kamati kuwa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati kwenye taarifa yake iliyowasilishwa hapa Bungeni kuhusu Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2019/2020 yamechukuliwa na Serikali na kuyafanyia kazi. Kamati inaendelea kusisitiza kuhusu upatikanaji wa vyanzo vipya vya mapato vitakavyosaidia kuongeza mapato ya Serikali. Aidha, Serikali ijielekeze zaidi katika programu za maendeleo zinazohusu sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi ili ziweze kuleta tija kwenye ukuaji wa uchumi utakaogusa wananchi wengi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilishauri kuwa msingi na shabaha ya mpango ujao ujielekeze katika kuoanisha na kuendeleza vipaumbele ambavyo havikutekelezwa kwa **asilimia 100** katika Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2017/2018 pamoja na kujibu changamoto na vikwazo vya kimfumo vilivyojitokeza katika kuendesha na kusimamia uchumi katika Mpango unaoendelea kutekelezwa. Aidha, ni muhimu Serikali kuzingatia muda wa utekelezaji wa miradi, kujenga nidhamu ya kazi, uimarishaji wa umakini katika kubuni, kusimamia na kutekeleza miradi ya maendeleo.

## 4.0. HOJA ZA KAMATI ZA BUNGE ZA KISEKTA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti imepewa jukumu la kuchambua hoja zitakazojitokeza kwenye Kamati za Bunge za kisekta wakati wa kujadili Bajeti za Wizara kwa ajili ya kuishauri Serikali. Kamati ya Bajeti ilitekeleza jukumu hilo katika kipindi cha mwezi Machi hadi Juni, 2018 kwa kupokea maombi mbalimbali ya nyongeza za fedha za bajeti zilizoombwa na Kamati za Kisekta kwa ajili ya Wizara ambazo Kamati hizo zinasimamia.

**Mheshimiwa Spika,** kwa muhtasari Kamati ilipokea jumla ya hoja 23, kati ya hoja hizo hoja 13 zilihusu fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mafungu mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2017/2018; hoja 9 zilihusu nyongeza ya fedha kwa ajili ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na hoja 1 ilielekezwa na Mheshiwa Spika moja kwa moja kwenye

Kamati ya Bajeti Hoja hiyo ilihusu fedha za Mfuko wa kuendeleza zao la korosho zinazotokana na asilimia 65 ya ushuru wa kusafirisha korosho ghafi nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilipokea Hoja zote na baada ya mashauriano na Kamati ya Bajeti ilizifanyia kazi kama ifuatavyo: -

**a)** **Fungu 68**- Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Serikali ilitoa kiasi cha **Shilingi bilioni 1.3** kati ya Shilingi **bilioni 10** zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya mradi wa Mkongo wa Taifa. Pia, Serikali ilitoa kiasi cha **Shilingi bilioni 1.28** kati ya **Shilingi bilioni 3** zilizoidhinishwa na Bunge kwa mradi wa Anuani za Makazi na Simbo za Posta.

**b)** **Fungu 14**-Jeshi la Zimamoto. Serikali ilitoa kiasi chote cha fedha kiasi cha **Shilingi milioni 500** kwa ajili ya ununuzi wa dawa za kuzimia moto.

**c)** **Fungu 51**- Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Serikali ilitoa kiasi chote cha fedha **Shilingi bilioni 20** kwa ajili ya kukamilisha mradi wa **NIDA**.

**d)** **Fungu 58** – Wizara ya Nishati. Serikali ilitoa kiasi cha **Shilingi bilioni 300** kati ya **Shilingi bilioni 469** kilichoidhinishwa na Bunge kwenye miradi ya kupeleka umeme Vijijini (REA).

**e)** **Fungu 100** - Wizara ya Madini. Serikali ilitoa kiasi cha **Shilingi bilioni 845** kwa taasisi ya TEITI (Dola za Canada 500,000).

f) Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Serikali ilikubali kutoa kiasi cha **Shilingi bilioni 38.9** kwa ajili ya miradi ya Afya na Shilingi **bilioni 29.7** kwenye miradi ya elimu.

**Mheshimiwa Spika,** baadhi ya hoja zilichukuliwa na Serikali na kuahidi kuzifanyia kazi katika mwaka wa fedha 2018/2019. Hoja hizo zilihusu:-

**a)** **Fungu 34**-Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Hoja kuhusu ujenzi wa Ubalozi wa Tanzania nchini Oman (Muscat), kiasi cha **Shilingi bilioni 1.8** zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya ujenzi huo.

**b)** **Fungu 14** - Jeshi la Zimamato. Hoja ilihusu ununuzi wa magari ya zimamoto kiasi cha **Shilingi bilioni 3**, Serikali iliahidi kuzitoa katika robo ya kwanza ya bajeti ya Serikali ya mwaka 2018/2019.

**c)** **Fungu 28** - Jeshi la Polisi na **Fungu 29** - Jeshi la Magereza. Hoja ilihusu madai ya ulipaji wa ankara za umeme **Shilingi bilioni 8** na ankara za Maji **Shilingi bilioni 7** kwa Jeshi la Polisi na madai ya ulipaji ankara za umeme **Shilingi bilioni 4** na ankara za Maji **Shilingi bilioni 2** kwa Jeshi la Magereza**.** Jumla ya madai ni kiasi cha **Shilingi bilioni 21**.
Serikali iliahidi kuwa kiasi hiki cha fedha kitalipwa baada ya uhakiki ya kukamilika kwa kuwa madai haya ni mapya.

**d)** **Fungu 57** – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Hoja ilihusu ulipwaji wa fidia katika eneo la Ras Mshindo katika Wilaya ya Kilwa kiasi cha **Shilingi bilioni 3.6**. Serikali iliahidi kulipa baada ya kukamilka uhakiki uliotarajiwa kuanza mwezi Julai, 2018.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa hoja za nyongeza ya fedha kwa ajili ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2018/19, Serikali ilitekeleza yafuatayo:-

a) TAMISEMI **(Fungu 73 - Mkoa wa Iringa na Fungu 36 - Mkoa wa Katavi).** Serikali ilikubali kuongeza kiasi cha **Shilingi bilioni 1.5** kwa ajili ya ukarabati na uendelezaji wa Hospitali ya Wilaya. Aidha, Serikali ilitenga kiasi cha **Shilingi bilioni 4.4** kwa ujenzi wa Majengo ya Utawala.

**b)** **Fungu 64** - Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Serikali ilikubali kutoa kiasi cha **Shilingi milioni 500** kwa ajili ya kufanya upembuzi akinifu (feasibility study) wa ujenzi wa bandari ya uvuvi.

**c)** **Fungu 46** Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Serikali ilikubali kutoa kiasi cha **Shilingi bilioni 5** kwa ajili ya kuchapisha vitabu vya miongozo ya walimu.

**d)** **Fungu 43 -** Kilimo, iliyohusu fedha za NFRA bakaa ya fedha za maendeleo **Shilingi bilioni 71**; Serikali Ilipendekeza fungu husika kuendelea kutumia kiasi kilichotengwa kwa mwaka 2018/19 **Shilingi bilioni 15**. Vilevile Serikali iliahidi endapo kama kutakuwa na mahitaji ya nyongeza Serikali itatoa fedha hizo. Aidha, Kamati ilishauri Serikali iruhusu Wakulima kuuza mazao nje ya nchi baada ya Serikali kufanya manunuzi, pendekezo ambalo lilikubaliwa.

**e)** **Fungu 98** –Wizara ya Ujenzi, hoja kuhusu mgawanyo wa fedha kati ya Wakala wa Barabara vijijini na TANROADS kwa uwiano wa **asilimia 50** kwa 50, Serikali iliahidi kufanyia tathmini pendekezo hili kupitia Bodi ya Mfuko wa Barabara na taarifa hiyo itawasilishwa kwa Kamati husika.

**Mheshimiwa Spika,** kimsingi Serikali imeweza kuzifanyia kazi hoja husika kwa kadiri ilivyowezekana kulingana na upatikanaji wa fedha. Hata hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutekeleza ahadi zake kama tulivyokubaliana kwenye mashauriano kwa mujibu wa Bajeti ilivyoidhinishwa na Bunge.

## 5.0. UTEKELEZAJI WA SHERIA YA FEDHA YA MWAKA 2018 KWA KIPINDI CHA NUSU MWAKA 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipitia na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2018. Aidha, taarifa hii imeainisha mikakati inayoendelea kutekelezwa na Serikali ya kusimamia ukusanyaji wa mapato kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya kodi na visivyo vya kodi ili kuweza kufikiwa kwa lengo la Serikali kwa kipindi kilichobaki kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi wa utekelezaji wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2018/19 kama ifuatavyo: -

## a) Kodi ya Mapato (Income Tax)

**Mheshimiwa Spika,** marekebisho yalifanyika ili kupunguza kiwango cha Kodi ya makampuni kutoka **asilimia 30** hadi **asilimia 20** kwa viwanda vya Madawa na Wazalishaji wa Bidhaa za Ngozi wapya kwa kipindi cha miaka 5. Hatua hii imewezesha, viwanda vitano (5) vipya vya madawa vimefunguliwa ambavyo ni **Prince Pharmaceuticals Co. Ltd, Kairuki Pharmaceutical Industry Ltd, Zinga Pharmaceutical Ltd, Vista Pharmaceutical Ltd Bahari Pharmaceutical Ltd and M Pharmaceuticals Ltd**. Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kupanua punguzo hili kwa viwanda vingine vya kimkakati pamoja na viwanda vilivyopo katika sekta hizo ili kuwe na ushindani ulio sawa

## b) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148

**Mheshimiwa Spika,** marekebisho kwenye sheria hii yalilenga kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye taulo za kike zinazozalishwa nchini. Hatua hii mpaka sasa imepunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha **Shilingi milioni 38.9**. Hatua hii imeathiri wazalishaji wa ndani wa taulo hizo kwa kuwa hivi sasa hawawezi kuomba marejesho ya VAT (Input tax) walizolipia katika ununuzi wa malighafi kutoka nje na uzalishaji. Hivyo taulo zinazozalishwa ndani zimekuwa na bei ya juu ukilinganisha na zinazoagizwa kutoka nje. Kamati inashauri Serikali kutoa msamaha maalumu *“special relief”* ili taulo za ndani ziweze kushindana na zinazoagizwa kutoka nje ili kulinda wazalishaji wa ndani.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali pia ilitoa msamaha wa kodi kwa miradi ya Serikali inayotekelezwa kwa mikopo ya kibiasahara na mikataba ya miradi ya utekelezaji kati ya Serikali na Taasisi za Fedha. Utekelezaji wa hatua hii umekuwa na changamoto kwa sababu miradi inayonufaika inaonekana ni ile tu ambayo itaanza mara baada ya mabadiliko hayo na hayahusu miradi ambayo ilikuwa imekwama kutokana na vifungu hivyo. Serikali iliahidi kwenda kulifanyia kazi suala hilo ili miradi ya nyuma nayo inufaike na kukwamuliwa kutokana na msamaha huo.

**c) Ushuru wa bidhaa, SURA 147**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi kwenye marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147 na kuona kuwa marekebisho ya viwango maalum vya kodi (*specific duty rates*) vya bidhaa zisizo za petroli zinazotoka nje kwa kiwango cha mfumuko wa bei. wa **asilimia 5** yamesaidia upatikanaji wa **kiasi cha Shilingi bilioni 1.464 kati ya shlingi bilioni 3.462** ya lengo la ukusanyaji wa kodi hiyo kwa Mwaka mzima (sawa na asilimia 42 tu). Changamoto hii ya upungufu wa mapato imesababishwa na upungufu wa uagizwaji wa bidhaa toka nje kama vile bia, vinywaji baridi (Soft drinks), Pombe kali (Spirits), mvinyo, tumbaku, maji na juisi ambavyo vimesababisha lengo la makusanyo kutofikiwa katika kodi hii.

**d) Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, SURA 41.**

**Mheshimiwa Spika,** marekebisho yaliyofanyika katika kiwango cha kodi kinachotozwa kwenye michezo ya kubahatisha wa matokeo ya michezo yamesaidia upatikanaji wa mapato ya kiasi cha **Shilingi bilioni 14.851** kati ya **Shilingi bilioni 29.702** zilizotarajiwa kupatikana kwa Mwaka mzima (sawa na asilimia 50). Mwenendo huu unaonesha kuwa kodi hii imefanya vizuri na itaweza kufikia lengo la ukusanyaji kwa mwaka kama lilivyokusudiwa na Serikali.

**e) Sheria ya Usimamizi wa Kodi**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilifanya marekebisho kwenye Sheria ya Usimamizi wa Kodi na kuanzisha utaratibu maalum wa kusamehewa kodi (*Tax Amnesty*) kwa muda wa miezi sita (Julai hadi Novemba 2018) kwa ajili ya kuondoa **asilimia 100** kwenye riba na adhabu kwa wafanyabiasha wanaodaiwa. Lengo lilikuwa ni kusamehe malimbikizo ya nyuma ya riba na adhabu (Interest and penalties) na hivyo kuhamasisha ulipaji kodi kwa hiari. Hatua hii imesaidia kupokea **maombi 9,070** yenye kiasi cha kodi cha **Shilingi trilioni 1.121 na kiasi cha riba na adhabu ya Shilingi bilioni 806.166.** Mpaka sasa kiasi cha **Shilingi bilioni 201.909** kimekusanywa kama kodi ya msingi (principal tax).

Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii ya kuhamasisha ulipaji wa kodi kwa hiari na ni vema Serikali ikafiria tena kuongeza muda ili kuruhusu maombi zaidi kwa walipa kodi ambao bado wanasita kutumia fursa hii muhimu.

**f) Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2004.**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC Customs Management Act pamoja na viwango vya Ushuru wa Pamoja wa Forodha (EAC – Common External Tariff "CET") na, 2004) zilifanyiwa marekebisho ili kuendelea kulinda viwanda vinavyozalisha mafuta ya kula nchini, kutoa unafuu kwa viwanda vya uzalishaji wa bidhaa na vyakula vinavyotumia ngano; kuongeza ufanisi katika udhibiti wa kodi (electronic fiscal devices); kuziba pengo la sukari nchini; kulinda uhamasishaji wa uzalishaji wa mbegu za mafuta ya kula pamoja na kuhamasisha uzalishaji wa ndani wa viwanda vilivyopo kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki. Yafuatayo ni marekebisho yaliyofanyika: -

1) Kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 25 badala ya asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye mafuta ghafi ya kula (*Crude Oil)* yanayotambulika katika HS Code 1511.10.00. Hatua hii ililenga katika kulinda na kuhamasisha uzalishaji wa mbegu za mafuta na mafuta ya kula hapa nchini kwa kuzingatia kuwa nchi yetu ina fursa kubwa ya kuongeza uzalishaji wa bidhaa hiyo. Hata hivyo, kwa kipindi cha Julai - Desemba 2018, kiasi cha mafuta ghafi ya kula yaliyoingizwa nchini yalikuwa na thamani ya jumla ya **Shilingi bilioni 4.9 (3,150,000 Kgm)** ikilinganishwa na thamani ya jumla **bilioni 262.3 (151,837,962 Kgm)** kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2017/18 (sawa na upungufu wa asilimia 98). Kamati inaipongeza Serikali kwa kudhibiti mafuta yaliyokuwa yanaingia kama ghafi *"crude oil"* ilihali ni mafuta yaliyosafishwa *"refined oil"* na ndiyo maana uingizaji wa mafuta ghafi umeshuka na wakati huo huo uingizwaji wa mafuta yaliyosafishwa umeongezeka. Kamati inaishauri Serikali kufanya utafiti ili kubaini endapo uzalishaji wa ndani

umeongezeka au kuna kiasi kikubwa cha mafuta kinachoingia nchini kutoka katika nchi jirani.

2) Kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 10 badala ya 35 kwenye ngano (HS code 1001.99.00 na HS cde 1001.99.90) kwa mwaka mmoja. Hatua hii ilichukuliwa na Serikali ili kutoa unafuu kwa viwanda vya wazalishaji wa bidhaa na vyakula vya ngano pamoja na kuongeza uzalishaji wa bidhaa hiyo ili kukidhi mahitaji. Kamati inaona kuwa ni vema Serikali ikaweka utaratibu wa kuandaa takwimu za utekelezaji wa kodi hii na nyingine ili kuona faida ya utekelezaji wa kodi husika na lengo lililokusudiwa.

3) Marekebisho ya ushuru wa forodha kwenye mashine za kieletroniki (HS code 8470.50.00) zilizonunulia au kuingizwa nchini kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 10. yatahamasisha wafanyabiashara na wajasiliamali kuanza kutumia mashine za kieletroniki katika biashara zao. Aidha, Kamati inashauri wananchi wote kudai risiti za kieletroniki pindi wanapofanya manunuzi.

**Mheshimiwa Spika**, hii ni baadhi tu ya bidhaa zinazotozwa Ushuru wa Pamoja wa Forodha (EAC – Common External Tariff "CET") kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hata hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha Kamati inapata fursa ya kujadili na kushirikishwa kwenye mapendekezo ya Serikali kuhusu bidhaa zinazotakiwa kwenda kujadiliana kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa lengo la kupata maoni na ushauri wa Bunge kuhusu bidhaa na huduma zinazopendekezwa badala ya kuletewa matokeo ya marekebisho yaliyofanyika kwenye Sheria ya Fedha na kupitishwa na Bunge bila kujadiliwa.

### g) Mfumo wa Stempu za Kodi za Elektroniki (Electronic Tax Stamps)

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeanzisha Mfumo wa Stempu za Kodi za Kieletroniki (ETS) ulioanza kutumika tarehe 1 Septemba 2018 kwa lengo la kutumia teknolojia ya kisasa kupata taarifa sahihi za uzalishaji viwandani na kwa wakati (*real time*)

zinazotumika kupanga mipango ya maendeleo ya Taifa. Kamati ilipewa taarifa kuwa zoezi la kufunga mitambo na kufanya majaribio kwa viwanda vya awamu ya kwanza yaani sigara, pombe kali na bia limekamilika. Takribani mitambo 37 (15 kwenye viwanda vya bia na 22 kwenye sigara na pombe kali) imefungwa. Kamati inapongeza hatua hii nzuri ya Serikali ya kutumia mfumo huu, hata hivyo inaendelea kuishauri Serikali kwa sasa kutumia mfumo huu kwenye bidhaa kama vile bia, sigara, na pombe kali na kufanya tathmini ya mafanikio yake kabla ya kutumia mfumo huu kwenye bidhaa nyingine kama vile maji, soda na juisi.

**Ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi**

**Mheshimiwa Spika**, takwimu zinaonyesha kuwa katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba 2018, makusanyo ya Kodi ya Majengo kwa Halmashauri zote yalikuwa kiasi cha **Shilingi bilioni 8.41,** sawa na **asilimia 28** tu ya lengo la ukusanyaji wa mapato hayo kwa mwaka mzima. Kwa upande wa makusanyo ya kodi za mabango (billboards) kwa halmashauri zote yalifikia **Shilingi bilioni 12.30,** sawa na **asilimia 62.65** ya lengo la ukusanyaji wa kodi hiyo kwa mwaka mzima. Kamati inaona kuwa kiwango cha ukuaji wa ukusanyaji wa kodi ya majengo kimeshuka kwa **asilimia 44.5** wakati ukusanyaji wa kodi za mabango umeongezeka kwa **asilimia 64.6.**
Kamati inashauri Serikali kuongeza bidi ya ukusanyaji wa kodi ya majengo kwa kushirikiana na Halmashauri husika.

**Jedwali Na. 2 Makusanyo ya Mapato Yasiyo ya Kodi katika kipindi cha Mwezi Julai – Desemba 2018 Mwaka wa Fedha 2018/19.**

| | 2017/18 | 2018/19 | | Ufanisi (Lengo-Nusu Mwaka) | Ufanisi (Lengo Mwaka) | Ukuaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Aina ya Kodi | Makusanyo Halisi | Makadirio | Makusanyo Halisi | | | |
| Kodi ya Majengo | 15,172.0 | 13,578.7 | 8,413.6 | 62.0% | 28% | -44.5% |
| Kodi ya Mabango | 7,471.2 | 9,813.4 | 12,300.4 | 125.3% | 62.65% | 64.6% |
| **Jumla Kuu** | **22,643.22** | **23,392.10** | **20,714.01** | **88.6%** | **44.3%** | **-8.5%** |

**Chanzo:** *Wizara ya Fedha na Mipango.*

## 6.0. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KATIKA KIPINDI CHA NUSU YA KWANZA YA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 NA MWELEKEO HADI JUNI 2019.

### 6.1. Mwenendo wa Makusanyo ya Mapato

**Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonesha kuwa, katika Mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali ilipanga kukusanya jumla ya **Shilingi trilioni 32.475** kati ya fedha hizo **Shilingi trilioni 20.158** yalikuwa ni mapato ya ndani, **Shilingi bilioni 735.5** mapato ya Halmsahauri, **Shilingi trilioni 8.905** ni mikopo ya ndani kwa ajili ya kudumisha deni (Roll over) na mikopo ya kibiashara kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, Serikali ilitarajia kupokea jumla ya **Shilingi trilioni 2.130** kutoka kwa Washirika wa maendeleo ambayo inajumuisha misaada ya Kibajeti na Misaada na Mikopo ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Desemba 2018 jumla ya Mapato yote ambayo Serikali imekusanya **Shilingi trilioni 12. 839** ambayo ni sawa na asilimia 80.4 ya lengo la nusu mwaka la kukusanya **Shilingi trilioni 15.974**. Kiasi hiki kilichokusanywa ni sawa na **asilimia 39.5** tu ya lengo la kukusanya kiasi cha **Shilingi trilioni 32.475** kwa mwaka mzima. Kutofikiwa kwa makusanyo katika kipindi cha nusu mwaka kwa kiasi kikubwa kumechangiwa na kutopokelewa kwa wakati misaada na mikopo kutoka nje ambapo hadi kufikia mwezi Desemba 2018, kiasi kilichokuwa kimepokelewa na Serikali kutoka kwa wahisani kilikuwa ni **Shilingi bilioni 878.8** kati ya Shilingi **trilioni 2.676** zilizokuwa zimehaidiwa kutolewa. Jedwali namba 3 hapo chini linaonyesha mwenendo wa ukusanyaji wa Kodi kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai-Desemba) 2018/19.

**Jedwali Namba.3. Mwenendo wa makusanyo kwa kipindi cha nusu mwaka Julai-Desemba 2018 (milioni)**

| AINA YA CHANZO | A. MATARAJIO YA BAJETI | B. MALENGO YA NUSU MWAKA | C. MAKUSANYO HALISI | KIWANGO AMBACHO HAKIKUFIKIWA | ASILIMIA YA MALENGO (C/A*100) % |
|---|---|---|---|---|---|
| **Jumla ya Kodi** | **32,475.9** | **15,974.9** | **12,839.6** | **-3,135.3** | **39.5** |
| Mapato ya ndani | 20,158 | 10,176.2 | 9,225.1 | -951.1 | 45.8 |
| Mapato ya kodi | 18,000 | 8,833.1 | 7,836.3 | -996.8 | 43.5 |
| Mapato yasiyo ya kodi | 2,178.7 | 1,089.35 | 1,101.6 | +12.25 | 50.6 |
| Mikopo ya Ndani | 1,193.6 | 596.8 | 72.2 | -524.6 | 6.04 |
| Mikopo ya 'Roll Over' | 4,600.0 | 2,300.0 | 1,742.1 | -557.9 | 65.5 |
| Mikopo Masharti ya Kibiashara | 3,111.1 | 1,555.5 | 0 | 0 | 0 |
| **Mapato ya Serikali za Mitaa** | 735. | 394 | 307.2 | -86.8 | 41.8 |
| **Misaada, Mikopo Kutoka Nje** | 2,676.5 | 1,322.7 | 878.8 | -1,443.7 | 32.8 |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha na Mipango.
**Angalizo:** *Vyanzo vya mapato vinavyohusu Mikopo ya Masharti nafuu na Kibiashara kwa kiasi kikubwa vina tegemea nguvu ya soko katika upatikanaji wake.*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba kwa mwenendo huu wa ukusanyaji wa mapato Serikali inaweza kufikia makusanyo yake kati ya asilimia 80 hadi 95 na hivyo kushindwa kufikia lengo la ukusanyaji wa mapato kwa kati ya **asilimia 5** hadi **15** kwa mwaka mzima. Pamoja na hatua hii ambayo inaweza kuridhisha katika utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2018/19, Kamati inaona kwamba ipo haja ya kuongeza wigo wa ukusanyaji wa Mapato ya ndani *"Widening Tax Base"* kwa kutafuta vyanzo vipya vya mapato.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati unaonesha kuwa katika ukusanyaji wa mapato ya ndani, Kodi ya Ushuru wa Forodha inaoongoza kwa kukusanya kiasi cha **Shilingi trilioni 3.143** ikifuatiwa na Walipa Kodi wakubwa kiasi cha **Shilingi trilioni 2.980** na mwisho kodi za ndani kiasi cha **Shilingi trilioni 1.594**.

Kwa takwimu hizi, inaonesha kwamba kwa kiasi kikubwa mapato yetu yanategemea biashara za Kimataifa *"International Trade"* na wafanya biashara wakubwa. Hivyo

ni lazima Serikali kuhakikisha kwamba inachukua hatua za makusudi ili kuongeza mauzo yetu nje ya nchi pamoja na kuweka mazingira wezeshi kwa nchi jirani kuendelea kutumia Bandari zetu ili kupata mapato mengi zaidi. Hatua yoyote ya kikodi ama kisera inayoathiri mauzo yetu nje ya nchi ama inaathiri mazingira ya matumizi ya bandari zetu na wafanyabiashara wakubwa ni lazima iangaliwe kwa umakini mkubwa.

**Jedwali Namba 4. Makusanyo ya kodi katika kipindi cha nusu mwaka 2018/19**

| Na | MWENENDO WA MAKUSANYO YA KODI KATIKA KIPINDI CHA NUSU MWAKA | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Kodi za Nani | 1,995,333.10 | 1,703,404.80 |
| 2. | Walipa Kodi wakubwa | 3,447,750.20 | 3,046,468.20 |
| 3 | Ushuru wa Forodha | 3,430,786.80 | 3,105,641.00 |
| 4 | **JUMLA** | **8,873,870.10** | **7,885,511.00** |

***Chanzo:*** *Wizara ya Fedha na Mipango.*

**Mheshimiwa Spika**, takwimu zinaonesha kuwa baadhi ya vyanzo vya ndani vya vya kikodi na visivyo vya kikodi havijaweza kutusaidia kupata mapato yanayostahili na hivyo kutoweza kutosheleza katika ugharamiaji wa miradi ya maendeleo. Hali kadhilika, mategemeo ya Serikali kupata fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo yamekuwa hafifu na wakati mwingine masharti yao yamekuwa yakibadilika badilika.

Hivyo, ili tuwe na uhuru wa kweli katika kutekeleza Bajeti ya Serikali, lazima Serikali iongeze juhudi ya upatikanji wa mapato badala ya kuhusisha wahisani katika upangaji wa Bajeti ya Serikali. Hatua hii itawezekana tu kwa kuchochea ukuaji na uzalishaji kwenye shughuli za kiuchumi zinazowahusisha wananchi walio wengi na hivyo kupata mapato yanayojitosheleza kupitia shughuli hizo.

## 6.2. Mwenendo wa Matumizi

### 6.2.1. Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inatumia mfumo wa "*Cash Budget"* ambapo kiasi cha fedha kinachokusanywa ndio kiasi ambacho kinatumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Maendeleo. Katika kipindi cha nusu mwaka Serikali ilitumia jumla ya kiasi cha **Shilingi trilioni 12.839** kati ya **Shilingi trilioni 20.468** zilizoidhinishwa na Bunge kwenye matumizi ya kawaida (kiasi hiki ni sawa na **asilimia 62.72**)

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hatua hii nzuri ya utolewaji wa fedha, Kamati imebaini kuna baadhi ya Mafungu yamepokea zaidi ya malengo yaliyopangwa katika kipindi cha nusu mwaka; Mfano Tume ya Mahakama (asulimia 104), Msajili wa Vyama vya Siasa (asilimia110), Kitengo cha Kuzuia fedha Haramu (asilimia114), Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (asilimia 104) Tume ya Mabadiliko ya Sheria (asilimia 338) na Hazina (asilimia 286), Muhasibu Mkuu (asilimia 134) na Tume ya Uchaguzi (asilimia 674). Aidha, Kamati imebaini kuwa Mafungu ya Msajili wa Hazina na Wizara ya Maliasili yamepewa chini ya asilimia 50. Kamati inashauri Serikali kuangalia mtiriko wa fedha "Cash flow Plan" kwa mafungu husika ili kusiathiri utekelezaji wa Bajeti kwa mafungu mengine.

**Jedwali Namba 5: Ulinganisho wa Sura ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2018/19 (Bilioni) na utolewaji wa fedha katika kipindi cha Nusu Mwaka 2018/19.**

| Na | | 2018/19 | 2018/19 | TOFAUTI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| | MAPATO | BAJETI | FEDHA ILIYOTOLEWA NUSU MWAKA | KIASI KILICHOBAKIA | ULINGANISHO MWAKA MZIMA |
| | MATUMIZI | C1 | C2 | C3(C1-C2) | |
| 1 | **Matumizi ya Kawaida** | **20,468,676** | **12,839.6** | **7,629.076** | **62.72** |
| | **o/w(i) Deni la Taifa** | **10,004,480** | **4,775.9** | **5,228.58** | 47.73 |
| | • Malipo ya Riba Ndani | 1,413,631 | 1,950.4 | 4,063.53 | 32.43 |
| | • Malipo ya Mtaji Ndani (Rollover) | 4,600,000 | | | |
| | • Malipo ya Riba na Mtaji Nje | 2,359,320 | 1,269.2 | 1,090.12 | 53.79 |
| | • Matumizi Mengine ya Mfuko Mkuu | 435,663 | 796.7 | -334.04 | 182.87* |
| | **(ii) Mshahara** | **7,369,731** | **3,311** | **4,058.7** | **44.76** |
| | **(iii) Matumizi Mengineyo (OC)** | **3,094,465** | **1,756.9** | **1,337.56** | **56.77** |
| 2 | **Matumizi ya Maendeleo** | **12,007,273** | **2,995.8** | **9,011.4** | **24** |
| | • Fedha za Ndani | 9,876,393 | 2,530.8 | 7,345.59 | 25 |
| | • o/w Matumizi ya Halmashauri | 345,727 | 184.3 | 161.42 | 53.30 |
| | • Fedha za Nje | 2,130,880 | 280.6 | 1850.28 | 13.16 |
| | **JUMLA YOTE** | **32,475,950** | | | |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa katika kipindi cha nusu mwaka 2018/19, kiasi cha **Shilingi trilioni 12.839** ya mapato yote yaliyokusanywa; Kiasi cha **Shilingi trilioni 4.77** (**sawa na asilimia 37.1**) yalitumika katika kugharamia ulipaji wa deni la Taifa pamoja na riba ya madeni yaliyoiva. Aidha, kiasi cha **Shilingi trilioni 3.311** kilitumika katika kulipia Mishahara

(**sawa asilimia 25.6**). Mwenendo huu unaonesha kuwa kiasi cha fedha cha Shilingi **trilioni 8.081** kimetumika katika ulipaji wa Deni la Taifa na Mishahara tu na kinachobakia (**Shilingi trilioni 4.749**) kimetumika katika matumizi mengineyo na maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** tathmini ya uhimilivu wa Deni iliyofanyika inaonyesha kuwa vigezo vyote vya Deni la Taifa ni himilivu ukilinganisha na nchi nyingine za jirani ambazo ama zinakaribia ukomo au zimevuka vigezo vilivyowekwa. Kamati inatambua kwamba Serikali inaongozwa na Sheria ya Mikopo Dhamana na Misaada Sura ya 134, hata hivyo Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha haivuki viwango vilivyowekwa kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona kuwa mwenendo wa utolewaji wa fedha kwenye matumizi mengineyo na miradi ya maendeleo sio wa kuridhisha. Mathalani, kati ya **Mafungu 92** ya Serikali ni mafungu 14 tu yaliyopokea fedha za maendeleo zaidi ya **asilimia 50** ikiongozwa na Wizara ya mambo ya ndani ambayo imepokea **asilimia 228**. Aidha kamati imebaini kwamba mafungu ya Sekta ambazo ni za huduma hasa kwa wananchi yamepokea fedha chini ya **asilimia 50**. Mafungu hayo ni Maji **asilimia 11.0,** Wizara ya Afya **asilimia14.66**, Wizara ya Elimu **asilimia 37.68,** Kilimo **asilimia 41.43** na Wizara ya Mifugo **asilimia 39.6.** Mwenendo huu ukilinganisha na kasi ya ongezeko la watu ni wazi kwamba haviendani sambamba hivyo kuna haja ya Serikali kuzipa kipaumbele sekta hizi katika mgao wa fedha za maendeleo.

## 7.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA JUMLA

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha Nusu Mwaka 2018/2019 pamoja na utekelezaji wa majukumu ya Kamati, Kamati ina maoni na mapendekezo ya ujumla yafuatayo:

**7.1.** **Mheshimiwa Spika**, **KWA KUWA** Serikali ilikubali kutoa **Shilingi bilioni 38.9** kwa ajili ya miradi ya Afya na **Shilingi bilioni 29.7** kwa ajili ya umaliziaji wa miradi ya elimu. **NA KWA KUWA**

hatua hii imekuwa na mafanikio kwa upande wa afya wakati miradi ya elimu imekwama utekelezaji na endapo ahadi hii ya Serikali haitatekelezwa itawakatisha tamaa wananchi kuchangia katika miradi ya maendeleo kwa siku zijazo. **HIVYO BASI,** Kamati inaendelea kusisistiza Serikali kuhakikisha inatoa kiasi kilichobaki ili kufikia **Shilingi bilioni 251** ambazo zilikuwa zinahitajika kwa ajili ya kukamilisha maboma hayo.

**7.2.** **Mheshimiwa Spika**, **KWA KUWA** katika kipindi cha Julai hadi Desemba mwaka 2018/2019, makusanyo ya mapato ya kodi yamekua kwa **asilimia 2** kutoka **Shilingi trilioni 7.678** hadi **Shilingi trilioni 7.836** katika ukilinganisha na kipindi kama hicho mwaka 2017/2018**. NA KWAKUWA** Katika mwaka 2018/2019 mapato ya Serikali yalitarajiwa kukua kwa **asilimia 18**. **HIVYO BASI,** Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya makusanyo ya mapato katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka (Januari – Juni, 2019) ili kufikia lengo.

**7.3.** **Mheshimiwa Spika**, **KWA KUWA** kila mwaka Serikali hupitia Sheria mbalimbali za Kodi pamoja na kuangalia Sera za Mapato. **NA KWA KUWA** Serikali imeonyesha ufanisi katika ukusanyaji wa vyanzo vilivyopo. **HIVYO BASI,** kamati inaishauri Serikali kuangalia sera na mikakati ya kuongeza mapato ya ndani hasa kwa kupanua wigo wa kodi pamoja na kubuni na kutafuta vyanzo vipya vya mapato pamoja na kuimarisha ukusanyaji wa vyanzo vilivyopo.

**7.4.** **Mheshimiwa Spika**, **KWA KUWA** takwimu za makusanyo zinaonesha kuwa baadhi ya Wizara na Idara za Serikali zinafanya vizuri katika kukusanya maduhuli. **NA KWA KUWA** bado juhudi inahitajika zaidi ili kuhakikisha mapato zaidi yanapatikana katika ukusanyaji wa maduhuli. **HIVYO BASI,** Ni vema Serikali ikasimamia ipasavyo malengo ya makusanyo yanayowekwa pamoja na jitihada inayowekwa katika kufikia malengo husika.

**7.5.** **Mheshimiwa Spika**, **KWA KUWA** Serikali bado haijaweza kufanya vizuri katika utolewaji wa fedha za ndani kwenye matumizi ya maendeleo kutokana na upungufu wa mapato. **NA KWA KUWA** fedha za nje Wahisani wa

maendeleo zimepokelewa kwa **asilimia 13.16** tu ya fedha zote zilizoahidiwa. **HIVYO BASI,** Kamati inashauri Serikali kuendelea kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano na Wahisani *(DCF- Development Corporation Framework)* ili kuimarisha uhusiano utakaosaidia kupatikana kwa fedha hizo kwasababu bado kama Taifa tunazihitaji.

**7.6.** **Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Serikali iliweka utaratibu wa kutoza amana ya **asilimia 15** pindi wamiliki wa viwanda wanapoagiza Sukari ya viwandani kutoka nje. **NA KWA KUWA** fedha hizo zilitakiwa kurejeshwa kwa wamiliki wa viwanda pindi uhakiki wa matumizi ya Sukari unapomalizika. **HIVYO BASI** Kamati inaishauri Serikali kutumia "*Escrow*" akaunti ambayo tayari imekwisha funguliwa kwa ajili ya kuhifadhi amana hizo ili pindi uhakiki unapokamilika fedha hizo zirejeshwe kwa wakati.

**7.7.** **Mheshimiwa Spika**, **KWA KUWA** katika utekelezaji wa bajeti katika kipindi cha nusu mwaka, sekta za kilimo, uvuvi na ufugaji zimepata fedha za maendeleo chini ya **asilimia 40**. **NA KWA KUWA** Sekta hizi zinaajiri takribani asilimia 70 ya watanzania na ndizo zinazalisha malighafi ya Viwandani. **HIVYO BASI** Kamati inashauri Serikali kuelekeza fedha kwenye sekta hizo ili kuchochea ukuaji wa uchumi wa viwanda, kupanua fursa ya ajira na kuboresha miundombinu ya uchumi na kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za jamii.

**7.8.** **Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Kamati imebaini kwamba hatua ya Serikali ya kusamehe riba na adhabu zitokanazo na makosa ya Kodi *"Tax Amnesty"* imeonyesha mafanikio makubwa sana na Serikali imefanikiwa kukusanya zaidi ya Shilingi bilioni 200 hatua hii ni ya kupongezwa. **HIVYO BASI** Kamati inashauri yafuatayo ili kiasi cha **Shilingi bilioni 720.6** ziweze kupatikana katika kipindi cha nusu ya pili cha mwaka 2018/2019.

i) Kwanza, kuharakisha kushughulikia **maombi 3,371** yaliyobaki katika **maombi 9,070** yaliyopokelewa; na

ii) Pili, kuharakisha kusikiliza kesi za kodi ambazo ziko kwenye ngazi ya Bodi na Bodi ya Rufaa;

**7.9. Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Serikali imekusanya chini ya **asilimia 35** ya kodi ya majengo kwa Halmashauri zote nchini. NA KWA KUWA kuna baadhi ya Halmashauri ambazo Serikali haijaweza kukusanya kiasi chochote kutokana na ukweli kwamba kodi hii inalipwa mara moja kwa mwaka na inatarajiwa kulipwa mwishoni mwa mwaka, **HIVYO BASI** Kamati ina mapendekezo yafuatayo: -

i) Kwa maeneo ambayo TRA hawajaweza kuyafikia kutokana na uwezo mdogo wa rasilimali watu na fedha ni vema wakaingia mikataba ya ufanisi (performance contract) na Halmashauri ili zikusanye kwa niaba yake;

ii) Kodi hii iruhusiwe kulipwa kwa awamu yaani *"Installment"* ili mapato yanayopatikana yatumike katika mwaka husika na si kusubiria hadi mwisho wa mwaka; na

iii) Kutumia teknolojia ya *satellite* kutambua nyumba zilipo ili kurahisiha ukusanyaji wa kodi hii.

**7.10. Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** michezo ya kubahatisha imekuwa ikikua kwa kasi sana nchini, aidha michezo hii kwa asili yake si ya kiuzalishaji hivyo haina mlolongo wa thamani (value chain). **NA KWA KUWA** michezo nchini inaendeshwa kwa mujibu wa sheria, michezo hii ina madhara makubwa sana kwa Taifa. **HIVYO BASI,** Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuongeza kodi kwenye mapato anayopata mchezaji *"Tax on wining"* ili kupata mapato zaidi na wakati huo huo kupunguza ushiriki. Vilevile Serikali inaweza kuweka kiwango cha dau la chini *"minimum bets"* ambalo mshiriki atapaswa kuwa nalo ili aweze kushiriki michezo hizo. Kinyume na ilivyo hivi sasa ambapo kiwango cha chini ni Shilingi 500 ambacho hata mtoto chini ya miaka 18 anaweza kukipata.

**7.11. Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Serikali imeanzisha mfumo wa Akaunti Jumuifu ya Fedha (TSA). **NA KWA KUWA** mfumo huo bado unakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile ucheleweshwaji wa malipo kutokana na kukosekana kwa mtandao wa uhakika *"Network"* pamoja

na uwepo kwa mkongo wa Taifa. **HIVYO BASI** Kamati inashauri Serikali kuhakikisha upatikanaji wa mtandao wa uhakika ili kuleta ufanisi.

**7.12. Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** utekelezaji wa Bajeti katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka wa fedha huwa haiwasilishwi Bungeni na badala yake huwasilishwa miezi minne tu hadi mwezi Aprili pindi Waziri wa fedha anapowasilisha Bajeti ya Serikali. **NA KWA KUWA** Kamati ya Bajeti na Bunge halipati nafasi ya kujadili utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika kipindi cha nusu ya pili ya Mwaka wa fedha Januari - Juni. **HIVYO BASI**, Kamati inaishauri Serikali kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka yaani January- June kati ya mwezi wa nane na wa tisa kila mwaka ili kamati ipate fursa ya kuishauri Serikali kikamilifu.

7.13. Mheshimiwa Spika, **KWA KUWA** Mabadiliko yanayofanywa na Baraza la Mawaziri wa Fedha, Uwekezaji na Biashara wa Afrika Mashariki hayawezi kubadilishwa na Bunge na badala yake hupitishwa kama yalivyoletwa kwa sababu hakuna Sheria wala Kanuni inayomlazimisha Waziri wa Fedha kuyapitisha kwenye kamati kwa niaba ya Bunge ama kuyaleta Bungeni kabla ya kwenda katika vikao vya Afrika Mashariki. **NA KWA KUWA** mabadiliko hayo mara nyinginye huleta athari kwa Sekta Binafsi nchini. **HIVYO BASI,** Kamati inalishauri Bunge lako kutunga kanuni itakayomtaka Waziri wa Fedha kuyawasilisha Mapendekezo hayo kwenye Kamati au Bungeni kabla ya kuyapeleka katika Vikao vya maamuzi vya Afrika Mashariki.

## 8.0. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa miongozo yenu ambayo mmekuwa mkitupatia Wabunge. Namshukuru Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip I. Mpango, Mb na Naibu Waziri Dkt. Ashatu Kijaji kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Nawashukuru pia wataalam wote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ambao walishirikiana na Kamati katika

hatua zote za kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha Nusu mwaka 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa ushauri na maoni mbalimbali yaliyohusu Taarifa hiyo. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifauatavyo: -

1. Mhe. George Boniface Simbachawene, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. David Ernest Silinde, Mb
4. Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mb
5. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
6. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
7. Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
8. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb
9. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb
10. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
11. Mhe. Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mb
12. Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
13. Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mb
14. Mhe. Abdallah Majurah Bulembo, Mb
15. Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mb
16. Mhe. Stephen Julius Masele, Mb
17. Mhe. Ali Hassan Omar, Mb
18. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
19. Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mb
20. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb
21. Mhe. Marwa Ryoba Chacha, Mb
22. Mhe. Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, Mb
23. Mhe. Andrew John Chenge, Mb
24. Mhe. Hussein Mohamed Bashe, Mb
25. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb
26. Mhe. Suleiman Ahmed Saddiq, Mb

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee kabisa, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Ndg. Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake katika kipindi chote. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Kaimu

Mkurugenzi Ndg. Lina Kitosi, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Michael Kadebe na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Godfrey Godwin, Emmanuel Rhobi, Maombi Kakozi na Lilian Masabala kwa kuratibu shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

George B. Simbachawene, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**
2 Februari, 2019

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na taarifa ya pili, namkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Karibu sana Mheshimiwa Chegeni.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI NA MITAJI YA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa yangu yote kama iliyoko hapa mezani iweze kuwa ndio taarifa rasmi kwa ajili ya *Hansard* ya Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji Mitaji ya Umma kwa mwaka 2018 na kuliomba Bunge lako Tukufu kuipokea na kuijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma imetekeleza majukumu yake ya kufuatilia uwekezaji katika mashirika taasisi za umma na makampuni ambayo Serikali ina hisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Kamati; katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Kanuni ya 12 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni ya Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, yako kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli zilizotekelezwa; katika kipindi cha mwaka kuanzia Januari, 2018 hadi Januari, 2019, Kamati ilitekeleza majukumu yake kwa njia ya kufanya vikao na kupokea, kuchambua na kujadili taarifa za taasisi na Mashirika ya Umma kuhusu uwekezaji unaotekelezwa na taasisi hizo. Aidha, Kamati imefanya ziara katika baadhi ya taasisi za umma ili kujiridhisha na iwapo uwekezaji unaofanywa na taasisi hizo una tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa uwekezaji wa mitaji ya umma na matokeo yake; kamati imekuwa ikifuatilia uwekezaji wa mitaji ya umma ambapo katika mwaka wa fedha 2017/2018, thamani ya uwekezaji wa Serikali wa ndani ya nchi katika taasisi 270 ulifikia jumla ya trilioni 55.17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa ya Msajili wa Hazina umeonesha kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018, Serikali imefanya uwekezaji uliofikia trilioni 54.48 katika taasisi na mashirika ambayo Serikali ina umiliki zaidi wa asilimia 50. Vilevile Serikali imewekeza jumla ya shilingi bilioni 696 katika makampuni ambayo umiliki wake wa hisa ni asilimia 50 na pungufu. Aidha, katika mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2018 Serikali ilipata faida ya mapato yasiyo ya kodi jumla ya shilingi bilioni 637 kutokana na uwekezaji uliofanywa katika taasisi na mashirika ya umma ambayo Serikali inaumiliki wa zaidi wa asilimia 50. Vilevile Serikali ilipata gawio la shilingi bilioni 35.96 kutokana na uwekezaji katika makampuni ambayo Serikali ina umiliki wa hisa wa asilimia 50 na pungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imefanya uwekezaji uliofikia jumla ya shilingi bilioni 580 katika mashirika 10 yaliyo nje ya nchi. Aidha, kutokana na uwekezaji uliofanyika katika taasisi hizo Serikali inatarajia kupokea kiasi cha dola la za Kimarekani 128,000 kutoka katika Kampuni ya

*Africa Insurance Corporation*. Aidha, fedha hizo bado hazijapokelewa na Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchambuzi wa kina uliofanywa na Kamati umebaini kuwa uwekezaji wa ndani wa Serikali umeongezeka kwa asilimia 13.7, kutoka shilingi trilioni 44.53 kwa mwaka 2016/2017 hadi shilingi trilioni 55.17 katika mwaka wa fedha 2017/2018. Aidha, faida inayotokana na uwekezaji huo imepungua kwa asilimia 23.95 kutoka shilingi bilioni 885 mwaka 2016/2017 hadi shilingi bilioni 673 mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018, Serikali imewekeza katika Taasisi na Mashirika ya Umma yenye umiliki wa zaidi ya asilimia 50 wenye jumla ya shilingi trilioni 54.48 na kupata faida ya shilingi bilioni 637, faida iliyopatikana ni sawa na asilimia 1.17 ya uwekezaji uliyofanyika. Hivyo, Serikali iliwekeza katika makampuni ambayo inaumilikiwa wa hisa 50 na pungufu yenye jumla ya shilingi bilioni 696 na kupata faida kwa njia ya gawio la shilingi bilioni 35.9. Aidha, faida iliyopatikana ni sawa na asilimi 5.17 ya uwekezaji uliyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa uwekezaji. Kutokana na dhima ya Serikali kuwekeza katika mashirika, Kamati ilifuatilia uwekezaji huo wa mitaji ya umma kwa kufanya uchambuzi na kubaini mambo makuu yafuatayo:-

(i) Kukosekana kwa Sera ya Gawio. Sera ya Gawio ni mwongozo unaotengenezwa kwa lengo la kuweka bayana mgawanyo wa faida baada ya kodi. Mwongozo huo huonesha kiasi cha asilimia ambacho kinapaswa kutolewa kwa wana hisa na kiasi kinachopaswa kuwekezwa katika kuendeshaji wa biashara kwa kuzingatia mpango wa biashara wa taasisi na mashirika ya umma na makampuni ambayo Serikali ina hisa. Mwongozo huo unabainisha ni kiasi gani Serikali inapaswa kutoa gawio. Katika uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Taasisi na mashirika ya umma yaliyo mengi hayana Sera ya Gawio hali iliyosababisha taasisi hizo

kukosa nyenzo muhimu za kuipatia Serikali mapato kwa kuwa ni mwana hisa katika taasisi hizo.

(ii) Utegemezi mkubwa wa ruzuku ya Serikali. Katika kupitia taarifa za taasisi na mashirika ya umma, Kamati imebaini kuwa zipo baadhi ya taasisi zinashindwa kutumia ipasavyo rasilimali zake kwa ajili ya kujiongezea mapato bila kutoka katika kujukumu lao la msingi. Kushindwa kuongeza juhudi katika upatikanaji wa fedha kunasababisha taasisi hizo kutegemea kwa kiasi kikubwa ruzuku kutoka Serikalini. Iwapo taasisi na mashirika ya umma yatajikita katika majukumu yake ya msingi yatajiendesha kibiashara pamoja na kujitegemea na kuzalisha mapato ya kutosha katika kuendeshaji wa shughuli zake.

(iii) Ukosefu wa Sera ya Uwekezaji, Mpango Mkakati na Mpango wa Kibiashara kwa taasisi zinazofanya uwekezaji. Taasisi na mashirika ya umma, yanatakiwa kuwa na nyaraka mbalimbali ili taasisi hizo ziweze kujiendesha kibiashara kwa kuwa na ufanisi wa kutosha. Kukosekana kwa nyaraka hizo kunazifanya taasisi za umma kukosa nguzo muhimu katika uendeshaji wake. Nyaraka hizo ambazo ni nguzo katika utekelezaji wa majukumu ya taasisi ni Sera ya Uwekezaji *(Investment Policy),* Mpango Mkakati *(Strategic Plan)* na Mpango wa Kibiashara *(Business Plan).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Uwekezaji ni mwongozo unaoandaliwa kwa kampuni na mashirika yanayofanya biashara hasa ambayo mapato yake yanategemea kwa kiwango kikubwa uwekezaji unaofanyika katika makundi mbalimbali. Lengo la sera hii ni kupunguza vihatarishi vinavyotokana na kuwa na uwekezaji mkubwa katika kundi moja yaani (*portfolio risk).* Kamati imebaini baadhi ya taasisi ambazo ziko katika kundi hili kutokuwa na Sera ya Uwekezaji hali inayosababisha upotevu wa fedha za umma zilizowekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia imebaini baadhi ya taasisi za umma kutokuwa na Mpango Mkakati au kuwa na Mpango Mkakati uliokwisha muda wake. Taasisi na

mashirika ya umma yanatakiwa kuwa na mpango mkakati utakaosaidia kutekeleza mpango wa maendeleo wa Taifa katika lengo lake la kisheria yaani *mandate*.

(iv) Upungufu wa mitaji pamoja na fedha za utekelezaji wa miradi ya uwekezaji. Kamati inapenda kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli, kwa jitihada za kufufua baadhi ya mashirika ya umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kurudia. Kamati inapenda kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kwa jitihada za kufufua baadhi ya mashirika ya umma hali itakayochachua sekta nyingi za kiuchumi na hatimaye kuinua uchumi wa nchi yetu. Uboreshaji wa Shirika la Ndege, kwa mfano Air Tanzania, uliohusisha pamoja na mambo mengine ununuzi wa ndege sita kwa sasa ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha *SGR* na maeneo mengine mbalimbali ambayo Serikali imefanya uwekezaji ni maeneo ya kutolea mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizi za Serikali, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa bado kuna changamoto kubwa ya ukosefu wa mitaji wa baadhi ya taasisi na mashirika ya umma. Serikali kushindwa kukamilisha jukumu lake la kupeleka mitaji katika taasisi zake, kunasababishia taasisi hizo kushindwa kutekeleza majukumu yake ya kimsingi kwa ufanisi na kwa kutoleta tija inayotarajiwa. Mfano taasisi zenye upungufu wa mitaji ni Benki ya Posta Tanzania, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania, Shirika la Mawasiliano Tanzania *(TTCL),* Kampuni ya Huduma za Meli, Shirika la Posta *(TPC)* na Benki ya Maendeleo ya *TIB*. Ufafanuzi zaidi kuhusu taasisi zenye uhapa wa mtaji unapatikana katika Taarifa ya Kamati.

(v) Ukiukwaji wa Sheria ya Fedha Na. 16 ya mwaka 2015, kifungu cha 46. Taasisi za umma zinatakiwa kudhibiti matumizi yake ya gharama za uendeshaji na kutokuzidi asilimia 60 kama Sheria ya Fedha Na.16 ya 2015, kifungu cha 46(10)(A)(1) inavyotamka. Aidha, Kamati

imebaini uwepo wa baadhi ya taasisi kukiuka matakwa ya sheria kwa kuwa matumizi mkubwa yanayosababisha taasisi kukosa faida na kushindwa kutoa gawio au kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Mfano wa taasisi zinazobainika kuwa na matumizi makubwa ni Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC),* Kampuni ya Mbolea Tanzania *(TFC)* na Shirika la Taifa la Maendeleo *(NDC). (Makofi)*

(vi) Utekelezaji wa miradi ya uwekezaji kwa baadhi ya ya taasisi za umma. Katika uchambuzi wa taarifa ya uwekezaji wa taasisi na mashirika ya umma, Kamati imebaini zipo taasisi zina miradi na shughuli nyingi zenye fursa kubwa ya kuchangia katika uchumi na ustawi wa Taifa. Hata hivyo, shughuli/miradi mingi haitengewi rasilimali za kutosha katika kuitekeleza kwa wakati. Kwa mfano, Shirika la Maendeleo ya Taifa *(NDC)* ni taasisi ya kimkakati ambayo miradi yake ya kielelezo imewekwa chini yake ili itekelezwe. Pamoja na wingi wa miradi tena yenye uwezekano mkubwa wa kutekelezwa kwa tija hakuna rasilimali na mikakati ya kutekeleza miradi hiyo kwa wakati.

(vii) Taasisi kushindwa kutekeleza Sera na Miongozo ya Ushiriki wa Sekta Binafsi na Sekta Ya Umma *(PPP).* Kamati ya Uwekezaji imekuwa ikiangalia utekelezaji wa miradi ya uwekezaji wa umma kama ina tija na inazingatia taratibu na sheria za kibiashara. Pamoja na mambo mengine, Kamati imebaini kusuasua kwa utekelezaji wa miradi kwa baadhi ya taasisi kutokana na ukosefu wa fedha za uendeshaji wa miradi hiyo. Hata hivyo, changamoto hiyo inaweza kutatuliwa iwapo taasisi za Serikali zitaingia ubia na sekta binafsi *(PPP)* katika uwekezaji wa miradi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikishwaji wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi mbalimbali utachangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi na kuipunguzia Serikali mzigo wa kuendesha miradi yote nchini. Uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kuwa taasisi na mashirika ya umma yamekuwa yakishindwa kutekeleza miradi ya uwekezaji kwa kuwa yamekuwa yakitegemea kwa kiasi kikubwa fedha kutoka Serikalini, ambapo fedha hizo zimekuwa hazipelekwi

kwa wakati katika taasisi hizo na hivyo kusababisha ucheleweshwaji wa miradi hiyo mingi. Hivyo basi, suluhisho la ukosefu wa fedha za uendeshaji wa miradi kwa taasisi za umma ni kuingia ubia na sekta binafsi ili utekelezaji wa miradi hiyo ufanyike kwa wakati na kwa ufanisi.

(viii) Uwepo wa baadhi ya sheria zinazoanzisha taasisi na mashirika ya umma kutoendana na wakati wa sasa. Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini uwepo wa baadhi ya taasisi na mashirika ya umma kutumia sheria zilizopitwa na wakati na hivyo kuzifanya taasisi hizo kushindwa kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa ukamilifu. Aidha, baadhi ya taasisi zinashindwa kuingia katika soko la ushindani wa kibiashara kwa kuwa sheria zilizoanzisha taasisi hizo haziendani na mazingira ya sasa ya kibiashara. Mfano wa taasisi ambazo sheria yake imepitwa na wakati, ni Mamlaka ya Chakula na Dawa *(TFDA)* na Kampuni ya Huduma ya Meli.

(ix) Serikali kuchelewa kulipa madeni kwa taasisi zake. Narudia, Serikali kuchelewa kulipa madeni kwa taasisi zake. Kumekuwa desturi ya taasisi za Serikali na baadhi ya Wizara kutolipa madeni yake baada ya kupata huduma kutoka katika taasisi hizi za umma. Kutokulipia huduma hizo, kunasababisha mrundikano wa madeni ya umma ya muda mrefu yanayochangia taasisi nyingi kushindwa kujiendesha pamoja na kushindwa kutekeleza miradi ya uwekezaji kutokana na kukosekana kwa fedha. Mfano, taasisi ambazo zinadai madeni makubwa ni *TANESCO*, *TEMESA*, *TTCL*, Shirika la Posta Tanzania kama ilivyofafanuliwa katika taarifa ya Kamati na mengine mengi. *(Makofi)*

(x) Ukosefu wa ufanisi katika uendeshaji wa taasisi za umma. Kamati imefanya uchambuzi katika eneo la utendaji na uendeshaji wa taasisi na mashirika ya umma kwa lengo la kubaini maeneo ambayo kama yakiboreshwa kunaweza kupatikana tija kubwa. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa maeneo ambayo yanapunguza ufanisi wa taasisi ni pamoja na mwingiliano wa mamlaka ya Serikali. Mapungufu katika matumizi mazuri ya TEHAMA, kutokamilika kwa ikama ya watumishi pamoja na ujuzi na weledi. Mfano

wa maeneo ambayo Kamati imeona yanapunguza ufanisi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania ni pamoja na mwingiliano wa mamlaka ya Serikali, mapungufu katika matumizi mazuri ya TEHAMA na ushirikiano kati ya wadau wakuu wa bandari *(port community).*

(xi) Baadhi ya Bodi za Wakurugenzi na taasisi kutokuwa hai. Bodi za Wakurugenzi ndizo zinazosimamia taasisi na mashirika ya umma kwa niaba ya Serikali. Bodi hizo zimekuwa na majukumu mbalimbali ikwemo kusimamia utendaji wa mashirika na taasisi za umma; kuchambua na kupitisha nyaraka za sera na kuwasilisha Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa uchambuzi; kuingia mikataba ya kiutendaji na Mtendaji Mkuu na kuhakikisha malengo yaliyokubaliwa yanatekelezwa; na kuidhinisha na kufuatilia miradi ya uwekezaji katika mashirika. Kwa muktadha huo, kukosekana kwa Bodi ya Wakurugenzi kunasababisha taasisi na mashirika ya umma kuwa na utendaji usioridhisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amekuwa akifanya teuzi nyingi sana za Wenyeviti mbalimbali wa Bodi ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na usimamizi mkubwa katika taasisi na mashirika ya umma. Changamoto kubwa iliyopo ni kuchelewa kwa uteuzi wa Wajumbe wa Bodi ambao wamekuwa wakiteuliwa na Wizara husika. Naomba nirudie hapa, Mheshimiwa Rais amekuwa akifanya teuzi nyingi sana za Wenyeviti mbalimbali wa Bodi ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na usimamizi mkubwa katika taasisi na mashirika ya umma. Changamoto kubwa iliyopo ni kuchelewa kwa uteuzi wa Wajumbe wa Bodi ambao wamekuwa wakiteuliwa na Wizara husika. Vilevile Serikali inatakiwa kuwa na mpango wa muendelezo yaani *(succession plan)* katika uteuzi wa Wajumbe wa Bodi na Taasisi za Umma ili ukomo wa ujumbe katika Bodi hizo usimalizike kwa wakati mmoja.

(xii) Utendaji wa Ofisi ya Msajili wa Hazina. Kwa mujibu wa Kanuni ya 12 ya Nyongeza ya 8(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati hii pamoja na majukumu mengine inajukumu la kuchambua na kujadili taarifa za mwaka na Msajili wa Hazina na Mashirika ya Umma

na Kampuni ambazo Serikali ina hisa. Kamati inapenda kutoa taarifa kuwa kwa kipindi chote cha uhai wa Bunge la Kumi na Moja, haijapokea taarifa ya mwaka ya Msajili wa Hazina hali ambayo inafanya utendaji wa kazi wa Kamati uwe mgumu. Hii ni kutokana na ukweli kuwa kama ilivyoelezwa kwenye Kanuni iliyoelezwa hapo juu, taarifa hizo ndiyo msingi wa shughuli za Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Msajili wa Hazina ina jukumu la kusimamia taasisi na mashirika ya umma yapatayo 270. Tathmini ya Kamati imebaini kuwa upungufu wa ikama ya watumishi na matumizi duni ya TEHAMA ndiyo chanzo kikubwa cha kutokufanyika hili. Maoni ya Kamati ni kuwa ili Ofisi hii iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu, inapaswa kuwa na watendaji wa kutosha na wenye ujuzi na weledi katika mambo wanayosimamia pamoja na mfumo mzima wa TEHAMA utakaowezesha kuwasiliana na mashirika ya umma mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo ya Kamati. Kutokana na uchambuzi uliofanywa na Kamati, maoni ya jumla ya Kamati kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma yamefafanuliwa katika taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo. Baada ya kutoa maoni ya jumla ya Kamati yaliyotokana na uchambuzi wa mitaji ya umma, naomba kutoa mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

(i) Kukosekana kwa Sera ya Gawio *(Dividend Policy).* Kwa kuwa Sera ya Gawio ni mwongozo unaoweka bayana mgawanyo wa faida baada ya kodi na kiasi cha asilimia ambacho kinapaswa kutolewa kwa wanahisa na kiasi kinachopaswa kuelekezwa kwenye uendelezaji wa biashara na taasisi;

Na kwa kuwa kukosekana kwa sera hiyo kunasababisha taasisi na mashirika ya umma kukosa nyenzo muhimu ya kuipatia Serikali mapato kwa sababu viongozi wa taasisi wamekuwa wakiamua na kujipangia kiasi cha gawio

cha kupeleka Serikalini hata kama kiasi hicho hakiendani na kiwango cha uwekezaji uliofanywa na Serikali na faida iliyopatikana kwa taasisi;

Kwa hiyo basi, Bunge linashauri kuwa Serikali kupitia Msajili wa Hazina ihakikishe kuwa kila taasisi inatakiwa kuwa na Sera ya Gawio *(Dividend Policy)* ili Serikali iweze kupata mapato ya kutosha. *(Makofi)*

(ii) Utegemezi mkubwa wa ruzuku ya Serikali. Kwa kuwa baadhi ya taasisi na mashirika ya umma yanashindwa kutumia ipasavyo rasilimali walizonazo kwa ajili ya kujiongezea mapato bila kutoka katika jukumu lao la msingi;

Na kwa kuwa kushindwa kuongeza juhudi katika ufuatiliaji wa fedha kunasababisha taasisi hizo kutegemea kwa kiasi kikubwa ruzuku kutoka Serikalini na kukwamisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

Kwa hiyo basi, Bunge linaishauri Serikali kusimamia vyema taasisi na mashirika ya umma ili zijikite katika jukumu lake la msingi. Kufanya hivyo kutawezesha taasisi hizo kuwa na utendaji wenye ufanisi na tija na kuongeza mapato ikiwa ni pamoja na kuondokana na utegemezi wa ruzuku ya Serikali.

(iii) Ukosefu wa Sera ya Uwekezaji, Mpango Mkakati na Mpango wa Kibiashara kwa Taasisi zinazofanya uwekezaji. Kwa kuwa taasisi na mashirika ya umma yanatakiwa kuwa na nyaraka mbalimbali kama Sera ya Uwekezaji, Mpango Mkakati na Mpango wa Kibiashara ili taasisi iweze kujiendesha kibiashara na kuwa na ufanisi wa kutosha;

Na kwa kuwa kukosekana kwa nyaraka hizo kunazifanya taasisi za umma kukosa nguzo muhimu katika uendeshaji wake na nyaraka hizo ni nguzo katika utekelezaji wa majukumu ya taasisi;

Kwa hiyo basi, Bunge linashauri kuwa Serikali kupitia Msajili wa Hazina, ihakikishe taasisi na mashirika yote ya umma

yanaandaa nyaraka zote muhimu zinazotakiwa katika uendeshaji wa taasisi na kuhakikisha nyaraka hizo zinatumika kikamilifu.

(iv) Upungufu wa mitaji pamoja na fedha za Utekelezaji wa miradi ya uwekezaji. Kwa kuwa baadhi ya taasisi na mashirika ya umma yamekuwa na changamoto kubwa ya upungufu wa mitaji kutokana na Serikali kushindwa kukamilisha jukumu lake la kupeleka fedha za uendeshaji katika taasisi zake;

Na kwa kuwa upungufu huo wa mitaji umezifanya taasisi hizo kushindwa kutekeleza miradi mbalimbali ya uwekezaji na kuongeza gharama za uendeshaji;

Kwa hiyo basi, Bunge linashauri kuwa Serikali ipeleke mitaji ya kutosha kwa taasisi na mashirika ya umma kama ilivyoahidi katika uanzishwajiwa taasisi hizo na kama fedha hizo zilivyoidhinishwa na Bunge.

(v) Ukiukwaji wa Sherika ya Fedha Na. 16 ya 2015. Kwa kuwa baadhi ya taasisi za umma zimekuwa zikikiuka Sheria ya Fedha Na. 16 ya mwaka 2015 inazozitaka taasisi za umma kudhibiti matumizi yake ya gharama za uendeshaji na kutozidi asilimia 60;

Na kwa kuwa, kutofuata matakwa ya sheria na kuwa na matumizi makubwa inasababisha taasisi kukosa faida na kushindwa kutoa gawio au kuchanga katika Mfuko Mkuu wa Serikali;

Kwa hiyo basi, Bunge linashauri kuwa Serikali izichukulie hatua taasisi zote zinazokiuka matakwa ya Sheria Na. 16 ya 2015 ili taasisi hizo ziweze kupunguza matumisi na kutengeneza faida. *(Makofi)*

(vi) Utekelezaji wa miradi ya uwekezaji kwa baadhi ya taasisi za umma. Kwa kuwa baadhi ya taasisi zilizoanzishwa na Serikali ni za kimkakati na hivyo kuwa na miradi na shughuli nyingi zenye fursa kubwa ya kuchangia

katika uchumi na ustawi wa Taifa. Hata hivyo, shughuli au miradi mingi haitengewi rasilimali za kutosha katika kuiendesha kwa wakati ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa mikakati ya kutekeleza miradi hiyo;

Na kwa kuwa, kukosekana kwa rasilimali za kutosha na mikakati ya kutekeleza miradi ya taasisi hizo kunasababisha taasisi hizo kushindwa kutekeleza miradi mikubwa yenye tija kwa ukuaji wa uchumi;

Kwa hiyo basi, Bunge linashauri kuwa Serikali ihakikishe inawekeza na kuwa na usimamizi madhubuti katika taasisi zake za kimkakati kama Shirika la Maendeleo *(NDC)* ili taasisi hizo ziweze kuendesha miradi ya maendeleo kwa ufanisi.

(vii) Taasisi kushindwa kutekeleza Sera na Miongozo ya Ushiriki wa Sekta Binafsi na Sekta ya Umma *(PPP).* Kwa kuwa Serikali imekuwa ikitakiwa kutoa fedha zote za uendeshaji wa miradi ya taasisi na mashirika ya umma, lakini fedha hizo zimekuwa hazipatikani kwa wahusika;

Na kwa kuwa, kukosekana kwa fedha hizo kumesababisha taasisi hizo kushindwa kutekeleza miradi yake ya uwekezaji kwa wakati na kukosa tija inayotarajiwa;

Kwa hiyo basi, Bunge linaishauri Serikali kuzitaka taasisi na mashirika yake kuingia katika ubia na sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya uwekezaji ili kuipunguzia mzigo Serikali na kuweza kutekeleza miradi hiyo kwa wakati.

(viii) Uwepo wa baadhi ya sheria zinazoanzisha taasisi na mashirika ya umma kutoendana na wakati wa sasa. Kwa kuwa sheria zinazotumiwa na baadhi ya taasisi na mashirika ya umma zimepitwa na wakati kutokana na kuwa ni za muda mrefu;

Na kwa kuwa, kupitwa huko na wakati kunazifanya taasisi na mashirika hayo kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa ufanisi katika mazingira ya sasa;

Kwa hiyo basi, Bunge linashauri Serikali kuleta Bungeni mapendekezo ya kuzifanyia marekebisho sheria zote za taasisi ambazo zimepitwa na wakati ili taasisi hizo ziweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

(ix) Serikali kuchelewa kulipa madeni kwa taasisi zake. Kwa kuwa Taasisi za Serikali na baadhi ya Wizara zimekuwa na desturi ya kutokulipa madeni yake baada ya kupata huduma kutoka kwenye taasisi nyingine za umma;

Na kwa kuwa kutolipia huduma hizo kunasababisha mrundikano wa madeni ya muda mrefu yanayochangia taasisi nyingi kushindwa kujiendesha pamoja na kushindwa kutekeleza miradi ya uwekezaji kutokana na kukosekana kwa fedha;

Kwa hiyo basi, Bunge linashauri kuwa Serikali pamoja na taasisi zake ilipe madeni yote yanayotokana na kupata huduma kutoka kwa taasisi nyingine ili taasisi hizo ziweze kutumia fedha hizo kujiendesha na kutekeleza miradi mbalimbali ya uwekezaji.

(x) Ukosefu wa ufanisi katika uendeshaji wa taasisi za umma, kwa kuwa baadhi ya Taasisi zinakosa ufanisi katika matumizi mazuri ya TEHAMA pamoja na kutokana ikama ya watumishi na kukosekana kwa nidhamu na weledi wa baadhi ya Watumishi. Na kwa kuwa, kukosekana kwa ufanisi katika Utendaji wa Uendeshaji wa Taasisi hasa matumizi ya TEHAMA kutokana na Ikama na nidhamu ya weledi ya watumishi kwa sababu taasisi hizo, kukosa tija, na kupoteza dhumuni la uwezeshaji katika taasisi hizo.

Kwa hiyo basi, Bunge linashauri kuwa Serikali kupitia Msajili wa Hazina ihakikishe taasisi zake zinawekeza katika TEHAMA pamoja na kuwa na vipimo tendaji kwa watendaji wote.

(xi) Baadhi ya Bodi za Wakurugenzi za Taasisi kutokuwa hai, kwa kuwa kumekuwa na changamoto ya Wizara kuchelewa kufanya teuzi wa Wajumbe wa Bodi za

Wakurugenzi wa Taasisi mbalimbali ambazo ujumbe wa bodi hiyo unakuwa umekwisha muda wake. Kwa kuwa kukosekana kwa Bodi hizo, kunasababisha taasisi za umma, kuwa na uendeshaji usioridhisha, na si usio na tija kwa Taifa.

Kwa hiyo basi, Bunge linaishauri Serikali kuhakikisha inakuwa na mpango mwendelezo *succession planning* katika uteuzi wa Wajumbe wa Bodi za Taasisi za Umma ili ukomo wa Wajumbe katika Bodi hizo usimalizike kwa wakati mmoja.

(xii) Utendaji wa kazi za Ofisi Msajili wa Hazina; kwa kuwa utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa kiasi kikubwa unategemea taarifa ya mwaka ya Msajili wa Hazina, aidha, Ofisi ya Msajili wa Hazina ina changamoto ya matumizi ya TEHAMA pamoja na ikama ya watumishi.

Na kwa kuwa kukosekana kwa taarifa ya mwaka wa Msajili wa Hazina kwa kiasi fulani kunakwamisha utekelezaji wa shughuli za Kamati kikamilifu. Vilevile kutokuwa na matumizi mazuri ya TEHAMA pamoja na ikama ya watumishi kuna sababisha Ofisi ya Msajili wa Hazina kushindwa kutimiza wajibu wake.

Kwa hiyo basi, Bunge linashauri:-

(a) Serikali kupitia Msajili wa Hazina ihakikishe taarifa ya mwaka ya Msajili wa Hazina inaandaliwa na kuwasilishwa kwa wakati kwa ajili ya kuboresha utendaji wa kazi. *(Makofi)*

(b) Serikali iongeze bajeti ya Ofisi ya Msajili wa Hazina ili ifanye uwekezaji kwenye TEHAMA na kukamilisha ikama ya watumishi ili kuwe na usimamizi madhubuti wa taasisi na mashirika ya umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge kwa uongozi wenu makini uliowezesha kuwasilisha taarifa hii hapa Bungeni. Kwa namna ya pekee, napenda kumshukuru Msajili wa Hazina Ndugu Athuman Mbuttuka pamoja na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Msajili

wa Hazina ikiwepo pamoja na Wizara ya Fedha ikiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Mpango na Mama Dkt. Ashatu Kijaji kwa uongozi wao mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa moyo wa uadilifu mkubwa. Orodha ya Wajumbe na Kamati inaonekana katika taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa ushirikiano wa hali ya juu alioutoa. Shukrani kwa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuratibu vema shughuli za kamati chini ya Mkurugenzi Ndugu Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Chikokoto na Makatibu wa Kamati Ndugu Amina Salumu na Ndugu Elieka Saanya na Msaidizi wa Kamati Ndugu Pauline Mavunde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunawashukuru watumishi kutoka Ofisi ya Mshauri wa Mambo ya Sheria wa Bunge Ndugu Seraphine Tamba na Ndugu Matamus Fungo pamoja na Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge kwa ushirikiano wao mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja; taarifa hii ni matokeo ya uchambuzi wa kina kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma unaofanywa na taasisi na mashirika ya umma. Maoni na mapendekezo yanayotokana na uchambuzi uliofanywa na Kamati ni kwa lengo la kuishauri Serikali katika eneo la uwekezaji wa mitaji ya umma ili uwekezaji huo, ulete tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa lipokee Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu uchambuzi na uwekezaji wa mitaji ya umma, kuijadili na hatimaye kuridhia maoni mapendekezo yake ili hatimaye Serikali iyafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA (PIC) KWA KIPINDI CHA JANUARI, 2018 HADI JANUARI, 2019 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*(Inatolewa chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016*)

---

**SEHEMU YA KWANZA**

**MAELEZO YA JUMLA**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) kwa mwaka 2018 na kuliomba Bunge lako Tukufu kuipokea na kuijadili.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma imetekeleza majukumu yake ya kufuatilia uwekezaji katika Mashirika na Taasisi za Umma na Makampuni ambayo Serikali ina hisa.

***Majukumu ya Kamati***

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 12 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ina majukumu yafuatayo:-

a) Kuchambua na kubaini iwapo utekelezaji wa miradi ya uwekezaji wa umma una ufanisi na kuwa umezingatia taratibu na Sheria na miongozo mujarabu ya biashara; na

b) Kuchambua na kujadili Taarifa ya Mwaka ya Msajili wa Hazina na Mashirika ya Umma na Kampuni ambazo Serikali ina hisa.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kutekeleza majukumu yake ya kikanuni, Kamati pia imefanya kazi zake kwa kuzingatia miongozo mingine kama ifuatayo:-

i) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977;

ii) Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011;

iii) Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001;

iv) Sheria ya Msajili wa Hazina Sura ya 370;

v) Sheria ya Mashirika ya Umma ya Mwaka 1992; na

vi) Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015

***Shughuli zilizotekelezwa***

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Mwaka mmoja kuanzia Januari, 2018 hadi Januari, 2019, Kamati ilitekeleza majukumu yake kwa njia ya kufanya vikao kwa kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za Taasisi na Mashirika ya Umma kuhusu uwekezaji unaotekelezwa na Taasisi hizo. Aidha, Kamati imefanya ziara katika baadhi ya Taasisi za Umma ili kujiridhisha iwapo uwekezaji unaofanywa na Taasisi hizo una tija. Vile vile, Kamati ilipatiwa semina za mafunzo kuhusu namna bora ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati na mambo ya kuzingatia katika uchambuzi na ukaguzi wa miradi ya uwekezaji wa mitaji ya Umma. Ufafanuzi kuhusu shughuli hizo ni kama ifuatavyo:-

**a) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Msajili wa Hazina kuhusu uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Januari, 2018 hadi Januari, 2019, Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ilipokea, ilichambua na ilijadili Taarifa za Msajili wa Hazina kuhusu uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya umma yapatayo ishirini na Nane (28). Orodha ya Taasisi hizo ni kama ifuatavyo:-

i. Mfuko wa GEPF;
ii. Taasisi ya Uhasibu Arusha (IAA);
iii. Mfuko wa uwekezaji wa pamoja (UTT – Project and Ifrastructure);
iv. Kampuni ya Uendelezaji wa Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro (KADCO);
v. Mamlaka ya Maji safi na Maji taka Mwanza (MWAUWASA);
vi. Shirika la Reli Tanzania (TRC);
vii. Kampuni ya Usimamizi wa Rasilimali za Uwekezaji na Huduma kwa Wawekezaji (UTT AMIS);
viii. Mamlaka ya Udhibiti wa Masoko ya Mitaji na Hisa (CMSA);
ix. Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC);
x. Wakala wa Huduma za Ufundi, Mitambo na Umeme Tanzania (TEMESA);
xi. Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB);
xii. Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA);
xiii. Wakala wa Biashara na Leseni (BRELA);
xiv. Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC);
xv. Mamlaka ya Maji Safi na Maji taka Dar es Salaam (DAWASA);
xvi. Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM);
xvii. Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA);
xviii. Shirika la Ugavi wa Umeme (TANESCO);
xix. Shirika la Ndege Tanzania (ATCL);
xx. Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL);
xxi. Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC);
xxii. Shirika la Viwango Tanzania (TBS);
xxiii. Kampuni ya Huduma za Meli;
xxiv. Benki ya Maendeleo (TIB Development);
xxv. Mamlaka ya Maji safi na Maji taka Arusha (AUWASA);
xxvi. Shirika la Posta Tanzania (TPC);
xxvii. Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA); na
xxviii. Shirika la Uzalishaji Mali JKT (SUMA JKT).

**b) Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Uwekezaji**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwezi Machi, 2018, Kamati ilifanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Uwekezaji

inayotekelezwa na Taasisi na Mashirika ya umma katika mikoa ya Iringa na Mbeya. Mantiki ya ukaguzi ni kuiwezesha Kamati kufanya tathmini ya ufanisi na tija ya uwekezaji. Taasisi zilizotembelewa ni:-

i. Chuo Kikuu Kishiriki cha Mkwawa;

ii. Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko;

iii. Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya; na

iv. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania.

Aidha, miradi iliyotembelewa na Ufafanuzi wake inaonekana katika Kiambatisho Na. 01 cha Taarifa hii.

***Muhtasari wa dosari zilizobainika katika uwekezaji wa Mitaji ya Umma***

**Mheshimiwa Spika**, kabla ya kutoa maelezo ya kina kuhusu matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za uwekezaji wa mitaji ya Umma, naomba kulidokeza Bunge lako tukufu kwa muhtasari dosari kuu zilizobainika katika utaratibu wa uwekezaji wa mitaji ya Umma. Dosari hizo ni:-

i. Baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma hayana mtazamo wa kibiashara hali inayosababisha Taasisi hizo kushindwa kujiendesha kwa tija;

ii. Baadhi ya Taasisi na Mashirika ya umma yanashindwa kujikita katika majukumu yake ya msingi, kwa kufanya hivyo, yamekuwa na utendaji usio na ufanisi na tija na kushindwa kuongeza mapato.

iii. Baadhi ya Taasisi na Mashirika mengi ya Umma yanayofanya uwekezaji wa kibiashara hayana Mpango Mkakati, Mpango wa kibiashara na Sera ya uwekezaji.

iv. Baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma yamekuwa yakijiendesha kwa hasara hadi kufikia miaka mitatu mfululizo na kuwa mzigo kwa Serikali.

v. Baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma yanashindwa kutumia vyema rasilimali walizonazo kwa ajili ya kuzalisha mapato na kutegemea kwa kiasi kikubwa ruzuku kutoka Serikalini.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA NA MATOKEO YAKE

***Maelezo ya Jumla kuhusu uchambuzi wa Taarifa ya Msajili wa Hazina kuhusu uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha unaoishia Juni, 2018***

**Mheshimiwa Spika**, Bunge ambalo ni chombo cha Uwakilishi kwa niaba ya wananchi, kimepewa madaraka ya kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 Ibara 63 (2). Katika kutekeleza dhima hiyo, jicho la Bunge katika kuangalia Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ni Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Kanuni ya 12 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, imeainisha jukumu la msingi la Kamati hii ambalo kwa ujumla ni kufuatilia Uwekezaji wa Mitaji ya Umma.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imekuwa ikifuatilia uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa njia mbalimbali zikiwemo uchambuzi wa Taarifa za Uwekezaji na ziara za ukaguzi wa Miradi ya Uwekezaji. Katika kipindi cha Januari, 2018 hadi Januari, 2019, Kamati ilichambua Taarifa za uwekezaji na kubaini kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018, Serikali ilifanya Uwekezaji katika jumla ya Taasisi Mia Mbili Sabini (270) za ndani ya nchi na Taasisi Kumi (10) za nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2017/18, thamani ya uwekezaji wa Serikali wa ndani ya nchi (domestic investment) ulifikia jumla ya **shilingi 55,178,297,752,577.60**. Uwekezaji huu umefanyika katika Taasisi na Mashirika

yapatayo 256 ambapo kati ya Taasisi hizo, Taasisi na Mashirika 217 ni yale ambayo Serikali ina umiliki wa Asilimia 100 na Taasisi na Mashirika 39 ni yale ambayo Serikali ina umiliki wa pungufu ya Asilimia 100. Aidha, kuna Taasisi 14 ambazo hazijaanza kuandaa hesabu zake za kujitegemea hivyo, kufanya jumla ya Mashirika na Taasisi zipatazo 270. Mchanganuo wa umiliki unaoneshwa katika Jedwali Namba 1.


**Jedwali Na. 1**

| NA | KIASI CHA UMILIKI KATIKA ASILIMIA (%) | IDADI YA TAASISI |
|---|---|---|
| 1. | 100 | 231 |
| 2. | 50+ | 2 |
| 3. | 50 | 4 |
| 4. | Pungufu ya 50 | 33 |
| 5 | **JUMLA** | 270 |

***Chanzo: Taarifa ya TR 2017/2018***

Picha halisi ya mchanganuo uliopo kwenye Jedwali Na. 01 inaonekana kupitia Chati Duara Na. 01 ya Taarifa hii.

**Chati Duara Na. 01: Picha halisi ya Mchanganuo wa umiliki wa Serikali katika Taasisi, Mashirika ya Umma na Kampuni ambazo Serikali ina hisa.**



**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Taarifa ya Msajili wa Hazina umeonesha kuwa, mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2018, Serikali imefanya uwekezaji wa jumla ya **Shilingi 54,481,995,164,552.20** katika jumla ya Taasisi na Mashirika 219 ambayo Serikali ina umiliki wa kuanzia Asilimia 51 mpaka 100. Vile vile, Serikali imewekeza jumla ya **Shilingi 696,302,588,025.43** katika makampuni 37 ambayo umiliki wake wa hisa ni Asilimia 50 na pungufu.

Aidha, Katika Mwaka wa fedha ulioshia tarehe 30 Juni, 2018, Serikali ilipata faida ya jumla ya kiasi cha **Shilingi 637,536,364,016.65** kutokana na uwekezaji uliofanywa katika Taasisi na Mashirika ya Umma ambayo Serikali ina umiliki wa kuanzia Asilimia 51 hadi 100. Faida hiyo ilitokana na kukusanya mapato yasiyo ya kodi (non-tax revenue). Mchanganuo wa mapato hayo ni kama ifuatavyo;

- Gawio (Dividends) – Shilingi 303,516,089,779.15;

- Mchango wa asilimia 15 ya Mapato Ghafi Shilingi 256,182,762,024.46;

- Mapato kutoka kwenye Mfumo wa Kusimamia na Kuratibu Mawasiliano ya Simu Nchini (TCRA-TTMS) Shilingi 14,293,108,336.08;

- Urudishaji wa Mikopo na Riba – Shilingi 1,336,259,181.19;

- Michango Mingineyo – Shilingi 16,208,144,695.77; na

- Mtaji uliozidi (redemption of excess capital) – Shilingi 46,000,000,000.00.

Hata hivyo, ingawa baadhi ya Taasisi hususan za Elimu, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Afya, Kilimo na Utafiti hazitowi gawio wala mchango wa Asilimia 15, Serikali inanufaika na Taasisi hizi kutokana na huduma mbalimbali zinazotolewa na Taasisi hizi kwa jamii.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na faida ambayo Serikali imepata kutokana na uwekezaji uliofanywa kwa Taasisi ambazo ina umiliki wa zaidi ya Asilimia 50 kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni, 2018, Serikali pia ilipata faida ya **Shilingi 35,965,754,612.05** kutokana na uwekezaji uliofanya katika Makampuni Kumi na Moja (11) ambayo Serikali ina umiliki wa hisa wa Asilimia 50 na pungufu ya Asilimia 50. Faida iliyopatikana ni kutokana na malipo ya Gawio kutoka katika Kampuni hizo kwenda Serikalini. Mchanganuo wa gawio lililopatikana unaonekana katika Jedwali namba 3.

**Jedwali Namba 3**

***Chanzo: Taarifa ya TR 2017/18***

**Mheshimiwa Spika**, Serikali pia imefanya uwekezaji katika Mashirika yaliyo nje ya Nchi. Uchambuzi wa Taarifa ya Msajili wa Hazina umeonesha kuwa, thamani ya uwekezaji uliofanywa na Serikali katika Mashirika Kumi (10) yaliyopo nje ya Nchi umefikia jumla ya **Shilingi 580,843,639,544.09.** Orodha ya Taasisi hizo pamoja na umiliki wa Serikali unaonekana katika jedwali Namba 2.

**Jedwali Namba 2**

| NA. | JINA LA TAASISI | UMILIKI WA SERIKALI |
|---|---|---|
| 1 | African Development Bank (ADB) | 0.76% |
| 2 | Shelter Afrique | 0.52% |
| 3 | East African Development Bank (EADB) | 24.98% |
| 4 | International Bank for Reconstruction and Development (IBRD) | 0.06% |
| 5 | International Development Association (IDA) | 0.26% |
| 6 | International Finance Corporation (IFC) | 0.04% |
| 7 | Multilateral Investment Guarantee Agency (MIGA) | 0.22% |
| 8 | PTA BANK | 8.36% |
| 9 | African Reinsurance Corporation (Africa Re) | 0.80% |
| 10 | African Trade Insurance Agency (ATI) | 8.37% |

***Chanzo: Taarifa ya TR 2017/18***

Kutokana na uwekezaji uliofanyika katika Taasisi zilizo nje ya Nchi, Serikali inatarajia kupokea kiasi cha **Dola za Kimarekani 128,000** kutoka katika Kampuni ya African Reinsurance Corporation (Africa Re) ambapo kuna uwekezaji wa Asilimia 0.80. Aidha, fedha hizo bado hazijapokelewa na Msajili wa Hazina. Hata hivyo, Uwekezaji wa Serikali katika Taasisi za nje haujalenga moja kwa moja kurejesha faida kifedha (financial return). Uwekezaji katika Mashirika haya ni kutokana na mikataba ya ushirikiano wa Nchi Kikanda na Kimataifa. Kutokana na uwekezaji huu, Nchi imekuwa ikipata misaada ya kifedha na mikopo ya riba nafuu ambayo imesaidia katika utekelezaji wa miradi yake mbalimbali ya maendeleo. Mara chache sana nchi imekuwa ikipata gawio kutokana na ufanisi wa uwekezaji uliofanywa na Serikali katika Mashirika haya ya nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Matokeo ya uchambuzi wa kina uliofanywa na Kamati umebaini kuwa, uwekezaji wa ndani

wa Serikali katika Taasisi na Mashirika ya umma na Makampuni ambayo Serikali ina hisa umeongezeka kwa asilimia **13.70** ambapo, katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 June, 2017 uwekezaji wa Serikali ulifikia jumla ya **Shilingi 48,530,723,061,897.90** ikilinganishwa na kiasi cha **Shilingi 55,178,297,752,577.60** kilichofikiwa katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2018. Ongezeko la uwekezaji uliofanywa na Serikali umetokana na baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma kufanya uthamini wa mali zake mfano; Mamlaka ya Viwanja vya Ndege – TAA kutoka **Shilingi Bilioni 458** hadi **Shilingi Trilioni 6.5**, Shirika la Ugavi la Umeme (TANESCO) kutoka **Shilingi Bilioni 662** hadi **Shilingi Trilioni 1.8**, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) kutoka **Shilingi Trilioni 2.9** hadi **Shilingi Trilioni 3.5**.

**Mheshimiwa Spika**, faida inayotokana na uwekezaji huo imepungua kwa Asilimia **23.95** ambapo, kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2017 faida ya uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma na Makampuni ambayo Serikali ina hisa ilikuwa ni **Shilingi 885,635,836,026.32**. Aidha faida iliyopatikana kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2018 ni **Shilingi 673,502,118,628.70**. Kupungua kwa faida kwa mwaka wa fedha 2017/18 kumetokana na kupungua kwa makusanyo yaliyotokana na kuitishwa kwa mtaji wa ziada (Excess capital) kutoka **Shilingi Bilioni 192.75** mwaka 2016/17 hadi **Shilingi Bilioni**. **62.2** mwaka 2017/18


**Mheshimiwa Spika**, katika uwekezaji wowote unaofanywa na Serikali inategemewa kupatikana kwa faida ambayo ni mapato yasiyo ya kodi au kutoa huduma iliyo bora. Uwekezaji wa Serikali umefanyika katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Taasisi na Mashirika ya Umma na Makampuni ambayo Serikali ina umiliki wa zaidi ya asilimia 50 na pungufu ya asilimia 50. Aidha, Uwekezaji uliofanywa na Serikali ukilinganishwa na faida iliyopatikana umekuwa ukitofautiana katika Taasisi zenye umiliki wa mkubwa na Makampuni yenye hisa chache.
Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018, Serikali iliwekeza katika Taasisi na Mashirika ya Umma yenye umiliki wa kuanzia Asilimia 51

hadi 100 wenye jumla ya **Shilingi 54,481,995,164,552.20** na kupata faida ya **Shilingi 637,536,364,016.65.** Faida iliyopatikana ni sawa na **asilimia 1.17** (Return on Investment) ya uwekezaji uliofanyika. Vile vile, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018, Serikali iliwekeza katika Makampuni ambayo ina umiliki wa hisa chache (asilimia 50 na pungufu) wenye jumla ya **Shilingi 696,302,588,025.43** na kupata faida kwa njia ya gawio la **Shilingi 35,965,754,612.05**. Aidha, faida iliyopatikana ni sawa na **asilimia 5.17** ya uwekezaji uliofanyika katika Makampuni ambayo Serikali ina hisa chache.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya jumla ya uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kuwa, faida ya jumla iliyopatikana kutokana na uwekezaji uliofanywa na Serikali kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2018 ni **asilimia 1.22** tu ya uwekezaji wote. Asilimia hiyo imetokana na ulinganisho wa uwekezaji wenye jumla ya **shilingi 55,178,297,752,577.60** na faida ya jumla ya **Shilingi 673,502,118,628.70**.

Aidha, mwenendo wa ukuaji wa uwekezaji wa mitaji na faida kwa miaka mitatu umeoneshwa katika Mchoro (Graph) Namba 1.

**Mchoro (Graph) Na. 01: Sura ya ongezeko la thamani ya uwekezaji na faida kwa mwaka 2015/16, 2016/17 na 2017/18**



***Uchambuzi wa Uwekezaji***

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kifungu (2) cha Sheria ya Msajili wa Hazina Sura 370; Uwekezaji katika Mashirika ya Umma umetafsiriwa kuwa ni Mtaji wa Serikali katika Mashirika kwa njia ya Hisa, Mikopo, Fedha Taslim, Hati Fungani na Majengo yaliyowekwa moja kwa moja katika Shirika, Kampuni au Taasisi ya Umma. Aidha, dhima ya Serikali kuwekeza katika Mashirika ya Umma ni kukuza Uchumi wa Nchi kwa madhumuni ya Kupata mapato kwa njia ya faida/gawio, kusogeza na kutoa huduma kwa urahisi kwa jamii na kuchochea maendeleo ya sekta mbalimbali za uchumi, kudhibiti utoaji wa huduma na kulinda maslahi ya jamii (Wazalishaji na Watumiaji) na kutengeneza ajira kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na dhima hiyo ya uwekezaji, Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa Taarifa zilizowasilishwa za Taasisi na Mashirika ya Umma ili kubaini ufanisi na tija ya uwekezaji unaofanywa na Taasisi hizo na kama umekidhi madhumuni ya uanzishwaji wake. Katika uchambuzi wake, Kamati ilitumia njia zifuatazo:-

i) Kupitia Taarifa za Uwekezaji na Utendaji wa Mashirika na Taasisi za umma zinazofanya uwekezaji wa mitaji ya Umma;

ii) Kupitia Sheria zilizoanzisha Taasisi na Mashirika ya Umma ili kujiridhisha iwapo uwekezaji umezingatia Taratibu, Sheria na Miongozo mujarabu ya biashara;

iii) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za Msajili wa Hazina kuhusu uchambuzi wa utendaji na uwekezaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma ili kupokea maoni ya Msimamizi wa Taasisi na Mashirika yanayofanya uwekezaji wa mitaji ya umma; na

iv) Kufanya mahojiano na Wenyeviti wa Bodi na Menejimenti za Taasisi na Mashirika ya Umma.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kutumia njia hizo, Kamati ilifuatilia uwekezaji huo wa mitaji ya umma kwa kufanya uchambuzi na kubaini mambo makuu yafuatayo:-

i) Kukosekana kwa Sera ya Gawio (Dividend Policy) kwa Taasisi na Mashirika ya Umma;

ii) Utegemezi mkubwa wa Ruzuku ya Serikali;

iii) Ukosefu wa Sera ya Uwekezaji, Mpango wa Uwekezaji na Mpango wa Kibiashara kwa Taasisi zinazofanya uwekezaji,

iv) Upungufu wa Mitaji pamoja na Fedha za utekelezaji wa Miradi ya Uwekezaji;

v) Ukiukwaji wa Sheria ya Fedha Na 16 ya 2015 Kifungu cha 46 (10)(A)(1);

vi) Utekelezaji wa miradi ya Uwekezaji kwa baadhi ya Taasisi za Umma;

vii) Taasisi kushindwa kutekeleza Sera na Miongozo ya ushiriki wa Sekta Binafsi na Sekta za Umma (PPP) katika kuendesha miradi;

viii) Uwepo wa baadhi ya Sheria zilizoanzisha Taasisi na Mashirika ya Umma kutoendana na wakati wa sasa;

ix) Serikali kuchelewa kulipa madeni kwa Taasisi zake;

x) Ukosefu wa ufanisi katika Uendeshaji wa Taasisi za Umma;

xi) Baadhi ya Bodi za Wakurugenzi za Taasisi kutokuwa hai; na

xii) Utendaji wa Ofisi ya Msajili wa Hazina

## Kukosekana kwa Sera ya Gawio (Dividend Policy) kwa Taasisi na Mashirika ya Umma

**Mheshimiwa Spika**, Sera ya Gawio ni mwongozo unaotengenezwa kwa lengo la kuweka bayana mgawanyo wa faida baada ya kodi. Mwongozo huo huonesha kiasi cha asilimia ambacho kinapaswa kutolewa kwa wana hisa na kiasi kinachopaswa kuelekezwa katika uendelezaji wa biashara kwa kuzingatia mpango wa biashara wa Taasisi na Mashirika ya Umma na Makampuni ambayo Serikali ina hisa. Mwongozo huu unabainisha ni kiasi gani Taasisi inapaswa kutoa kama gawio.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ni mmiliki katika Taasisi na Mashirika ya Umma kwa kuwa imewekeza kiasi kikubwa cha fedha, Umiliki wa Serikali unatofautiana kulingana na kiasi cha mtaji kilichowekezwa. Kuna Taasisi zinazomilikiwa na Serikali kwa Asilimia Mia Moja na nyingine chini ya Asilimia Mia Moja. Tofauti ya umiliki pia huchangia tofauti katika upatikanaji wa faida (gawio). Kiasi cha gawio kinatofautiana kutoka Taasisi moja hadi nyingine kutokana na hali ya kibiashara na malengo yaliyopo ya Taasisi husika.

Aidha, Taasisi ambazo zinamilikiwa na Serikali kwa Asilimia Mia Moja zinatakiwa kuandaa mapendekezo ya Sera ya Gawio na kuyapeleka kwa Msajili wa Hazina kwa ajili ya kupata idhini. Kwa Taasisi ambazo Serikali ni mbia, mapendekezo hayo hupitishwa katika kikao cha wana hisa baada ya Bodi na Menejimenti ya Taasisi kukamilisha mapendekezo. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa, Taasisi na Mashirika ya Umma yaliyo mengi hayana Sera ya Gawio hali inayosababisha Taasisi hizo kukosa nyenzo muhimu ya kuipatia Serikali mapato kwa kuwa ni mwana hisa katika Taasisi hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Katika Taasisi 28 zilizofika mbele ya Kamati, ni Taasisi moja pekee (Kampuni ya KADCO) ndio yenye Sera ya Gawio kati ya Taasisi 11 zinazotakiwa kuwa na Sera ya Gawio. Mfano wa Taasisi na Mashirika ya Umma ambayo yamefika mbele ya Kamati na yanatakiwa kuwa na Sera ya

Gawio lakini yamebainika kutokuwa na Sera ya Gawio ni Mfuko wa uwekezaji wa pamoja (UTT – Project and Ifrastructure), Kampuni ya Usimamizi wa Rasilimali za Uwekezaji na Huduma kwa Wawekezaji (UTT AMIS), Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC), Shirika la Ugavi wa Umeme (TANESCO), Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC),

**Utegemezi Mkubwa wa Ruzuku ya Serikali**

**Mheshimiwa Spika**, Katika kupitia Taarifa za Taasisi na Mashirika ya Umma, Kamati imebaini kuwa, zipo baadhi ya Taasisi zinashindwa kutumia ipasavyo rasilimali zake kwa ajili ya kujiongezea mapato bila ya kutoka katika jukumu lao la Msingi. Kushindwa kuongeza juhudi katika utafutaji wa fedha kunasababisha Taasisi hizo kutegemea kwa kiasi kikubwa ruzuku kutoka Serikalini.

**Mheshimiwa Spika,** Iwapo Taasisi na Mashirika ya Umma yatajikita katika majukumu yake ya msingi na kuweza kujitegemea kwa kuzalisha mapato ya kutosha kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zake, zitaisaidia Serikali kutumia rasilimali zilizopo kwa ajili ya kutekeleza miradi mikubwa ya uwekezaji na yenye tija kwa taifa badala ya fedha hizo kutumika kama ruzuku kwa ajili ya shughuli za uendeshaji wa Taasisi.

Kwa mfano, katika kufanya uchambuzi wa Taasisi na Mashirika ya Umma Kamati imebaini kuwa, uwezo wa Chuo Kikuu cha Dodoma kujitegemea katika kipindi cha miaka mitatu (2014/15, 2015/16 na 2016/17) umefikia wastani wa Asilimia 52. Kamati inaona iwapo chuo kitaongeza bidii katika utafutaji wa fedha kupitia utafiti, ushauri elekezi na kutumia ardhi ya chuo kuongeza mapato, itapunguza utegemezi wa Serikali na kuongeza zaidi uwezo wa kujitegemea.

**Ukosefu wa Sera ya Uwekezaji, Mpango Mkakati na Mpango wa Kibiashara kwa Taasisi zinazofanya uwekezaji**

**Mheshimiwa Spika**, Taasisi na Mashirika ya Umma yanatakiwa kuwa na nyaraka mbalimbali ili Taasisi hizo ziweze kujiendesha

kibiashara na kuwa na ufanisi wa kutosha. Kukosekana kwa Nyaraka hizo kunazifanya Taasisi za Umma kukosa nguzo muhimu katika uendeshaji wake. Nyaraka ambazo ni nguzo katika utekelezaji wa majukumu ya Taasisi ni Sera ya Uwekezaji (Investment Policy), Mpango Mkakati (Strategic Plan) na Mpango wa Kibiashara (Business Plan).

**Mheshimiwa Spika,** Sera ya Uwekezaji ni mwongozo unaoandaliwa kwa Kampuni na Mashirika yanayofanya biashara hasa ambayo mapato yake yanategemea kwa kiwango kikubwa uwekezaji unaofanyika katika makundi mbalimbali. Lengo la sera hii ni kupunguza vihatarishi vinavyotokana na kuwa na uwekezaji mkubwa katika kundi moja (portfolio risk). Taasisi hizi zinawekeza katika ununuzi wa Hisa, Hatifungani, Majengo na Akiba katika muda maalum (Fixed Deposits).

Hata hivyo, Kamati imebaini baadhi ya Taasisi ambazo zipo katika kundi hili kutokuwa na Sera ya Uwekezaji hali inayohatarisha upotevu wa fedha za Umma zilizowekezwa. Katika Taasisi na Mashirika yaliyofika mbele ya Kamati, ni Taasisi Tatu tu ndizo zenye Sera ya Uwekezaji kati ya Taasisi Kumi na Mbili zinazotakiwa kuwa na Sera ya Uwekezaj. Mfano wa Taasisi ambazo hazina Sera ya Uwekezaji ni Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Shirika la Ugavi wa Umeme (TANESCO) na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia imebaini baadhi ya Taasisi za Umma kutokuwa na Mpango Mkakati au kuwa na Mpango Mkakati uliokwisha muda wake. Taasisi na Mashirika ya Umma yanatakiwa kuwa na Mpango Mkakati utakaosaidia kutekeleza mpango wa Maendeleo wa Taifa katika eneo lake kisheria (mandate). Kwa kuwa, Mpango mkakati ni nyaraka inayoandaliwa kutoa dira ya mwelekeo wa Kampuni au Shirika katika kipindi cha miaka 5 na kwa Mashirika ya umma mpango huu unatakiwa uendane na mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka 5. Taasisi zilizobainika kutokuwa na Mpango Mkakati ni DAWASA na kampuni ya Huduma za Meli (MSCL),

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na nyaraka muhimu zilizotajwa hapo juu, Taasisi zinazofanya biashara zinatakiwa kuwa na Mpango wa biashara. Mpango wa Biashara ni nyaraka inayoandaliwa kwa Mashirika na Kampuni zinazofanya biashara, mpango huu unakuwa katika kipindi cha miaka miwili, mitatu ukiwa na lengo la kutoa mwelekeo wa namna biashara itakavyotekelezwa katika kipindi husika. Mpango huu unatokana na mpango Mkakati. Kwa kuzingatia vipaumbele vilivyopo katika Mpango Mkakati na mpango wa Biashara, Bajeti ya mwaka inaandaliwa ikiainisha rasilimali zinazohitajika kutekelezwa katika kipindi cha mwaka mmoja. Kwa muktadha huo, ni muhimu kwa Taasisi na Mashirika ya Umma kukamilisha nyaraka zote muhimu kwa ajili ya uendeshaji bora na wenye tija.

**Upungufu wa Mitaji pamoja na Fedha za utekelezaji wa Miradi ya Uwekezaji**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapenda kuipongeza Serikali ya awamu ya tano kwa jitihada za kufufua baadhi ya Mashirika ya Umma hali itakayochachua sekta nyingi za kiuchumi na hatimaye kuinua uchumi wa Nchi. Uboreshaji wa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) uliohusisha pamoja na mambo mengine ununuzi wa Ndege Sita kwa sasa na ujenzi wa Reli ya kati kwa kiwango cha SGR ni maeneo ya kutolea mfano.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na jitihada hizo za serikali, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, bado kuna changamoto kubwa ya ukosefu wa Mtaji kwa baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma. Serikali kushindwa kukamilisha jukumu lake la kupeleka mtaji katika Taasisi zake kunazisababishia Taasisi hizo kushindwa kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa ufanisi na kutoleta tija inayotarajiwa. Mfano wa Taasisi zenye upungufu wa Mtaji ni Benki ya Posta Tanzania, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania, Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Kampuni ya Huduma za Meli, Shirika la Posta Tanzania (TPC) na Benki ya Maendeleo ya TIB.

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na upungufu wa mtaji katika benki ya Posta kwa muda mrefu tangu kuanzishwa kwake Mwaka 1991. Ongezeko la mtaji uliowekezwa na wana hisa limekuwa dogo au kukosekana kwa muda mrefu na hivyo ukuaji wa mtaji umekuwa ukitegemea faida iliyokuwa ikipatikana mwaka hadi mwaka. Upungufu wa mtaji uliilazimu Benki kuandaa makakati wa kuuza hisa zake kwa watanzania kupitia soko la hisa la Dar es Salaam mwaka 2017. Pamoja na nia njema na juhudi za makusudi za Serikali kuamua kujenga benki chache imara na zenye mtaji wa kutosha kwa kuziunganisha Benki ya TPB na Benki ya Twiga pamoja na Benki ya Wanawake, bado kuna changamoto kubwa ya Upungufu wa mtaji katika Benki ya Posta Tanzania. Hivyo ni jukumu la Serikali kama mwana hisa mkubwa wa benki kutoa fedha kwa ajili ya kuongeza mtaji wa benki.

Vile vile, Kamati imebaini kuwa, kuna haja ya Serikali kuongeza mtaji katika Shirika la Mawasiliano la Taifa (TTCL) ili liweze kufanya kazi zake kwa ufanisi na kuendana na kasi ya ushindani katika soko. Pamoja na kuongezeka kwa mtaji wa TTCL kutoka **hasi ya Shilingi Bilioni 15.745** kwa Mwaka 2015/16 hadi kufikia **Shilingi Bilioni 12.814** kwa Mwaka 2016/17, bado kuna upungufu mkubwa wa mtaji ili shirika liweze kukabiliana na ushindani uliopo katika sekta ya mawasiliano kwa kuwa sekta ya mawasiliano inakuwa kwa kasi ya haraka. Mpango wa Biashara wa TTCL unaeleza kuwa, Kampuni inahitaji jumla ya **Dola za Kimarekani 762** katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2019/20 hadi 2022/23.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa za Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) zilizowasilishwa mbele ya Kamati zimebainisha kuwa, NDC inatekeleza miradi mingi ya kimkakati inayohitaji fedha nyingi kuanzia katika hatua ya upembuzi yakinifu hadi utekelezaji. Kwa kiasi kikubwa miradi hiyo inategemeana yaani kukamilika kwa mradi mmoja kunafungua fursa ya kutekelezwa kwa mradi mwingine. Hata hivyo, utekelezaji wa miradi hiyo umekuwa na changamoto kutokana na kukosekana kwa fedha za kuiendesha hali ilyosababishwa na kushuka kwa mtaji wa uendeshaji kwa **Asilimia 123.97**

kutoka **Shilingi Bilioni 14.472** Mwaka 2015/16 hadi mtaji hasi wa **Shilingi Bilioni 34.416** mwaka 2016/17.

**Mheshimiwa Spika**, katika Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za kamati iliyowasilishwa katika Bunge lako Tukufu Mwezi Februari, 2017, Kamati hii ilitoa maelezo kuhusu changamoto ya Mtaji inayoikabili Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) na kuitaka Serikali kuongeza mtaji katika Benki hiyo. Taarifa ya kamati ilieleza kuwa, Benki inashindwa kutekeleza majukumu yake ya kimkakati kutokana na upungufu wa mtaji walionao. Benki ilianza na mtaji wa **Shilingi Bilioni 60** ingawa mtaji ulioidhinishwa (Authorized Capital) ni **Shilingi Bilioni 800**. Serikali iliahidi kutenga katika Bajeti yake ya kila Mwaka kiasi cha Shilingi Bilioni 100 ili kukamilisha mtaji unaohitajika na Benki lakini fedha hizo hazikutolewa.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2017/18, Serikali ilichukua mkopo wa bei nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika wenye jumla ya **Shilingi Bilioni 210** na kuzikopesha fedha hizo kwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania kwa ajili ya kusaidia uendeshaji wa Benki. Hata hivyo hadi Benki inakutana na Kamati ilipokea kiasi cha **Shilingi Bilioni 102** pekee na Mkataba unaitaka AfDB kutoa fedha zote zilizobaki kufikia mwezi Juni, 2019. Aidha, fedha hizo zimepelekwa TADB kama mkopo badala ya mtaji. Kamati inapongeza jitihada hizo, lakini uchambuzi umebainisha hatari kubwa ya kufilisika kwa Benki inayoweza kutokea iwapo wanufaika wa mkopo utakaotolewa na Benki watashindwa kurejesha fedha hizo kwa wakati kwakuwa TADB inatakiwa kuilipa Benki ya Maendeleo ya Afrika. Kufilisika kwa TADB kutatokana na mtaji mdogo wa Benki wa **Shilingi Bilioni 60** ambao utashindwa kulipa mkopo wa **Shilingi Bilioni 210**.

**Mheshimiwa Spika**, tatizo la mtaji limejitokeza pia katika Shirika la Posta Tanzania. Shirika halijawahi kupewa mtaji wa kujiendesha (working capital) tangu kuanzishwa kwake kinyume na matakwa ya sehemu ya V kifungu cha 11 (1) cha Sheria Na. 19 ya Mwaka 1993 iliyoanzisha Shirika la Posta ili kuwezesha uendeshaji wake. Aidha, kwenye vitabu vya mahesabu vya Shirika mali za majengo na viwanja baada

ya mgawanyo wa lililokuwa Shirika la Posta na Simu zimetambulika kama -'*Advance towards share capital*'. Pamoja na Shirika kutopewa mtaji, pia kuna changamoto ya Shirika kuorodheshwa kwenye orodha ya Mashirika yanayosubiriwa kurekebishwa (specification) hali inayosababisha Shirika lishindwe kukopa licha ya kuwa na viwanja na majengo mengi Nchi nzima ambayo yangetumika kama rehani (collateral security). Aidha, Kamati inashauri Shirika liondolewe katika orodha ya Mashirika yanayosubiri kurekebishwa (Di-specification) kama ilivyofanya kwa Mashirika mengine ili Shirika liwe huru na liweze kujiendesha kwa ufanisi zaidi.

Vile vile, tatizo la upungufu wa mtaji limebainika pia katika Benki ya Maendeleo ya TIB ambapo, kulingana na mpango mkakati wa Benki, TIB inahitaji mtaji wa **Shilingi Bilioni 500** ili iweze kugharamia miradi mikubwa ya maendeleo. Hata hivyo, Serikali imetoa mtaji wa **Shilingi Bilioni 160** pekee (mwaka 2010 Shilingi Bilioni 50, mwaka 2012 Shilingi Bilioni 50, mwaka 2014 Shilingi Bilioni 10 na mwezi Disemba, 2017 Shilingi Bilioni 50) na kufanya jumla ya mtaji kufikia **Shilingi Bilioni 230.83** mwaka 2017. Benki ya Maendeleo ni Taasisi maalumu iliyoundwa na kumilikiwa na Serikali kwa dhumuni la kuziba mianya inayotokana na mapungufu kwenye soko la mtaji na hivyo kuhamasisha na kutia chachu ya maendeleo katika sekta muhimu kwa uchumi wa Nchi. Hivyo basi, Serikali ikamilishe azma yake ya kuweka mtaji katika benki hii.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa miradi ya maendeleo unahitaji uwekezaji wa kutosha ikiwa ni pamoja na mtaji wa Taasisi na Mashirika ya umma. Hivyo, Serikali iongeze mtaji katika Taasisi zake (hasa Taasisi za kimkakati) ili Taasisi hizo ziweze kujiendesha kwa tija na kuiletea manufaa Nchi yetu.

### Ukiukwaji wa Sheria ya Fedha Na 16 ya 2015 Kifungu cha 46 (10)(A)(1)

**Mheshimiwa Spika**, Taasisi za Umma zinatakiwa kudhibiti matumizi yake ya gharama za uendeshaji na kutozidi Asilimia 60 kama Sheria ya Fedha Na 16 ya 2015 kifungu cha 46 (10)

(A) (1) inavyotamka. Aidha, Kamati imebaini uwepo wa baadhi ya Taasisi kukiuka matakwa ya Sheria na kuwa na matumizi makubwa yanayosababisha Taasisi kukosa faida na kushindwa kutoa gawio au kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Mfano wa Taasisi ambazo zimekutana na Kamati na kubainika kuwa na Matumizi makubwa ni Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania TPDC, Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) na Shirika la Maendeleo ya Taifa (NDC).

Kulingana na uchambuzi wa kina uliofanywa na Kamati, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) limebainika kujiendesha kwa hasara kwa miaka mitatu mfululizo, kuanzia mwaka 2014/15 hadi 2016/17 matumizi yalikuwa yakiongezeka ikilinganishwa na mapato yaliyokusanywa na kupelekea Shirika kupata hasara kama ifuatavyo; Mwaka 2014/15 **Shilingi 293,715,000,000,** Mwaka 2015/16 **Shilingi 372,625,000,000** na Mwaka 2016/17 **Shilingi 157,181,000,000**

**Mheshimiwa Spika**, kamati pia imebaini uwepo wa hasara katika Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) ambapo, imekuwa ikipata nakisi kutokana na matumizi makubwa yanayozidi mapato hali iliyosababisha kupatikana kwa hasara ya **Shilingi Milioni 4,216** mwaka 2014/15, **Shilingi Milioni 3,321** Mwaka 2015/16 na **Shilingi Milioni 1,957**

Vile vile, Shirika la Maendeleo ya Taifa (NDC) limebainika kujiendesha kwa hasara kutokana na kuwa na matumizi makubwa yanayozidi mapato ya Shirika ambapo, Mwaka 2015/16, Shirika lilipata hasara ya Shilingi **4,745,716,000** na Mwaka 2016/17, Shirika lilipata hasara ya Shilingi **4,195,395,000.**

**Mheshimiwa Spika**, kupatikana kwa hasara ya muda mrefu kwa baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma, kunachangia kwa kiasi kikubwa uendeshaji wa kusuasua kwa Taasisi hizo na kusababisha miradi mingi ya uwekezaji kushindwa kutekelezeka na kukamilika kwa wakati ili iweze kuleta tija iliyotarajiwa. Aidha, Taasisi nyingi kutokuwa na mtazamo wa kibiashara kunachangia kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa nakisi na kuikosesha Serikali mapato.

**Utekelezaji wa miradi ya uwekezaji kwa baadhi ya Taasisi za Umma**

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wa Taarifa za uwekezaji za taasisi na Mashirika ya Umma, kamati imebani kuwa zipo Taasisi zina miradi na shughuli nyingi zenye fursa kubwa ya kuchangia katika uchumi na ustawi wa Taifa. Hata hivyo, shughuli/miradi mingi haitengewi rasilimali za kutosha katika kuziendeleza kwa wakati.

Kwa mfano, Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) ni Taasisi ya kimkakati ambayo miradi mingi ya kielelezo inawekwa chini yake ili itekelezwe. Miradi hiyo ni kama Mradi unganishi wa Mchuchuma na Liganga, mradi wa kiwanda cha kutengeneza matairi cha Arusha, mradi wa *Kilimanjaro machine tool*, mradi wa viuadudu Kibaha, mradi wa kuendeleza maeneo ya viwanda Kibaha, mradi wa Magadi Engaruka kwa kutaja baadhi. Pamoja na wingi wa miradi tena yenye uwezekano mkubwa kutekelezwa kwa tija hakuna rasilimali na mikakati ya kutekeleza miradi hiyo kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, Shirika jingine lililofika mbele ya Kamati na kupata fursa ya kuwasilisha miradi yake ni SUMA JKT. Miradi inayotekelezwa na Shirika ni Kampuni ya ulinzi, kampuni ya ujenzi, SUMA JKT Tower – Dodoma, Mradi wa Matrekta, kiwanda cha ushonaji Mgulani, kiwanda cha samani Chang'ombe, kiwanda cha kuchakata kokoto, kiwanda cha kutengeneza bidhaa za ngozi, kiwanda cha maji ya kunywa, kiwanda cha kuchakata nafaka Mlale Songea, uuzaji wa zana za kilimo na vipuli na SUMA JKT *recreation and catering services.*

**Mheshimiwa Spika**, tathmini ya kamati juu ya Suma JKT imebaini kuwa, ni Taasisi ambayo malengo yake yako katika makundi matatu. Kundi la kwanza ni kuendesha shughuli kwa minajili ya kupata faida, kundi la pili ni kutoa huduma na tatu kwa kiasi fulani kutimiza majukumu ya kitaifa. Ushauri wa kamati kwa Taasisi hii ni kuwa warejee Dhima ya uwepo wao na kuongeza jukumu la mafunzo maalum. Kupitia mafunzo

maalum watatumia kampuni tanzu zao kufundisha vijana waliotoka JKT ili waweze kuwa na uwezo mkubwa wa kiujasiliamali ili pindi wanapomaliza mafunzo waweze kujitegemea. Utaratibu huu utaipatia Suma JKT nguvu kazi nafuu na yenye nidhamu kubwa lakini zaidi itawezesha kutengeneza tabaka la wajasiliamali wa Tanzania wenye weledi na nidhamu ya hali ya juu.

**Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Mbolea Tanzania ni Taasisi muhimu kwa maendeleo ya Taifa kwa kuzingatia nafasi ya sekta ya kilimo katika kujenga uchumi wa Nchi na ustawi wa watu wake. Pamoja na kuwepo soko la mbolea nchini na nchi jirani na pamoja na Kampuni hii kuwa na mtandao wa maghala ya kuhifadhi mbolea kwa sehemu kubwa ya nchi, hawana mtaji wa kutosha wa uendeshaji. Ushauri wa kamati ni kuwa Kampuni hii ambayo inategemewa na Serikali kutoa huduma nchi nzima hata pale ambapo sekta binafsi hawako tayari ipewe mtaji wa kutosha kuendesha shughuli hizo. Uamuzi huo uende sambamba na kuwapatia rasilimali za kuendesha Kampuni kwa tija ikiwemo rasilimali watu.

**Taasisi kushindwa kutekeleza Sera na Miongozo ya ushiriki wa Sekta Binafsi na Sekta za Umma (PPP) katika kuendesha miradi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma imekuwa ikiangalia utekelezaji wa miradi ya uwekezaji wa Umma kama ina tija na inazingatia taratibu na Sheria za kibiashara. Pamoja na mambo mengine, Kamati imebaini kusuasua kwa utekelezaji wa miradi kwa baadhi ya Taasisi kutokana na ukosefu wa fedha za uendeshaji wa miradi hiyo. Hata hivyo, changamoto hiyo inaweza kutatuliwa iwapo Taasisi za Serikali zitaingia ubia na Sekta binafsi (PPP) katika utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Ushirikishwaji wa Sekta binafsi katika kutekeleza miradi mbalimbali utachangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi na kuipunguzia Serikali mzigo wa kuendesha miradi yote nchini. Aidha, Taasisi nyingi zimekuwa zikikosa mitaji wa uendeshaji kutokana na ufinyu wa fedha ikilinganishwa na

wingi wa miradi inayotaka kutekelezwa. Uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kuwa, Taasisi na Mashirika ya umma yamekuwa yakishindwa kutekeleza miradi ya uwekezaji kwa kuwa yamekuwa yakitegemea kwa kiasi kikubwa fedha kutoka Serikalini ambapo fedha hizo zimekuwa hazipelekwi kwa wakati katika Taasisi hizo hali inayosababisha ucheleweshwaji wa miradi mingi. Hivyo basi, suluhisho la ukosefu wa fedha za uendeshaji wa miradi ni kwa Taasisi za Umma kuingia ubia na Sekta binafsi (PPP) ili utekelezaji wa miradi ufanyike kwa wakati na kwa ufanisi.

**Uwepo wa baadhi ya Sheria zilizoanzisha Taasisi na Mashirika ya Umma kutoendana na wakati wa sasa**

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini uwepo wa baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma kutumia Sheria zilizopitwa na wakati na hivyo kuzifanya Taasisi hizo kushindwa kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa ukamilifu. Aidha, baadhi ya Taasisi zinashindwa kuingia katika soko la ushindani wa kibiashara kwa kuwa Sheria zilizoanzisha Taasisi hizo haziendani na mazingira ya sasa ya kibiashara. Mfano wa Taasisi ambazo Sheria yake imepitwa na wakati ni Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) na Kampuni ya Huduma za Meli.

**Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Chakula na Dawa imeundwa kupitia Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Na.1 ya Mwaka 2003 Sura ya 219 ya Sheria za Tanzania. Aidha, kumekuwepo na changamoto nyingi zinazoikumba TFDA na kusababisha kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi pamoja na kushindwa kukidhi mahitaji ya sasa ikiwemo masuala ya kiuendeshaji, makosa na adhabu kupitwa na wakati kutokana na Sheria iliyopo kupitwa na wakati.

Vile vile, Changamoto ya Sheria iliyopitwa na wakati imejitokeza pia katika Kampuni ya Huduma za Meli. Kampuni haina hadhi ya kisheria kwa kuwa haikuanzishwa kwa Sheria yake bali imesajiliwa kama Kampuni kwa Sheria ya Makampuni Sura ya 212. Kamati imebaini kuwa, kukosekana kwa hadhi ya kisheria ya Kampuni (Legal Status of the

Company) kunasababisha Kampuni kushindwa kuwa na mipango thabiti ya uendeshaji ikiwa ni pamoja na kushindwa kupanua wigo wa huduma zake hadi katika ukanda wa bahari.

**Serikali kuchelewa kulipa madeni kwa Taasisi zake**

**Mheshimiwa Spika**, Kumekuwa na desturi ya Taasisi za Serikali na baadhi ya Wizara kutolipa madeni yake baada ya kupata huduma kutoka katika Taasisi nyingine za Umma. Kutolipia huduma hizo kunasababisha mlundikano wa madeni ya muda mrefu yanayochangia taasisi nyingi kushindwa kujiendesha pamoja na kushindwa kutekeleza miradi ya uwekezaji kutokana na kukosekana kwa fedha. Mfano wa Taasisi ambazo zinadai madeni makubwa ni TANESCO, TEMESA, TTCL na Shirika la Posta Tanzania (TPC)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi wa Taarifa ya Shirika la Ugavi wa Umeme (TANESCO) na kubaini kiasi kikubwa cha madeni ambacho Shirika linazidai Taasisi mbalimbali. Hadi kufikia Juni, 2017 TANESCO ilikuwa inadai jumla ya **Shilingi Bilioni 239.339**. Kati ya madeni hayo, Taasisi ambazo zinadaiwa kiwango kikubwa ni pamoja na ZECO **Shilingi Bilioni 135.7** ambapo, hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2018 deni la ZECO lilifikia Shilingi Bilioni 148.370 ikijumuisha VAT ya Shilingi Bilioni 24.755. Hivyo VAT ikiondolewa deni linalobaki ni Shilingi Bilioni 123.615. TANESCO pia inaidai DAWASCO **Shilingi Bilioni 31.6**, Jeshi la Wananchi (TPDF) **Shilingi Bilioni 8.8**, Magereza **Shilingi Bilioni 7.6**, Wizara ya maji Shilingi **Bilioni 6.2** na Hospitali ya Muhimbili **Shilingi Bilioni 3.2**.

Vile vile, Wizara na Taasisi za Serikali zimekuwa zikidaiwa fedha nyingi na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA). Madeni hayo makubwa yametokana na Taasisi za Serikali kuchelewa kulipa Ankara zao za huduma walizopewa baada ya TEMESA kuwafanyia kazi kulingana na taratibu zilizopo. Kukosekana kwa fedha hizo kunawasababishia TEMESA kukosa au kutopata vipuri kwa wakati kuwezesha kutoa huduma na hivyo kudhoofisha utendaji kazi wake.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa madeni katika Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) unaonesha kuwa, madeni ambayo Shirika linazidai Taasisi mbalimbali yameongezeka kutoka **Shilingi Bilioni 106.470** mwaka 2015/16 hadi kufikia **Shilingi Bilioni 155.630** mwaka 2016/17 ikiwa ni ongezeko la **Asilimia 46.2**. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, ongezeko hilo limechangiwa na deni ambalo TTCL imefanya biashara na Serikali kutokana na Mkongo wa Taifa (Government trade receivables)

Aidha, uchambuzi wa Kamati umebainisha kuwa, iwapo Taasisi za Serikali zikiwa na desturi ya kulipia huduma wanazozipata kutoka katika Taasisi za umma, zitazisaidia Taasisi hizo kuweza kuendesha miradi yake pamoja na kulipa madeni ya wazabuni wao.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini Serikali kushindwa kulipa madeni yake kwa wakati kwa Shirika la Posta Tanzania (TPC). Shirika lilikabidhiwa jukumu la kuwalipa kwa niaba ya Serikali wastaafu waliokuwa wafanyakazi wa iliyokuwa Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki kwa ahadi kuwa, Serikali itakuwa ikirejesha fedha hizo. Shirika limeendelea kutimiza jukumu hilo kwa uaminifu mkubwa lakini Serikali imekuwa ikisuasua kurejesha kiasi kilichotumika ambacho kimsingi kinatolewa kwenye sehemu ya mapato ya Shirika yaliyopaswa kutumika kama fedha za uendeshaji. Tangu Mwezi Januari, 1994 hadi Mwezi Agosti, 2018, Shirika limelipa jumla ya **Shilingi 16,241,556,898/=** wakati Serikali imerejesha kwa Shirika jumla ya **Shilingi 11,104,270,665/=** na mara ya mwisho Serikali ilirejesha **Shilingi 2,700,000,000/=** mwezi Januari, 2016. Kwa muktadha huo, Shirika linaidai Serikali jumla ya **Shilingi 5,661,015,025/=.**

### Ukosefu wa Ufanisi katika Uendeshaji wa Taasisi za Umma

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi katika eneo la utendaji na Uendeshaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma kwa lengo la kubaini maeneo ambayo kama yakiboreshwa kunaweza kupatikana tija kubwa. Mfano ni mapitio ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) ambayo

yanaonesha kuwa, endapo sekta hii itasimamiwa kwa umakini inaweza kuchangia kiasi kikubwa kwenye pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** maeneo ambayo Kamati imeona yanapunguza ufanisi wa TPA ni pamoja na Muingiliano wa Mamlaka za Serikali, mapungufu katika matumizi mazuri ya TEHAMA na ushirikiano kati ya wadau wakuu wa bandari (port community). Changamoto ya muingiliano wa Mamlaka za Serikali ambazo ni wadau wa bandari, kuliwahi kusababisha TPA kukabiliwa na anguko la mapato lililotokana na kukimbiwa na wateja kutokana na utozaji wa kodi ya Ongezeko la Thamani kwa mizigo iendayo nchi jirani. Pia uamuzi wa Tanzania kukusanya kodi ya nchi jirani hasa DRC katika Bandari ya Dar es Salaam ulikimbiza wateja wengi hali iliyopelekea mapato ya Bandari na Nchi kwa ujumla kupungua. Aidha, Serikali iliondoa kodi hizo na kuifanya TPA kurejesha wateja wake.

Kutokana na athari zilizojitokeza katika suala la kutoza kodi ya Ongezeko la Thamani pamoja na kukusanya kodi ya nchi jirani ya DRC, Kamati inashauri kuwa, kama kukiwa na maamuzi ambayo kwa namna moja au nyingine yataathiri utendaji na ufanisi wa bandari, ni vyema kukawa na ushirikishwaji wa Taasisi mbalimbali za Serikali ikiwemo TPA ambae ndiye mdau mkubwa wa bandari kwa sababu madhara yakitokea muathirika mkubwa ni Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA).

**Mheshimiwa Spika,** utendaji wa bandari zetu unahusisha wadau na vitengo vingi mpaka mzigo ufike mikononi mwa mteja. Pamoja na uwepo wa matumizi ya Tehama mifumo inayotumika katika Taasisi hii haisomani pamoja na kuwa inafanya kazi kwa kutegemeana. Hali hii huchangia kuchelewesha mizigo ya wateja na kutoa mianya ya ubadhilifu. Eneo jingine ni ushirikiano mdogo wa Taasisi ambazo kwa njia moja au nyingine uwepo wao unatakiwa katika kuondosha mizigo bandarini. Ushirikiano mdogo miongoni mwa wadau wa bandari (port community)

hatimaye huchangia kwa kiasi kikubwa kupungua kwa ufanisi hali inayopelekea wateja kuzikimbia bandari zetu.

**Mheshimiwa Spika**, eneo jingine linalochangia ukosefu wa ufanisi na tija katika taasisi za Umma ni ikama ya watendaji. Taasisi zilizo nyingi hazina watendaji kwa idadi inayotakiwa lakini hata watendaji waliopo hawana ujuzi na weledi kuendana na uchumi wa dunia ya sasa. Ni mapendekezo ya Kamati kuwa wapatikane watendaji wa kutosha kutekeleza majukumu ya Taasisi husika lakini na watendaji wote wawezeshwe kupata ujuzi na weledi unaotakiwa.

**Mheshimiwa Spika,** suala la nidhamu ya utendaji katika Taasisi za Umma ni eneo jingine linalochangia kushuka kwa ufanisi. Kumekuwepo na matumizi yasiyokuwa na tija katika Taasisi hizo, lakini pia utendaji wa wafanyakazi mmoja mmoja kutojituma na kutochangamkia kazi ni maeneo ambayo yanapunguza tija. Hali hii ni tofauti na Taasisi binafsi na hasa zile za kimataifa. Kamati inashauri eneo hili liangaliwe kwa kina na ikibidi watendaji wapewe malengo kwa vipindi maalum na wawajibike kwa utendaji wao.

**Baadhi ya Bodi za Wakurugenzi za Taasisi kutokuwa hai**

**Mheshimiwa Spika**, Bodi za Wakurugenzi ndizo zinazosimamia Taasisi na Mashirika ya Umma kwa niaba ya Serikali. Bodi hizo zimekuwa na majukumu mbalimbali ikiwemo kusimamia utendaji wa Mashirika na Taasisi za Umma, kuchambua na kupitisha nyaraka za kisera na kuwasilisha ofisi ya Msajili wa Hazina kwa uchambuzi, Kuingia Mkataba wa kiutendaji na Mtendaji Mkuu na kuhakikisha malengo yaliyokubaliwa yanatekelezwa na Kuidhinisha na kufuatilia miradi ya uwekezaji katika Mashirika. Kwa muktadha huo, kukosekana kwa bodi za Wakurugenzi kunasababisha Taasisi na Mashirika ya Umma kuwa na utendaji usioridhisha na usio na tija kwa Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa Rais amekuwa akifanya teuzi nyingi sana za Wenyeviti mbalimbali wa Bodi ili kuhakikisha kunakuwa na usimamizi mkubwa katika Taasisi na Mashirika

ya Umma. Changamoto kubwa iliyopo ni kuchelewa kwa uteuzi wa Wajumbe wa Bodi ambao wamekuwa wakiteuliwa na Wizara husika. Hali hiyo imekuwa ikisababisha Bodi hizo kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu kutokana na kutokuwepo kwa wajumbe wa bodi na kusababisha hasara kubwa katika Taasisi na Mashirika ya Umma.

Aidha, Serikali ingekuwa na mpango wa muendelezo (succession plan) katika uteuzi wa Wajumbe wa Bodi za Taasisi za Umma ili ukomo wa ujumbe katika bodi hizo usimalizike kwa wakati mmoja.

**Utendaji wa Ofisi ya Msajili wa Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 12 ya Nyongeza ya 8 (b) ya kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, Kamati hii pamoja na majukumu mengine ina jukumu la Kuchambua na Kujadili Taarifa ya Mwaka ya Msajili wa Hazina na Mashirika ya Umma na Kampuni ambazo Serikali ina hisa. Kamati inapenda kutoa taarifa kuwa kwa kipindi chote cha uhai wa Bunge la Kumi na Moja haijapokea Taarifa ya Mwaka ya Msajili wa Hazina hali ambayo inafanya utendaji wa Kamati uwe mgumu. Hii ni kutokana na ukweli kuwa, kama ilivyoelezwa katika Kanuni iliyorejewa hapo juu Taarifa hii ndio msingi wa shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Msajili wa Hazina ina jukumu la kusimamia Taasisi na Mashirika ya Umma yapatayo 270 lakini tathmini ya kamati imebaini upungufu wa ikama ya watumishi na matumizi duni ya TEHAMA. Maoni ya Kamati ni kuwa, ili ofisi hii iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu inapaswa kuwa na watendaji wa kutosha na wenye ujuzi na weledi katika mambo wanayoyasimamia pamoja na mfumo mmoja wa TEHAMA utakaowawezesha kuwasiliana na Mashirika ya umma kwa mara moja.

***Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati***

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma iliwasilisha Taarifa yake Januari, 2017 mbele ya Bunge lako

Tukufu. Taarifa hiyo ilijumuisha Maoni na Mapendekezo ya Kamati ambayo Serikali ilitakiwa kuyafanyia kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika Taasisi na Mashirika ya Umma. Kamati imekuwa ikifuatilia utekelezaji wa mapendekezo yake kupitia kwa Msajili wa Hazina ambaye ndiye msimamizi mkuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma kwa niaba ya Serikali.

Hata hivyo, baadhi ya mapendekezo yaliyototewa na kamati hayajafanyiwa kazi kikamilifu na Serikali hali inayosababisha Utendaji na Uwekezaji wa baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma kutokuwa na ufanisi na tija. Hoja ambazo utekelezaji wake haujakamilika kikamilifu ni kama ifuatavyo:-

i) Kamati ilipendekeza Serikali ipeleke mitaji kwa Taasisi na Mashirika ya Umma ambayo iliahidi kufanya hivyo wakati wa uanzishwaji wa Taasisi hizo ili ziweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na tija. Aidha, pamoja na mapendekezo hayo muhimu kwa Serikali, bado kuna Taasisi za Umma ambazo hazina mtaji wa kutosha hali inayosababisha Taasisi hizo kushindwa kutekeleza miradi ya uwekezaji na kupata mapato yatokanayo na uwekezaji. Baadhi ya Taasisi ambazo hazina mtaji wa kutosha ni Benki ya Posta Tanzania, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania, Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) na Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC).

ii) Hoja nyingine ambayo haijafanyiwa kazi kikamilifu ni kutokuwepo kwa uwiano mzuri wa mapato na matumizi. Kamati ilipendekeza Serikali iziagize Taasisi na Mashirika ya umma kuzingatia Sheria ya Msajili wa Hazina Sura 370 na kuziwajibisha endapo zitavuka kiwango cha matumizi cha Asilimia 60 ya mapato ghafi. Hata hivyo, bado kuna Taasisi ambazo matumizi yake ambayo hayaendani na uwekezaji yanazidi Asilimia 60 na hazijachukuliwa hatua yoyote licha ya kwamba ni kosa kisheria.

iii) Hoja ya Serikali na Taasisi zake kutolipa madeni yake kwa wakati bado haijafanyiwa kazi kikamilifu na Serikali kwa kuwa Serikali imekuwa na desturi ya kutolipia huduma inazozipata kutoka katika Taasisi za Umma na kufanya Taasisi hizo kushindwa kujiendesha.

iv) Kamati ilipendekeza Serikali izisimamie vizuri Taasisi zake za Umma ili ziweze kuwa wabunifu na kutumia rasilimali walizonazo kwa ufanisi ili ziweze kujiendesha kibiashara, kuzalisha mapato, kupunguza na hata kuachana na utegemezi wa ruzuku ya Serikali. Aidha, pendekezo hili halijafanyiwa kazi kikamilifu kwa kuwa bado Serikali ina mzigo mkubwa kwa kuhudumia Taasisi ambazo kama zingesimamiwa vema na kutumia rasilimali walizonazo kwa ufanisi wa hali ya juu zingezalisha mapato ya kutosha na kuweza kujiendesha na kuachana na utegemezi wa ruzuku ya Serikali.

## SEHEMU YA TATU

## MAONI NA MAPENDEKEZO

### *Maoni*

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi wa kina uliofanywa na Kamati kuhusiana na Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kamati inapenda kutoa maoni ya jumla kama ifuatavyo:-

Taasisi na Mashirika ya Umma yanatakiwa kuwa na mtazamo wa kibiashara ili yaweze kutumia kikamilifu rasilimali walizonazo kwa ajili ya kuzalisha mapato ya kutosha na kuondoa utegemezi wa ruzuku ya Serikali. Kwa kufanya hivyo kutaisaidia Serikali kutekeleza miradi mingi zaidi ya kimkakati na itakayoleta tija kwa Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kuwa Dhima ya Serikali kuwekeza katika Mashirika ya Umma ni kukuza Uchumi wa Nchi kwa madhumuni ya Kupata mapato kwa njia ya faida/ gawio, kusogeza na kutoa huduma kwa urahisi kwa jamii na kuchochea maendeleo ya sekta mabalimabli za uchumi, kudhibiti utoaji wa huduma na kulinda Maslahi ya Jamii (Wazalishaji na Watumiaji) na Kutengeneza ajira kwa wananchi. Hata hivyo, kama Taasisi na Mashirika ya Umma yatashindwa kujiendesha kwa faida na kukosa tija na ufanisi Serikali itashindwa kufikia dhima yake.

**Mheshimiwa Spika**, Dhamira ya Serikali ya kuzitaka Wizara zote pamoja na Taasisi zilizo chini yake kuhamia Dodoma ni njema sana kwa kuwa ndio Makao Makuu ya Nchi. Pamoja na nia hiyo njema, kamati inashauri kuwa, Taasisi ambazo biashara yake kubwa ipo katika Jiji la Dar es Salaam, Serikali iangalie busara ya kubakisha makao makuu ya Taasisi hizo Dar es Salaam badala ya kuzihamishia katika Jiji la Dodoma. Mfano wa Taasisi ambazo kimsingi shughuli kubwa zinafanyika katika Jiji la Dar es Salaam ni Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Shirika la maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL)

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inategemea kupata faida kwa njia ya gawio au mchango katika Mfuko Mkuu wa Serikali pamoja na upatikanaji wa huduma bora kwa wananchi kutokana na uwekezaji uliofanywa. Mapato yatokanayo na uwekezaji uliofanywa na Serikali yanaiwezesha Serikali katika kutekeleza miradi mbalimbali ya uwekezaji. Kamati inashauri kuwa, Taasisi na Mashirika ya Umma yaongeze ufanisi katika utendaji wake ikiwa ni pamoja na kuwa na mtazamo wa kibiashara ili kuongeza mapato kwa kiasi kikubwa ili Serikali iweze kupata fedha za kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Mapato ya jumla kutokana na uwekezaji uliofanywa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Juni, 2018 ni **Asilimia 1.22** tu ya uwekezaji wa **Shilingi 55,178,297,752,577.60** uliofanywa katika taasisi na mashirika na Makampuni ambayo Serikali ina hisa. Mapato hayo ni madogo sana na yataongezeka iwapo Taasisi na Mashirika ya Umma na Makampuni ambayo Serikali ina hisa yatajiendesha kwa kuzingatia taratibu na Sheria na miongozo ya biashara. Aidha, Kamati inashauri Taasisi zote zinazotoa huduma ziboreshe huduma zake kwa maslahi mapana ya nchi.

***Mapendekezo***

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kutoa maoni ya jumla ya Kamati yaliyotokana na uchambuzi wa mitaji ya umma, naomba kutoa mapendekezo ya kamati kama ifuatavyo:-

**kukosekana kwa Sera ya Gawio (Dividend Policy) kwa Taasisi na Mashirika ya Umma**

**KWA KUWA**, Sera ya Gawio ni mwongozo unaoweka bayana mgawanyo wa faida baada ya kodi na kiasi cha asilimia ambacho kinapaswa kutolewa kwa wana hisa na kiasi kinachopaswa kuelekezwa katika uendelezaji wa biashara ya Taasisi,

**NA KWA KUWA**, kukosekana kwa Sera hiyo kunasababisha Taasisi na Mashirika ya Umma kukosa nyenzo muhimu ya kuipatia Serikali mapato kwa sababu viongozi wa Taasisi wamekuwa wakiamua na kujipangia kiasi cha gawio cha kupeleka Serikalini hata kama kiasi hicho hakiendani na kiwango cha uwekezaji uliofanywa na Serikali na faida iliyopatikana kwa Taasisi,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linashauri kuwa Serikali kupitia Msajili wa Hazina ihakikishe kila Taasisi inayotakiwa kuwa na Sera ya Gawio (dividend policy) inakuwa na Sera hiyo ili Serikali iweze kupata mapato ya kutosha.

**Utegemezi Mkubwa wa Ruzuku ya Serikali**

**KWA KUWA**, baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma yanashindwa kutumia ipasavyo rasilimali walizo nazo kwa ajili ya kujiongezea mapato bila ya kutoka katika jukumu lao la Msingi,

**NA KWA KUWA**, Kushindwa kuongeza juhudi katika utafutaji wa fedha kunasababisha Taasisi hizo kutegemea kwa kiasi kikubwa ruzuku kutoka Serikalini na kukwamisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaishauri Serikali kuzisimamia vema Taasisi na Mashirika ya umma ili zijikite katika jukumu lake la msingi. Kufanya hivyo, kutaziwezesha taasisi hizo kuwa na utendaji wenye ufanisi na tija na kuongeza mapato kutokana na majukumu hayo ikiwa ni pamoja na kuondokana na utegemezi wa ruzuku ya Serikali.

**Ukosefu wa Sera ya Uwekezaji, Mpango Mkakati na Mpango wa Kibiashara kwa Taasisi zinazofanya uwekezaji**

**KWA KUWA**, Taasisi na Mashirika ya Umma yanatakiwa kuwa na nyaraka mbalimbali kama Sera ya Uwekezaji, Mpango Mkakati na Mpango wa Biashara ili Taasisi hizo ziweze kujiendesha kibiashara na kuwa na ufanisi wa kutosha

**NA KWA KUWA**, Kukosekana kwa Nyaraka hizo kunazifanya Taasisi za Umma kukosa nguzo muhimu katika uendeshaji wake kwa kuwa nyaraka hizo ni nguzo katika utekelezaji wa majukumu ya Taasisi,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linashauri kuwa Serikali kupitia Msajili wa Hazina ihakikishe Taasisi na Mashirika yote ya Umma yanaandaa nyaraka zote muhimu zinazotakiwa katika uendeshaji wa Taasisi na kuhakikisha nyaraka hizo zinatumika kikamilifu.

**Upungufu wa Mitaji pamoja na Fedha za utekelezaji wa Miradi ya Uwekezaji**

**KWA KUWA**, baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma yamekuwa na changamoto kubwa ya upungufu wa Mtaji kutokana na Serikali kushindwa kukamilisha jukumu lake la kupeleka fedha za uendeshaji katika Taasisi zake,

**NA KWA KUWA**, upungufu huo wa mtaji umezifanya Taasisi hizo kushindwa kutekeleza miradi mbalimbali ya uwekezaji na kuongeza gharama za uendeshaji,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linashauri kuwa Serikali ipeleke mitaji ya kutosha kwa Taasisi na Mashirika ya Umma kama ilivyoahidi wakati wa uanzishwaji wa taasisi hizo na kama fedha hizo zilivyoidhinishwa na Bunge.

**Ukiukwaji wa Sheria ya Fedha Na 16 ya 2015 Kifungu cha 46 (10)(A)(1)**

**KWA KUWA**, baadhi ya Taasisi za Umma zimekuwa zikikiuka Sheria ya Fedha Na 16 ya 2015 kifungu cha 46 (10)(A)(1)

inazozitaka Taasisi za Umma kudhibiti matumizi yake ya gharama za uendeshaji na kutozidi Asilimia 60,

**NA KWA KUWA**, kutofuata matakwa ya Sheria na kuwa na matumizi makubwa yanasababisha Taasisi kukosa faida na kushindwa kutoa gawio au kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linashauri kuwa Serikali izichukulie hatua Taasisi zote zinazokiuka matakwa ya Sheria ya Fedha Na 16 ya 2015 ili Taasisi hizo ziweze kupunguza matumizi na kutengeneza faida.

**Utekelezaji wa miradi ya uwekezaji kwa baadhi ya Taasisi za Umma**

**KWA KUWA**, baadhi ya Taasisi zilizoanzishwa na Serikali ni za kimkakati na hivyo kuwa na miradi na shughuli nyingi zenye fursa kubwa ya kuchangia katika uchumi na ustawi wa Taifa. Hata hivyo, shughuli/miradi mingi haitengewi rasilimali za kutosha katika kuziendeleza kwa wakati ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa mikakati ya kutekeleza miradi hiyo,

**NA KWA KUWA,** kukosekana kwa rasilimali za kutosha na mikakati ya kutekeleza miradi ya Taasisi hiyo kunasababisha Taasisi hizo kushindwa kutekeleza miradi mikubwa yenye tija kwa ukuaji wa uchumi,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linashauri kuwa Serikali ihakikishe inawekeza na kuwa na usimamizi madhubuti katika Taasisi zake za kimkakati kama Shirika la Maendeleo ya Taifa (NDC) ili Taasisi hizo ziweze kuendesha miradi ya maendeleo kwa ufanisi.

**Taasisi kushindwa kutekeleza Sera na Miongozo ya Ushiriki wa Sekta Binafsi na Sekta ya Umma (PPP) katika kuendesha Miradi**

**KWA KUWA**, Serikali imekuwa ikitakiwa kutoa fedha zote za uendeshaji wa miradi kwa Taasisi na Mashirika ya Umma lakini fedha hizo zimekuwa zikipatikana kwa kusuasua,

**NA KWA KUWA**, kukosekana kwa fedha hizo kumesababisha Taasisi hizo kushindwa kutekeleza miradi yake ya uwekezaji kwa wakati na kukosa tija iliyotarajiwa,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linashauri Serikali kuzitaka Taasisi na Mashirika yake kuingia katika ubia na Sekta binafsi (PPP) katika utekeleaji wa miradi ya uwekezaji ili kuipunguzia mzigo Serikali na kuwezesha utekelezaji wa miradi yake kwa wakati.

**Uwepo wa baadhi ya Sheria zilizoanzisha Taasisi na Mashirika ya Umma kutoendana na wakati wa sasa**

**KWA KUWA**, Sheria zinazotumika na baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma zimepitwa na wakati kutokana na kuwa ni za muda mrefu,

**NA KWA KUWA**, kupitwa huko na wakati kunazifanya Taasisi na Mashirika hayo kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa ufanisi katika mazingira ya sasa,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linashauri Serikali kuleta Bungeni mapendekezo ya kuzifanyia marekebisho Sheria zote za Taasisi ambazo zimepitwa na wakati ili kuziwezesha Taasisi hizo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwenye mazingira ya sasa yenye ushindani mkubwa wa kibiashara.

**Serikali kuchelewa kulipa madeni kwa Taasisi zake**

**KWA KUWA**, Taasisi za Serikali na baadhi ya Wizara zimekuwa na desturi ya kutolipa madeni yake baada ya kupata huduma kutoka katika Taasisi nyingine ya Umma,

**NA KWA KUWA**, kutolipia huduma hizo kunasababisha mlundikano wa madeni ya muda mrefu yanayochangia Taasisi nyingi kushindwa kujiendesha pamoja na kushindwa kutekeleza miradi ya uwekezaji kutokana na kukosekana kwa fedha,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linashauri kuwa Serikali pamoja na Taasisi zake ilipe madeni yote yanayotokana na kupata huduma kutoka katika Taasisi nyingine ili Taasisi hizo ziweze

kutumia fedha hizo kujiendesha na kutekeleza miradi mbalimbali ya uwekezaji.

**Ukosefu wa Ufanisi katika Uendeshaji wa Taasisi za Umma**

**KWA KUWA**, baadhi ya Taasisi zimekosa ufanisi katika matumizi mazuri ya Tehama pamoja na kutokuwa na ikama ya watumishi na kukosekana kwa nidhamu na weledi kwa baadhi ya watumishi,

**NA KWA KUWA**, kukosekana kwa ufanisi katika utendaji na uendeshaji wa Taasisi hasa matumizi ya Tehama, kutokuwa na Ikama na nidhamu na weledi kwa watumishi kunasababisha Taasisi hizo kukosa tija na kupoteza dhumuni la uanzishwaji wa Taasisi hizo,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linashauri kuwa Serikali kupitia Msajili wa Hazina ihakikishe Taasisi zake zinawekeza katika Tehama pamoja na kuwa na vipimo vya utendaji kazi kwa kila mtumishi ili kuhakikisha kunakuwepo na tija iliyotarajiwa.

**Baadhi ya Bodi za Wakurugenzi za Taasisi kutokuwa hai**

**KWA KUWA**, kumekuwa na changamoto ya Wizara kuchelewa kufanya uteuzi wa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi wa Taasisi mbalimbali ambazo ujumbe wa bodi hizo unakuwa umekwisha muda wake,

**NA KWA KUWA**, kukosekana kwa bodi hizo kunasababisha Taasisi za Umma kuwa na utendaji usioridhisha na usio na tija kwa Taifa kutokana na kukosekana kwa Msimamizi wa Taasisi hizo kwa niaba ya Serikali,

**Kwa hiyo basi**, Bunge linashauri kuwa Serikali ihakikishe inakuwa na mpango wa muendelezo (succession plan) katika uteuzi wa Wajumbe wa Bodi za Taasisi za Umma ili ukomo wa ujumbe katika bodi hizo usimalizike kwa wakati mmoja.

**Utendaji wa Ofisi ya Msajili wa Hazina**

**KWA KUWA,** utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa kiasi kikubwa unategemea Taarifa ya Mwaka ya Msajili wa Hazina.

Aidha Ofisi ya Msajili wa Hazina ina changamoto ya matumizi ya Tehama pamoja na ikama ya watumishi,

**NA KWA KUWA,** kukosekana kwa Taarifa ya Mwaka ya Msajili wa Hazina kwa kiasi fulani kunakwamisha utekelezaji wa shughuli za Kamati kikamilifu, Vile vile, kutokuwa na matumizi mazuri ya Tehama pamoja na ikama ya watumishi kuna sababisha Ofisi ya Msajili wa Hazina kushindwa kusimamia na kuzifikia Taasisi na Mashirika ya Umma yote 270 kwa wakati,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaishauri kuwa

a) Serikali kupitia Msajili wa Hazina ihakikishe Taarifa ya Mwaka ya Msajili wa Hazina inaandaliwa na kuwasilishwa kwa wakati kwa ajili ya kuboresha utendaji wa Kamati

b) Serikali iongeze Bajeti ya Ofisi ya Msajili wa Hazina ili ifanye uwekezaji kwenye TEHAMA na kukalisha ikama ya watumishi ili kuwe na usimamizi madhubuti wa Taasisi na Mashirika ya Umma yote yaliyopo ndani ya Nchi kwa wakati ili kufikia malengo ya Serikali.

## SEHEMU YA NNE

## HITIMISHO

***Shukrani***

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa uongozi wenu makini ulioniwezesha kuwasilisha Taarifa hii hapa Bungeni. Aidha, Kamati imeweza kutekeleza majukumu yake kutokana na maelekezo ya kiti chako ikiwa ni pamoja na ushauri na msaada kwa kipindi chote cha utekelezaji wa shughuli za Kamati.

Kwa namna ya pekee, napenda kumpongeza Ndugu Athumani S. Mbuttuka kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kuteuliwa kuwa Msajili wa Hazina. Vile vile, napenda kumshukuru Msajili wa Hazina kwa ushirikiano wake wa dhati alioutoa kwa Kamati kwa kushauri namna bora ya kuzifanya

Taasisi na Mashirika ya Umma kuwa na ufanisi katika utendaji na uwekezaji wake na kuleta tija kwa Taifa ili kukamilisha dhima ya Serikali kufanya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Aidha, napenda kuwashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Msajili wa Hazina ambao wamekuwa wakishirikiana kwa karibu na Kamati katika kuhakikisha kunakuwa na usimamizi madhubuti wa Taasisi na Mashirika ya Umma.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa moyo na uadilifu mkubwa. Aidha nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya kamati na kunipa heshima ya kuiwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Zaynab Matitu Vulu, Mb – M/Mwenyekiti
3. Mhe. Amina Idd Mabrouk, Mb _ Mjumbe
4. Mhe. Atupele Fredy Mwakibete, Mb _ Mjumbe
5. Mhe. Charles John Mwijage, Mb _ Mjumbe
6. Mhe. Daimu Iddi Mpakate, Mb _ Mjumbe
7. Mhe. Desderius John Mipata, Mb _ Mjumbe
8. Mhe. Edwin Mgante Sannda, Mb _ Mjumbe
9. Mhe. Esther Alexander Mahawe _ Mjumbe
10. Mhe. Esther Amos Bulaya, Mb _ Mjumbe
11. Mhe. Esther Michael Mmasi, Mb _ Mjumbe
12. Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb _ Mjumbe
13. Mhe. Godfrey William Mgimwa, Mb _ Mjumbe
14. Mhe. Janet Zebedayo Mbene, Mb _ Mjumbe
15. Mhe. Juma Othman Hija, Mb _ Mjumbe
16. Mhe. Lolesia Jeremia Bukwimba _ Mjumbe
17. Mhe. Maftah Abdallah Nachuma, Mb _ Mjumbe
18. Mhe. Muhammed Amour Muhammed, Mb _Mjumbe
19. Mhe. Othman Omar Haji, Mb _ Mjumbe
20. Mhe. Qambalo Willy Qulwi, Mb _ Mjumbe
21. Mhe. Richard Philip Mbogo, Mb _ Mjumbe
22. Mhe. Sonia Jumaa Magogo, Mb _ Mjumbe
23. Mhe. Vuma Hole Augustine, Mb _ Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa ushirikiano wa hali ya juu alioutoa ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri stahiki na kuiwezesha kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa wakati. Shukran kwa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuratibu vema shughuli za kamati chini ya Mkurugenzi Ndugu Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Chikokoto na Makatibu wa Kamati Ndugu Amina Salumu na Ndugu Elieka Saanya na Msaidizi wa Kamati Ndugu Pauline Mavunde. Pia tunawashukuru Watumishi kutoka Ofisi ya Mshauri wa Mambo ya Sheria wa Bunge Ndugu Seraphine Tamba na Ndugu Matamus Fungo pamoja na Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge kwa ushirikiano wao mzuri.

***Hoja***

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii ni matokea ya uchambuzi wa kina kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma unaofanywa na Taasisi na Mashirika ya Umma, maoni na mapendekezo yanayotokana na uchambuzi uliofanywa na Kamati ni kwa lengo la kuishauri Serikali katika eneo la Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ili uwekezaji huo ulete tija kwa Taifa.

Naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa liipokee Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kuhusu uchambuzi wa uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kuijadili na hatimaye kuridhia Maoni na Mapendekezo yake ili hatimaye Serikali iyafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA**

02 Februari, 2019

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji, hoja imeungwa mkono, asante sana, Dkt. Raphael Masunga Chegeni.

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza sasa na mjadala kwa ujumla na tutawapa fursa Wabunge kuchangia taaifa zote mbili kwa pamoja tutaanza na Mheshimiwa Ester Bulaya, baadaye Mheshimiwa Bobali na Mheshimiwa Dkt. Kamala wajiandae.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, kwanza kabla sijaanza kuchangia, lazima nisisitize mambo ya msingi na kama Bunge lazima tuvae viatu vyetu katika kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa na tabia ya kutofanyia kazi Maazimio ya Bunge na Kamati yetu tumesema, na changamoto inayotokana na kutofanyia kazi maazimio ya Bunge lako tukufu ni kusuasua kwa uwekezaji na utendaji wa mashirika yetu, hilo ni jambo baya sana na inaonesha Serikali hii inalidharau Bunge na tumesema kwenye Kamati yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na Wabunge wenzangu, kuna suala la Kikanuni hapa kama ambavyo Kamati ya *PAC* na Kamati ya *LAAC* inavyofanyia kazi taarifa ya *CAG* sisi tunafanya kazi na Msajili wa Hazina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyoongea hatujawahi kupewa ripoti na Msajili wa Hazina, hili ni jambo la kikanuni na tulipohoji tukaambiwa taarifa inakwama Wizara ya Fedha, aibu, mnatufanya sisi tushindwe kufanya kazi yetu vizuri kwa niaba ya Bunge kwa kusimamia mashirika na kuja kuishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na shirika letu pendwa la ndege, ni jambo jema kufufua Shirika la Ndege na hakuna mtu anayepinga. Lakini tujiulize tunafufua wakati gani, tuna mipango gani, kwa malengo gani ya ushindani wa kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika letu la Ndege kwa miaka mitatu mfufulizo wametengeneza hasara ya bilioni 316, mnajua ni kwa sababu gani! Shirika halina mpango wa kibiashara. Kwa nini tusibebe kitimoto, tusibebe mbuzi, tusibebe samaki kwenye ndege ya abiria? Haya mambo hayatutendei haki kama Taifa, kwa mfano, tumewekeza. Kwa mfano trilioni moja kununua ndege, lakini hivi karibuni tumeambiwa shirika letu limeingiza bilioni nne halafu limeenda kufanyia ukarabati ndege mbili kwa bilioni 13. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Eeeh!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama haitoshi tuna upungufu wa marubani, Mwenyekiti wa Bodi alikuja kutuambia kwenye Kamati na ma-*engineer* yaani hivi ninavyowaambia marubani wa *bombadier* ndio wanaorusha *dreamliner. (Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani ni kama dereva wa Noah mkabidhi basi la Shabiby abebe abiria, ndio mambo hayo! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka Shirika letu la Ndege lakini lazima mambo kama haya yafanyiwe kazi ili Shirika letu liwe na ufanisi, lijiendeshe kibiashara, lakini tuwe na usalama wa abiria wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu imewekeza takribani shilingi trilioni 54 kwenye Mashirika ambayo yana hisa kuanzia asilimia 50 mpaka 100, lakini imepata faida asilimia moja tu. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Eeh!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewekeza trilioni 54 faida kwa mwaka 2017 ilipata bilioni

800 sasa hivi, kwa hesabu za Juni, 2018 faida iliyopatikana bilioni 600 pungufu ya bilioni zaidi ya 200. Hizo bilioni 200 mngenipa bilioni tano ningemaliza mradi wangu wa maji Bunda. Hizo bilioni 200 hapa kila Mbunge ana matatizo lukuki au basi *at least* mngeenda kupunguza ahadi yenu ya shilingi milioni 50 kila kijiji ambayo hamjaitekeza, tangu muingie madarakani. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti taarifa.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa.

**MHE. HALIMA J. MDEE**: Si ulikataza taarifa jana?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Bulaya kwamba analipotosha Bunge kwa sababu kwenye uwekezaji huwa kuna muda wa kupata *return on investment.* Sasa *ATC* imeanza haina miaka mingi anaanza kusema kwamba tayari inapata hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati kwenye biashara kuna kitu kinaitwa *alternative minimum tax,* Kampuni ikiendesha biashara kwa miaka mitatu kama haijapata faida, inaweza ika-*claim* wakati inaendelea kupata *return on investment*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilitaka nimpe taarifa kwamba kwenye biashara ni *practice* yaani huwezi ukaanza biashara leo, ukapata faida leo leo. Halafu lingine ningependa kumpa taarifa kwamba pamoja na huduma za *ATC…*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, *ATC* inatoa huduma, lakini wakati huo huo inatengeneza ajira. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Bashungwa, Mheshimiwa Esther taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala la upungufu wa marubani ni kadri *ATC* inavyozidi kupanuka.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Bashungwa taarifa hiyo Mheshimiwa

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutengeneza ajira kwa marubani na ma-*engineer*.

**MWENYEKITI:** Taarifa hiyo Mheshimiwa Ester.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niu-*junior* unamsumbua sio *type* yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nililotaka kulisema hapa, tumesema Serikali haitoa mitaji kwenye mashirika mbalimbali. Nitoe mfano, tumeanzisha Benki ya Kilimo, Benki yetu ya Kilimo, lengo kubwa la kuanzisha ni kusaidia wakulima wetu, Benki yetu ili isimame ilikuwa inahitaji Mtaji wa bilioni 800, lakini sasa hivi ina bilioni 60 tu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge mnakumbuka Kilimo ndio kinaajiri asilimia zaidi ya 70 ya Watanzania na kuna habari chini ya *carpet* kwamba benki hii, ambayo ina mtaji, wa bilioni 60 ndio alikuwa amepewa kazi ya kwenda kununua

korosho za bilioni 900 wapi na wapi? Aibu haiwezekani na ni kwa sababu Serikali haifatilii mashirika yake haifuatilii vyombo vyake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na hili pia sijui mnabisha?

**MHE. RICHARD P. MBOGO**: Taarifa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Mbogo.

**TAARIFA**

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji ambaye ni Mjumbe mwenzangu, Benki ya Kilimo ilianzishwa kwa mtaji wa bilioni 60, lakini kwa jitihada za Serikali imeongezeka mtaji wa bilioni 200 kama na kumi, kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika na nusu imekwisha pokelewa na nusu nyingine ikapokelewa hivi punde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile gawio la faida la kutoka bilioni 880 na kupungua mpaka kufika bilioni 600 lilitokana na kwamba katika bilioni 800 Sheria ya Bajeti ya *retained earnings* ambazo zimebaki asilimia 70 zilichukuliwa kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, kupungua huko, kutoka bilioni 800 mpaka bilioni 600 ni kwa sababu ya sheria tulichukua asilimia 70 ya *retain earnings* zikaenda kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya taarifa hiyo.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei angesema hiyo pesa, hiyo pesa anayoisema ni mkopo kutoka *TIB* yaani Benki yenye mtaji wa bilioni 60 unaenda kukopa kuipa bilioni mia mbili naa; na hapa kwenye taarifa yetu tumesema kuna hatari ya benki kufilisika kwa sababu itashindwa kulipa deni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ambalo nataka kusema hapa ni Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi kukopa bila kulipa madeni kwa taasisi zake na kusababisha utendaji mbovu wa mashirika *TANESCO* inadai zaidi ya bilioni mia mbili naa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye ripoti yetu utaona JWTZ inadaiwa Bilioni 8...

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa muda wako umemalizika Mheshimiwa Ester.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Ya kwanza eehe.

**MWENYEKITI:** Ya kwanza eeh, haya Taarifa Mheshimiwa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Na ulinde muda wangu.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana, tunapoongelea mashirika kufa, kwa watu kutolipa madeni, tusisahau deni la Mwenyekiti wa CHADEMA ambalo alipangishwa bilioni 1.2 kulipa kodi kwa *NHC. (Vigelegele/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yake siipokei kwa sababu SUMA JKT, viongozi wa Chama cha Mapinduzi wamekopa matrekta na hamjalipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, JWTZ inadaiwa bilioni nane, Wizara ya Maji - *DAWASA* inadaiwa bilioni sita, Wizara ya Afya - Muhimbili inadaiwa bilioni 2 na maeneo mengine. Lakini tunajua mbali ya madeni, ambayo...

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Taarifa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:...***TANESCO* inaidai Serikali, Shirika hili linashindwa kujiendesha, kwa sababu inashindwa kulipa madeni, na hela nyingi zipo kwa Serikali. Serikali inaua Mashirika yake…

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti**,** taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Ester taarifa tafadhali, Mheshimiwa Waziri.

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Esther Bulaya anayezungumza, kwamba *commitment* ya Serikali ndani ya Shirika la *TANESCO* kwanza sasa hivi, anaposema *TANESCO* inashindwa kujiendesha, *TANESCO* sasa hivi, haipokei ruzuku yoyote kutoka Serikalini na miaka ya nyuma kabla ya Serikali hii ya Awamu ya Tano haijaingia madarakani *TANESCO* ilikuwa inapokea zaidi ya bilioni 200. Lakini kwa sasa hivi, haipokei na uwekezaji mbalimbali *TANESCO* imekuwa ikifanya na miradi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, sambasamba na hilo, napenda niseme pia…

**MBUNGE FULANI:** Lipeni madeni.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI: ...**hii *commitment* ya Serikali katika utekelezaji wa miradi mikubwa, kwa mfano *Kinyerezi I Extension, Kinyerezi II* na miradi mbalimbali.

**MBUNGE FULANI:** Nazungumzia madeni, madeni

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: ...**miradi mbalimbali inafanywa na Serikali Kuu, kwa hiyo akisema Serikali inaikwamisha *TANESCO* sio kweli. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndio nimesema moja ya maazimio ambayo hayajafanyiwa kazi kwenye taarifa yetu ya mwaka jana ni pamoja na Serikali kutolipa madeni, hapo sijazungumza madeni ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, takribani...

**MBUNGE FULANI:** Taarifa Mwenyekiti.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** mmefilisi nyie.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Ester, Taarifa.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa taarifa toa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni taarifa ya Kamati na imesisitiza kwamba Serikali haifanyii kazi Maazimio ya Bunge na haya ni miongoni mwa Maazimio ya Bunge ya mwaka jana na mwaka huu tumerudia tena. Lakini kuna ubadhirifu mkubwa, mkandarasi katika Uwanja wa Ndege wa Songwe amelipwa pesa zaidi ya bilioni 3.3 na kazi haijaisha na zoezi la kuweka taa katika Uwanja wa Songwe bado haijakamilika. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mwenyekiti muda.

**MWENYEKITI:** Malizia dakika moja.

**MBUNGE FULANI:** Mwenyekiti, muda, muda.

**MWENYEKITI:** Malizia**.**

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti**,** haya lazima tuyaseme kwa sababu wazalendo wanasema kwa lengo la kujenga, sisi wengine tusipokufa na ajali, tuna maisha marefu sana, tunahitaji Serikali itimize wajibu wake ili wananchi wapate huduma bora na mashirika yetu yafanye kazi, kwa ufanisi, lipeni madeni, acheni blah blah!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ester Bulaya*.*

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea mbele naomba tutambue uwepo wa wageni waliopo asubuhi hii, kuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge, kuna mgeni wa Mheshimiwa Kiza Mayeye ambaye ni rafiki yake kutoka Jiji la Dodoma Ndugu Leonard Mwasandube, karibu sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Kuna wageni watano Mheshimiwa Flatei Massay ambao ni Wapiga kura wake kutoka Mbulu Mkoani Manyara, wakiongozwa na Ndugu Adamu Hyayuma, karibu sana. Pia kuna wageni 21 wa Mheshimiwa Rashid Shangazi, kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndugu Abdallah Awadhi, naona hawapo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na mjadala wetu, lakini kutokana na muda na tunahitaji watu wachangie vizuri, mwisho wa taarifa ni mbili tu kuanzia sasa. Tunaendelea na Mheshimiwa Bobali baadae Mheshimiwa Zainab Vullu ajiandae.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii kuchangia. Niseme kwamba nimezipitia hizi taarifa za Kamati zote mbili; Kamati ya Bajeti na Kamati ya *PIC.* Niseme wazi kabisa kwamba

ninawapongeza sana Wajumbe wa *PIC* kwa kazi kubwa waliyoifanya na wameleta taarifa ambayo iko *very heavy,* nawashukuru sana na nawapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kuchangia jambo moja tu kwenye mjadala huu leo na jambo lenyewe si lingine ni korosho. Mimi nilitegemea Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti angetueleza kwamba hizi fedha ambazo Serikali wanatumia kununua korosho zimetoka kwenye kifungu gani, angeanzia hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, wakulima wamecheleweshewa fedha zao sana, hiyo haitoshi tumesikia juzi Serikali imeuza korosho tani laki moja. Binafsi nilimfuata Waziri nikaenda kumpongeza kwamba sasa najua wakulima watapata fedha zao. Cha ajabu korosho tani laki moja imeuzwa kwa mujibu wa maelezo ya Waziri wa Katiba, nilikuwa namuangalia, Serikali imeingiza shilingi bilioni 418 kwa tani laki moja. Kwa mahesabu ya kawaida itakuwa Serikali imeuza korosho kwa shilingi 4,180.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Serikali imeuza shilingi 4,180 Serikali ije itueleze mnaendelea kulipa *grade one* shilingi 3,300 kwa faida hii kubwa mliyoipata, hilo moja. La pili…

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili…

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa ya kwanza hiyo.

**T A A R I F A**

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali imeuza korosho kwa shilingi 4,000 na kitu halafu unawalipa wakulima shilingi 3,300 maana yake Serikali inafanya kangomba na hiyo ni kangomba kubwa sana tusiikubali. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Hakuna taarifa juu ya taarifa, Mheshimiwa Bobali endelea.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, nimeikubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha ajabu zaidi mimi nilimfuatilia Mheshimiwa Rais wakati anatangaza uamuzi wa kwenda kununua korosho alisema atanunua korosho za Watanzania wote kwa shilingi 3,300 hakuna kauli nyingine iliyotolewa na kiongozi yeyote mwingine kubatilisha bei hii.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Sasa hivi wakulima…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bobali taarifa subiri.

**T A A R I F A**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa muongeaji, kwanza anaaka kupotosha Bunge, Mheshimiwa Rais aliahidi kulipa shilingi 3,300 moja kwa moja kwa mkulima bila kuzingatia kuna watu wanadai hela za magunia, wabebaji, wasafirishaji, *cess* ya

Halmashauri. Kama Serikali imekwenda kuuza 4,000 maana yake hizo fedha zinazobaki zinakwenda kulipa hizo taasisi nilizozitaja. Kwa hiyo, ukisema kwamba Serikali inafanya kangomba ni upotoshaji mkubwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kuchauka, Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani nayo taarifa aliyonipa Mheshimiwa Kuchauka kwa sababu moja, Serikali ilikwenda kwenye Kamati ya Kilimo ikakiri kwamba korosho gharama yake ilivyo sasa ukijumlisha hizo zote ni shilingi 3,800; Serikali tena kwa taarifa yake yenyewe kabisa iliyo rasmi imekiri gharama ya korosho ni shilingi 3,800 ukijumlisha gharama hizo zote ambazo Mheshimiwa Kuchauka amezisema. Sasa kama mmeuza shilingi 4,180 tunataka kauli mtuambie hii iliyoongezeka mtawarudishia wakulima? Hilo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, sasa hivi ninapozungumza wakulima wanalipwa shilingi 2,640 hawalipwi tena shilingi 3,300...*(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Tayari mbili.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alisema korosho itakuwa...

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utararibu.

**MWENYEKITI:** Haya Kuhusu Utaratibu.

**KUHUSU UTARATIBU**

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe utaratibu...

**MWENYEKITI:** Kuhusu Utaratibu tafadhali tutulizane

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe utaratibu kwa mujibu wa Kanuni ya 64(a) ambayo inazungumzia kwamba...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tulizaneni mumsikilize basi kanuni iliyovunjwa, tuendelee Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Kanuni ya 64(a) Mbunge hatakiwi kusema uongo...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** ...anasema uongo.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Hamjamsikiliza sasa.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mbunge anasema uongo...

**MWENYEKITI:** Kwa nini hamsikilizi?

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Naomba uanze upya...

**MBUNGE FULANI:** Hakuna Kanuni ya 64(a), Kanuni ya 64(a) haipo...

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Nimesema 64(1)(a)...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Chief Whip.*

**MBUNGE FULANI:** Hakuna Kanuni ya 64(a).

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Unasema uongo kwa sababu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Manyanya naomba ukae.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Haipo 64(a).

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Hebu tulia huko, wewe nitakupeleka tena gerezani tena kakae kule, hujachoka kukaa gerezani wewe, hujachoka kukaa Segerea wewe ninavyoona.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Bulaya kama hatusikilizani hatutaweza kuelewa anachozungumza.

**MBUNGE FULANI:** Serikali haitulii!

**MWENYEKITI:** Si kwamba Serikali hawatulii na ninyi hamtulii...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Subirini basi, sasa kama mtu hajasikilizwa tutawezaje kujua amesema nini?

Waheshimiwa Wabunge tafadhalini kama mtu hataki kuchangia bora aseme aende akapumzike tuendelee na mjadala vizuri, hilo ndilo neno la mwisho; kwa sababu kama mtafanya vurugu mchango hautoenda vizuri. Kwa hiyo naomba tufuate utaratibu tuendelee na kazi yetu lakini tuzungumze maneno yaliyo sahihi si tunapeana taarifa hovyo bila mpango maalum kwa wakati tunazungumza maneno ambayo sio sahihi. Mheshimiwa Bobali naomba umalizie una dakika saba na nusu tu na mwenzio unayegawana naye. *(Makofi)*

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima sasa hivi wanalipwa shilingi 2,640; kama kuna Waziri ama Mbunge anasema nasema uongo akathibitisha kwamba mimi nasema uongo, nipo radhi kujiuzuru Ubunge kama unaweza kuthibitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mimi ninayoyasema kwamba wakulima hawalipwi shilingi 2,640 na anaweza kunithibitishia, nitajiuzuru Ubunge. Wakulima wanalipwa shilingi 2,640 Rais alisema wakulima wote watalipwa shilingi 3,300 kwa kuingiziwa moja kwa moja. Ni tamko gani la Serikali limetolewa na kiongozi yeyote wa Serikali likabadilisha bei hii? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Taarifa

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bobali inawezekana hiyo taarifa ikakutoa Ubunge, tumsikilize Mheshimiwa. Taarifa kwa ufupi...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Muda umeisha basi, haya kengele imeshapigwa muda umeisha Mheshimiwa kaa, muda umemalizika Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** *(Hapa alizungumza bila kutumia kipaza sauti).*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Sio ya kwanza dakika saba na nusu anagawana na mwenzake, Katibu mara ya ngapi, ya pili?

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Katibu anasema kengele ya pili hiyo.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Tumemaliza, Katibu amesema ni ya pili kwa hiyo tunaendelea na mchangiaji anayefuata Mheshimiwa Zainab Vullu na baadae Mheshimiwa Dkt. Kamala ataendelea dakika kumi kumi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Chief Whip.*

**MWONGOZO WA SPIKA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuomba Mwongozo wako. Kanuni zetu za Bunge zinatutaka kukaa ndani ya Bunge kwa utulivu, utulivu ni pamoja na kuchangia kupambana kwa hoja lakini si kwa utaratibu wa kuvunja nidhamu, kuzomea na kupiga kelele bila utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mjadala unaoendelea sasa ni mjadala muhimu; sisi kama Serikali tungependa kusikiliza

sana maoni ya Wabunge, lakini pale ambapo Wabunge wanavunja kanuni na kuanza kuzomea, kupiga kelele na kutuondoa katika usikivu na utaratibu wa Bunge, mimi naomba Mwongozo wako jambo hili kama linaruhusiwa ndani ya Bunge na katika uendeshaji bora wa shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Sasa nijibu miongozo yote miwili pamoja au kila mtu peke yake?

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Haya sema Mheshimiwa *Chief Whip*

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mjadala huu umeanza kumekuwa na tabia ya Mawaziri wa Serikali hii kuwajibu wachangiaji na wanachukua muda mrefu katika kutoa hoja zao. Kama hiyo haitoshi kumekuwa na tabia ya miongozo ambayo malengo yake ni kuwatoa kwenye mjadala wachangiaji na hii ndio imekuwa sababu ya kelele na fujo hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba mwongozo ako, ni kawaida au desturi ya Bunge hili Mawaziri kutoa miongozo au kuchangia kabla mjadala haujafungwa ili wapate haki ya kuchangia au ni namna gani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tusikilizane, ma-*Chief Whips* wote wawili wana lengo la tuendeshe Bunge kwa utaratibu na kwa nidhamu inayotakiwa, wote wana lengo hilo kila mmoja kwa upande wake. Lakini taarifa ni haki ya Mbunge, tunakubaliana na hilo kwa hiyo hatuwezi kuweka *limitation.* Ikiwa mtafanya vurugu kiti kina maamuzi ya kuzuia taarifa ili tuendelee na shughuli zetu. Kwa hiyo, ninachoomba

tuendelee vizurikuchangia lakini mtu asije akazungumza neno ambalo si la kweli ikawa tumenyamaza kimya, lazima apigwe taarifa kama kutakuwa na jambo kama hilo. Mawaziri wana muda wao wa kuchangia lakini naye pia mkipotosha Bunge ana haki ya kusimama na kutoa taarifa. *(Makofi)*

Tumemaliza hilo, kuna lingine?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tu uendelee kutupa mwongozo. Kwa mujibu wa Kanuni hoja ambazo zimeletwa mbele ya Bunge ni hoja za Kamati na si za Serikali na Mawaziri wanachangia kama Wabunge wengine na ndiyo maana Mawaziri hawahitimishi hoja hii na kama hawahitimishi wanayo haki na wao kuchangia na ndio maana wanapata muda wa kuchangia. Wana haki ya kuomba mwongozo, utaratibu na taarifa kwa sababu hoja hii ni ya Kamati na si ya Serikali. *(Makofi)*

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Sasa itakuwa ma-*Chief Whip* kazi yao kubishana hapa ndani leo. Tunamaliza hiyo hatuna tena taarifa wala nini, haya tuendelee.

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mila za Bunge hili kuna utaratibu maalum wa kuomba kuchangia na Mawaziri wana muda wao wa kuchangia. Vinginevyo naomba Mwongozo wako wanachokifanya hapa hawatapata tena muda maalum wa kuchangia kama Mawaziri? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tutulizane. *Chief Whip* Mheshimiwa Jenista yuko sahihi hizi ni Taarifa za Kamati kwa hiyo mtu yoyote humu ndani anakuwa kama Mbunge wa kawaida na mchangiaji wa kawaida, anaweza kutoa taarifa

wakati wowote. Hata hivyo maamuzi ya Kiti ndiyo ya mwisho kutoa taarifa, kwa sababu ikiwa mtaendelea kufanya vurugu, taarifa nitazuia na nikizuia taarifa mtu atakayechangia hovyo namtoa nje. Tuendelee sasa.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** *(Hapa alizungumza bila kutumia kipaza sauti).*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yussuf usinifundishe kazi. Tunaendelea sasa na Mheshimiwa Zaynabu Vulu na baadae Dkt. Kamala na Mheshimiwa Silinde wajiandae.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kusimama hapa leo na namuomba Mwenyezi Mungu alijalie Bunge hili tuendelee kujadiliana kwa salama na amani katika Kamati hizi mbili ambazo zinalenga kubeba uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwatoe hofu Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, inapotokea Mbunge yeyote anapochangia, anapotoka nje ya mstari msisite kusimama kwa mujibu wa kanuni na kufafanua yale ambayo yanapaswa yafafanuliwe. Maana kuna wengine hapa wanataka kutulisha matango pori na sisi hatutaki kula matango pori, tumeona bundi na bundi wameshindwa. Kwa hiyo, endeleeni kuchapa kazi na fanyeni kazi yenu kwa uadilifu kama ilivyo. Ninyi mnaisimamia Serikali na tunapaswa na wananchi wanapaswa kujua Serikali yetu inafanya nini, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia suala la uwekezaji. tunapozungumzia suala la uwekezaji Serikali inaweka mkono wake ili kuhakikisha uchumi na mapato ya nchi yetu yanaendelea. Niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuifufua *ATCL,* imenunua ndege sita hadi sasa na inahakikisha uchumi unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimsaidie mwanangu, mwanafunzi wangu Ester Bulaya, unapojua kuendesha gari

ya Volkswagen hushindwi kuendesha V8 na unapotoka kuendesha V8 huwezi kushindwa kuja kuendesha *beetle*, *IT* au *corolla* kama unavyosema mwenyewe. Kwa hiyo, mwanafunzi wangu naomba hilo ulizingatie usisahau ulipotoka. *(Makofi)*

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anapozungumzia...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** ...kwamba marubani wanakosea kukosea ndege, anataka kuupotosha umma. Mimi nasema Serikali imefanya jambo zuri na la uhakika kufufua uchumi wa ndege na kuendelea kujenga reli ya *SGR.* Ndege na reli zikiwa pamoja uchumi utaimarika.

Tunaomba tu Serikali ihakikishe na suala la bandari linawekwa katika moja ya ajenda zake ili wafanyabiashara badala ya kutumia magari kutoa hapa kupeleka maeneo mengine kwa kutumia barabara sasa wanaweza wakatumia hiyo reli na ikapokelewa bandarini na uchumi ukaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongeze kusema kwamba tunahitaji kuyasimamia na kuyaboresha mashirika yetu ya umma. Iangalie uwezekano, wa pale panapohitaji kupeleka mtaji basi ipeleke mtaji kwa wakati, wakati huo huo kuangalia rasilimali watu. Rasilimali watu katika mashirika yetu ni muhimu sana, wao ndio watasaidia kuhakikisha kazi zinakwenda vizuri na kwa weledi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala la bodi za Wakurugenzi na Wenyeviti, mashirika yahakikishe kwamba bodi za Wakurugenzi na Wenyeviti wanateuliwa kwa wakati ili waweze kusimamia shirika alilopangiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Shirika la SUMA JKT, hili shirika lina vitengo vingi vya kufanyia kazi, lakini nishauri kama Kamati ilivyoshauri, wale vijana wanaokwenda JKT iwe kwa mujibu wa sheria au kujitolea kuwekwe na sera ambayo itawasaidia na kusaidia shirika na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, wanaokwenda kufanya kazi za kujitolea, wafanye mafunzo ya kijeshi ambayo ni nidhamu, lakini baada ya hapo, waende kwenye Shirika la SUMA JKT ambako kule watafundishwa kushona, kulima, kutengeneza maji kwa ajili ya biashara; na mbinu za ujenzi na ujenzi ambao hauna gharama kubwa. Nao wakitoka hapo, wanakwenda kujiajiri wenyewe ama wanaweza wakaajiriwa kwenye Taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hili shirika likiwezeshwa vizuri, linaweza likasaidia, kwa mfano, tukisema shirika hili lipewe kazi ya kushona *uniforms* za Jeshi zote, kwa sababu tayari wana kiwanda cha nguo. Pia tunaweza tukasema washone viatu vya majeshi yote, kwa sababu tayari wana kiwanda cha kushona viatu na ngozi. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikaona ni jinsi gani tunaweza tukaisaidia SUMA JKT ikawa kiwanda cha kuzalisha bidhaa lakini vilevile ikawa kiwanda cha kuzalisha rasilimali watu, wakitoka hapo wakaenda kufanya kazi maeneo mengine ama wajiajiri wenyewe. Kwa sababu sehemu kubwa ya vijana wetu wako mitaani wamezagaa, wengine hawana utaalam lakini wana elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, elimu wanayoipata shuleni na elimu watakayokuwa wameipata vyuoni, wakienda huko wanaweza wakapata utaalam wa kuja kufanya kazi za kujipatia kipato; na vilevile kipato watakachopata kitakatwa kodi na hiyo kodi itaingia kwenye sehemu ya kipato cha Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri tukaona ni jinsi gani tunaweza kuisaidia Serikali kwa kuzalisha vijana ambao watakwenda kufanya kazi na kujiajiri, wakati huo huo SUMA JKT na yenyewe ikafanya kazi ya kuwafundisha hata maeneo mengine.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kidogo.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo, SUMA JKT wamekopesha matrekta...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali isimamie upatikanaji wa fedha ambazo zinatokana na malipo ya matrekta waliokopa watu. Matrekta hayo, mengine Wabunge tumo humo tunaodaiwa. Tunaomba Bunge lisimamie kama wamo Wabunge waliokopa, basi Serikali ilete barua huku ili hela zilizokopwa zirudishwe kwa wanaohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya *PIC.*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zaynabu Vullu, tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Kamala, baadaye Mheshimiwa Silinde na Mheshimiwa Mwijage wajiandae.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii muhimu kuchangia hoja tuliyonayo ambayo ni muhimu sana kwa uchumi wa Taifa, lakini pia na kwa maendeleo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia kwa kueleza dhana moja; na niseme kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati. Kwa hiyo, hoja ambayo napenda kuanza nayo ni kwamba ukiangalia taarifa mbalimbali za Benki ya Dunia, ukaangalia taarifa mbalimbali zinazotolewa na Shirika la Fedha Duniani *(IMF)* na taarifa mbalimbali ambazo tumepokea kwenye Kamati, zinabainisha kwamba uchumi wa Tanzania na baadhi ya nchi nyingine ndani ya *Sub-Saharan Africa* umekuwa ukikua kwa kasi kati ya chumi zinazokuwa kwa kasi. Ni jambo jema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wachumi tunafahamu kwamba katika uchumi huwa jambo moja likiwa jema huwa inamaanisha usiangalie hilo tu, huenda kuna jambo lingine jema zaidi. Sasa hatari ya uchumi, ukijikuta sana kufurahia jambo ambalo unaona ni jema ukasahau kwamba kuna lingine ambalo ni jema zaidi, basi unaweza ukajikuta unaendelea kuwa pale pale unafurahia na hilo dogo ambalo unafikiri ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kazi ya Bunge ni kushauri. Kwa hiyo, napenda kuishauri Serikali kwamba pamoja na ukweli kwamba uchumi wetu ni kati ya chumi zinazokua kwa kasi zaidi, lakini lazima tujue kwamba suala la uchumi kukua kwa kasi zaidi ni jambo moja, lakini kuna suala lingine uchumi huo una ukubwa kiasi gani? Kwa lugha nyepesi tunasema, *the size of the economy matters more. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili ili tuelewane, nitalieleza vizuri. Ukiangalia uchumi wa Marekani kwa mfano, *GDP* yao *size* ni 22 *trillion US Dollars.* Ukiangalia Ubelgiji, nchi ambayo ni ndogo, ukubwa wake ni *square kilometers* 36,000; ukiangalia Tanzania, ukubwa wa nchi yetu ni karibu 945,000 *square kilometers.* Kwa hiyo, utaona Wabelgiji wao *GDP* yao ni 540 *billion US Dollars.* Tanzania tunajitahidi, lakini ni *60 billion US Dollars.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa uchumi wa Ubelgiji ukikua hata kwa asilimia moja, maana yake kwao ni jambo kubwa. Uchumi wa Marekani hata ukikua kwa asilimia 0.5, maana yake hilo ni jambo kubwa. Kwa hiyo, hizi sifa za Benki ya Dunia na mashirika ya fedha duniani na wachumi wengi waliobobea wakikwambia wewe uchumi wako unakua kwa kasi na wewe ukafurahia ukapumzika, inawezekana ukawa haufikirii sawa sawa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachumi tuko ndani ya Bunge hili kushauri, ni lazima tuikumbushe Serikali kwamba ni vyema uchumi ukue vizuri, ni jambo jema, lakini kuna jambo lingine tunaweza tukafanya zaidi. Jambo hili ni lipi? Tuangalie *size* ya uchumi wetu, tuangalie *radical changes* zipi tunaweza

tukafanya ili walau ku-*double* uchumi wetu. Tunasema, *radical changes. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa kuna neno mara nyingi linaitwa *continuous improvement.* Mimi sio muumini wa *continuous improvement* kwa sababu mtu akikwambia uendelee kufanya *continuous improvement,* maana yake anakwambia uendelee kuonekana unaboresha kidogo kidogo lakini uendelee kukaa pale pale. Tunachohitaji ni kitu kinaitwa *radical change. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *radical change* mojawapo ambayo tumeanza kufanya ambayo nitaomba niipongeze Serikali, kwa mfano, kufanya maamuzi ya makusudi kabisa kwamba sasa tunataka tuwekeze kwenye *Stiegler's Gorge* tuzalishe Megawati 2,100, huo uamuzi ni *radical change.* Hawa rafiki zetu wa Benki ya Dunia, hawatakaa wakupongeze. Hawa watu wa Mashirika ya Fedha Duniani hawatakaa wakupongeze. Hawa wataalam wetu, wachumi wazuri sana wa huko pengine, hawatakaa wakupongeze, kwa sababu wanajua unachokifanya ni *radical change. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine ni *standard gauge.* Niseme tu, nilipata bahati wakati fulani kuwa Mwenyekiti wa Mawaziri wa Afrika Mashariki, sasa Wajapani tuliwapa kazi ya kutushauri kwamba je, hii *standard gauge* nchi za Afrika Mashariki tunaweza kufanya au tusifanye? Basi wakatoa fedha za kufanya utafiti ule; Wajapani hao, wakaja na utafiti wakasema, hizi nchi za Afrika Mashariki *standard gauge* ninyi bado sana. Mwendelee tu na hizo reli zenu mlizonazo msonge mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikamwuliza Mheshimiwa Rais, unajua ukiwa Waziri wa Afrika Mashariki au Mambo ya Nje, wewe siyo Waziri; Waziri ni Rais. Kwa hiyo, huwezi ukafanya jambo bila kumwuliza Rais wako. Nikamwuliza, tunaenda kufanya uamuzi, tufanyeje? Akaniambia msimamo wa *Cabinet* si unaujua? Nikasema

ndiyo. Akasema, ni *standard gauge,* hao Wajapani wasiwadanganye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilipofika pale kwenye kikao nikatumia Uenyekiti wangu vibaya, nikamwita Waziri wa Kenya nikamwambia unajua ni *standard gauge.* Unasemaje? Bwana yule akasema Mheshimiwa, lakini *standard gauge* nadhani Wajapani hawa wametupa hela, wamefanya na utafiti; nikasema sikiliza, hiyo siyo sahihi, ni *standard gauge.* Kwa hiyo, tulipoingia kwenye kikao, nilichofanya, nikawapeleka haraka haraka, wala sikuhoji sana, nikapitisha uamuzi ukaja wa *standard gauge. (Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo napenda nichangie ni kuhusu matumizi ya fedha za maendeleo. Ukiangalia taarifa tuliyopokea ya fedha za maendeleo jinsi zinavyotolewa, ukisoma vizuri na ukawa mkweli, lazima ushauri kwamba utolewaji wa fedha za maendeleo zinavyotolewa hazitolewi sawa sawa. Kwa nini? Ukiangalia fedha za maendeleo, kwa mfano, Wizara ya Mambo ya Ndani imepata asilimia 202 ya kile kilichokusudiwa. Sasa ni jambo jema ukiipa asilimia 202, sitaki kuuliza wamefanya nini Mambo ya Ndani, lakini sasa unapoanza kuangalia sekta nyingine ambazo unaona ni muhimu, unaona fedha za maendeleo hatujawapa kama ambavyo tulitarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Maliasili na Utalii hatujawapa hata shilingi moja za fedha ya maendeleo; siyo jambo jema hilo. Ukiangalia Wizara ya Afya tumewapa asilimia 14 peke yake, fedha za maendeleo; siyo jambo jema sana; ukiangalia Biashara na Viwanda tumewapa asilimia 6.96. Sasa kama tunajenga Tanzania ya Viwanda, mtu yeyote angetarajia sasa kwenye viwanda fedha ya maendeleo utapeleka nyingi. Siyo jambo jema pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *energy,* Wizara ya Madini, tumewapa asilimia 10, siyo jambo jema pia; ukiangalia *National Land Use Planning,* kitu ambacho ni muhimu, tumewapa asilimia sifuri, siyo jambo jema. Sasa

nafikiri kama Mbunge na kama mtu unakuwa mkweli, ni vizuri kuyasema haya. Hatujamaliza mwaka wa fedha, tuna miezi sita mingine inayokuja, basi tumshauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha aangalie afanye itakavyowezekana ili hizi sekta muhimu ambazo hazijapata chochote basi ziongezewe zipewe fedha nyingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lugola nadhani yuko humu ndani, ni rafiki yangu ananifahamu, tumefanya wote kazi, hizi asilimia 202 ulizopewa, mimi nadhani zinatosha, hebu sasa tupeleke fedha kwenye sekta nyingine ili tuweze kukuza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine ambali napenda nilichangie, ni muhimu sana. Ukisoma taarifa tulizopokea, kwenye ongezeko la mikopo, tunasema fedha za mikopo imeongezeka kwa asilimia 63 kwa sekta binafsi, kwenye madini imeongezeka kwa asilimia 9.8 na kwenye viwanda imeongezeka asilimia 4.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake ni nini? Ukiangalia hii asilimia 63 iliyoongezeka kwenye mikopo binafsi, hii ni mikopo kwa sababu watu ni wafanyakazi wanapewa mikopo ile ya mishahara; na ukiangalia hawa siyo kwamba wanakwenda kuwekeza. Hii ni mikopo ya kujikimu. Sasa kama...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Kamala. Nashukuru.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Silinde, baadaye Mheshimiwa Mwijage na Mheshimiwa Bashe wajiandae.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata fursa hii ya kuchangia Taarifa ya Kamati ya Bajeti. Nianze kwa kusema jambo moja tu; moja ya vitu ambavyo ninamwonea huruma sana Rais, Dkt. Magufuli, ni anazungukwa na watu wanaompa taarifa za uongo sana. Bahati mbaya sana, tunapokaribia kwenda kwenye Uchaguzi Mkuu, watu wanaongea uongo sana, yaani unaweza kumwambia mtu jambo ambalo hata yeye mwenyewe anajua kabisa unamdanganya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza hoja zilizokuwa zinajadiliwa tangu tulipoanza Bunge hili, hususan siku ya jana na mwendelezo wa siku ya leo, bado hatujibu maswali ya msingi wanayohitaji Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza kuiangalia Taarifa ya Kamati ya Bajeti, unaweza ukapata maelezo ambayo sisi Wajumbe tulikuwa tunapewa ndani ya Kamati ya Bajeti. Kuna vitu havipo kwenye taarifa yetu ambavyo ndivyo vingekuwa vina uwezo wa kujibu maswali ya msingi ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa tulipewa ya Mfuko wa Maji. Mfuko huu ambao Serikali ya Chama cha Mapinduzi ilisema inakwenda kumtua mama ndoo kichwani, kati ya shilingi bilioni 299.9 ambazo Serikali ilitakiwa itoe kupeleka katika Mfuko wa Maendeleo ya Maji, imetoa shilingi bilioni 1,637 sawa sawa na asilimia 0.6. Haya hampendi kuyasikia, lakini ndiyo ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wahisani waliahidi kutoa shilingi bilioni 284, mpaka sasa wametoa shilingi bilioni 4,320, sawa sawa na 4%. Haya sasa hebu niambie, unatatuaje tatizo la maji? Unamtuaje mama ndoo kichwani katika kipindi hiki cha miaka minne, kuelekea uchaguzi, hili haliwezi kuzungumzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliahidi ndani ya Bunge kwamba itamalizia majengo yote ya wananchi wa Tanzania waliyoyajenga kwa nguvu kazi yao; kwenye shule

na afya; kwa maana ya Shule za Sekondari na Msingi, maboma yote, waliahidi. Ikapigwa hesabu fedha iliyokuwa inahitajika katika mwaka wa fedha uliokuwa unapita, shilingi bilioni 251. Sisi kwenye Kamati ya Bajeti tulipambana na Wizara ya Fedha tukawaita mbele ya Kamati ya Uongozi Serikali ikaji-*comit* kwamba katika Mwaka wa Fedha unaokuja robo ya kwanza tutatoa shilingi bilioni 29. Mpaka leo tunavyozungumza, hawajapeleka hata senti moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya ndiyo maswali ya msingi ambayo wananchi wanataka majibu ya moja kwa moja. Sasa unakwenda kujadili mambo makubwa. Amezungumza vizuri sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Kamala, ukuaji wa uchumi. Kwenye takwimu za Serikali zinaji-*contardict* zenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kamati ya Bajeti, niwaeleze, katika mwaka wa fedha uliopita, ukisoma taarifa yao, inasema, mwaka wa fedha kipindi kama hiki kilichopita, ukuaji wa uchumi ulikua kwa asilimia 5.8, yaani Julai – Desemba na mwaka huu uchumi umekuwa kwa 6.0% yaani imeongezeka 2%. Ukirudi nyuma ukapitia taarifa ya mwaka 2018, uchumi wa Tanzania ulikua kwa 6.8%; yaani ni uongo uliopindukia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2018 kwenye taarifa yao ambayo ipo; sasa bahati mbaya sana, taarifa ambayo iko ndani ya *Hansard* ambayo Wabunge wote tunazo, mimi ninazo na Wabunge wote mnazo, labda kama hamsomi, inaonesha 6.8%. Taarifa ya leo imebadilisha matokeo ya mwaka 2018, halafu wanakuja wataalam wanakwambia huwa tuna-*adjust,* yaani *what a fix?* Yaani *can you fix a country like this? I wonder!* Hii ndiyo bahati mbaya. Sasa ndio watu waliopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakwenda kuangalia *DSE,* ndani ya mwaka mmoja Soko la Hisa la Dar es Salaam limepoteza mtaji wa shilingi trilioni nne. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Uuuiii!

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya hayazungumzwi na ndiyo yanayohusu mzunguko wa fedha wa Taifa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ndiyo Mheshimiwa Obama.

**T A A R I F A**

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa. Nakushukuru.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Nilisema taarifa ya mwisho ni mbili na ni maamuzi ya Mwenyekiti. Mheshimiwa Obama.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nilitaka kumwambia ndugu yangu, Mheshimiwa Silinde, tuko naye kwenye Kamati ya Bajeti na haya maswali tuliwauliza watu wa Wizara ya Fedha, kwa nini wakati mwingine *figures* zinabadilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uki-*compute* Pato la Taifa kwa kutumia *quarter* au nusu *quarter* au *three quarters,* ukija baadaye ukapiga ya mwaka mzima ile *aggregation* lazima ibadilike. Kwa hiyo, ninachotaka kukwambia, hayo yote Mheshimiwa Silinde ameambiwa, lakini anataka kupotosha Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Silinde.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi huwa sina muda wa kudanganya na sipendi kumjibu Mheshimiwa Obama, nafikiri alikuwa anatafuta tu nafasi ya kuzungumza humu ndani. *(Kicheko/Vigelegele/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mzunguko wa fedha ni asilimia 3.2, mfumuko wa bei ni asilimia 3.3. Uki-*calculate* namna ya ukuaji wa Pato la Taifa, tunakua kwa asilimia moja, wala siyo sita. Ukiwauliza Serikali juu ya hizi takwimu, soma taarifa ya Benki Kuu, soma taarifa wanayotoa Serikali, yaani ni vitu viwili *contrary.* Nami najua kwa nini *BoT* wanataja taarifa ya ukweli, ni kwa sababu inasomwa na *IMF,* inasomwa na *World Bank,* inasomwa na watu ambao wanajua. Taarifa ya wanasiasa inakuja kisiasa kweli kweli na hilo ndilo tatizo kubwa sana ambalo linalikabili Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Watanzania wanataka kujua maswali madogo madogo; mfumuko wa bei umeshuka kwa nini bei za vyakula, bei za bidhaa zinapanda? Serikali inapaswa kujibu mambo madogo madogo. unataka u-*deal* na *micro economy* ambayo hujaifanyia *feasibility study,* ni kama tu umekurupuka, hujui jambo lolote inavyokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa angalia matumizi; ukienda kuangalia kwenye Fungu la matumizi huku, unakuta Hazina, ndani ya nusu mwaka tulitakiwa tuwape bilioni 144 mpaka sasa wamepewa bilioni 414 asilimia 286. Ukiangalia Tume ya Uchaguzi 1.2 wamepewa *8.3 billion* sawasawa na asilimia 674. Kaangalie yale Mafungu yaliyozidishiwa fedha, narudia kusema, siku Mheshimiwa Dkt. Magufuli atakapomaliza utawala wake, mtu wa kwanza kwenda Jela atakuwa ni Katibu Mkuu wa Hazina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti,na msimdanganye, atakwenda, kwa sababu Mheshimiwa Rais akishaondoka madarakani hana *power* tena ya kumlinda mtu aliyeko. Anayekupenda anakwambia ukweli, ukipitia matumizi

kwenye hivi vitabu, mwakani *CAG* akipitia haya taarifa itakayoletwa ndani ya Bunge kutakuwa na zaidi, yaani matumizi ya fedha, mtakuja kuambiwa hapa, safari hii mmetajiwa *1.5 trillion,* itakuja trillion nane, kwa sababu fedha zilizokuwa *misallocated*, *is too much* na Bunge hatuletewi kile kitabu cha kuonesha Serikali inafanya *reallocation* kila mara, hakiji humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tungependa kufahamu, Serikali ni kwa nini hailipi fedha za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na mashirika ya umma, ni kwa nini Serikali katika robo ya kwanza mwaka 2018 tulipitisha kwenye fungu kwamba Serikali kama bilioni 60 za kulipa milioni 50 kila kijiji kwenye *pilot study,* mpaka sasa hivi, ni kwa nini hawjapeleka na ndiyo ahadi yao katika Uchaguzi Mkuu? Tunahangaika na uchumi mdogo ili kuutengeneza uchumi mkubwa, hilo ndilo ambalo tunalihitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na yote haya machache niliyoyasema, lakini naiomba Serikali pamoja na Kamati ya Bajeti tuliyopendekeza, siyo tu ije iyajibu, lakini tunataka *commitment* ya Serikali kwenye kutekeleza haya na wala siyo…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Silinde.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Mwijage.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Awali ya yote ningependa kuwapongeza Wenyeviti waliowasilisha taarifa za Kamati zao, ni Kamati nzuri, ni kioo, kinatuonesha tunafanya nini. Langu ningependa kuanza kuchangia Kamati ya Bajeti, mimi ni Mjumbe wa *PIC,* nampongeza *Comrade Simbachawene* na niende taratibu kwa sababu sijawa mzoefu. Nimpeleke ukurasa wa 22 alipozungumzia michezo ya kubahatisha, kwamba mapato ya Serikali kwenye michezo ya kubahatisha

yameongezeka, lakini michezo ya kubahatisha imeleta uzezeta, imeleta uzembe, watu hawafanyi kazi. Sasa hili la kupata mapato kwenye kuangamiza jamii ningependa tuliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti nimpeleke ukurasa wa 23 alipozungumzia mafuta ya kula na zile takwimu nzuri za upunguaji wa asilima 90 wakapendekeza zaidi kwamba tubaini endapo uzalishaji wa ndani umeongezeka, ningependa aongezee kwenye taarifa yake...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tutulie tumsikilize Mheshimiwa Mwijage.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa aende zaidi aangalie mchango wa *crude palm oil,* mchango wa mafuta ya kupikia katika *re-export* na aangalie mchango wa *re-export commodity* katika uchumi wa Taifa, aangalie viwanda vimeendeleaje baada ya maamuzi haya, lakini aende zaidi aangalie mafuta haya yalikuwa yanachangiaje kwenye maamuzi ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati ya Bajeti nimpongeze kwa pendekezo lao la ukurasa wa 25 alipoitaka Serikali kwamba iwashirikishe kabla haijaenda kwenye *CET - Common External Tariff*, lakini ningependa aongeze hapo kwamba Serikali inapokwenda kwenye *CET* wakati inalenga *East Africa Community* ijue kwamba ina mshirika mwingine anaitwa *SADC*. Sisi tuko *East African Community* lakini tuwe waangalifu tusiwekewe magoli na wenzetu wa *East Africa* katika mchezo ambao sisi tunafaidi kutoka kwenye *SADC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 26 Kamati ya Bajeti imezungumzia suala la udhoofu katika kukusanya mapato ya majengo, kwamba pato katika upande wa majengo ni dhoofu, ningependa kumwuliza au waiulize Serikali kwamba lile pendekezo, ule ushauri Mheshimiwa Rais kwamba watoze kiwango kidogo ili nchi, nyumba zote ziweze kulipa limefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye Kamati yangu, Msajili wa Hazina au Taasisi, Kamati yetu inasimamia mashirika 270. Mashirika haya 270 yana fursa kubwa kwenye uchumi wa Taifa, lakini linaloonekana wazi na kama tulivyoeleza kuna *under capitalization*; mashirika haya hayapewi pesa ya kutosha, lakini yakipewa pesa ya kutosha yatazalisha pato kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri kama tulivyowashauri, huyu ni ng'ombe wa maziwa, tumpe nyasi, tukubali tumpe mashudu, kwetu wanasema *atana gatalonda*, poteza kusudi uje upate. Katika eneo hili la mashirika 270 kuna fursa kubwa ya ajira, lakini kuna upungufu wa weledi katika kufanya shughuli, si suala la vyeti suala la weledi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapeleke kwenye ukurasa wa tisa wale wanaofuatilia kitabu cha *PIC,* ukiangalia makampuni yaliyolipa gawio makampuni 11, kuna kampuni inalipa bilioni tisa, naomba nishauri kwamba hawa ndiyo ng'ombe wa maziwa, kampuni kama *NMB*, lazima itengenezewe mazingira na ituoneshe namna gani italipa zaidi, kampuni kama *PUMA Energy* lazima itengenezewe mazingira kusudi iweze kulipa zaidi, kuna kampuni kama *Cigarette* lazima itengenezewe mazingira na kampuni kama Tanzania *Planting* au *TPC*. Kwa hiyo, kampuni zinazofanya vizuri, lazima tuzifuatilie kusudi tuweze kupata zaidi katika mapato hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wanaofuatilia kitabu chetu niwapeleke ukurasa wa 28, nataka nilizungumzie alilozungumza Makamu Mwenyekiti wa Kamati yangu kuhusu mtazamo mpya wa SUMA JKT. SUMA JKT ni zaidi ya JKT tunayoijua, Taifa sasa linao upungufu wa watu wenye weledi, lakini iko fursa kubwa ndani ya JKT kukusanya vijana waliopewa mafunzo, wakapelekwa JKT wakapewa mafunzo mazuri na wakaweza kufanya vizuri. JKT Kigoma wana mradi wa mawese, wanaweza kupelekwa Kigoma, wakalima mawese na kuweza kuzalisha bidhaa za sabuni na zingine.

Nashauri na Kamati yetu imeshauri kwamba tuliangalie suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, bandari yetu ya Dar es Salam, Bandari ya Dar es Salam nao ni mgodi na kimsingi sisi bandari ya Dar es Salam hatujaitumia kikamilifu. Kamati yetu iliona Bandari ya Dar es Salam ina matatizo makubwa makubwa matatu. Tatizo la kwanza ni la kisheria na kama mnavyojua Waheshimiwa Wabunge, tuliwahi kutunga Sheria, kwa mfano, ile Sheria ya *VAT* iliweza kuiathiri Bandari ya Dar es Salam. Pia sasa kuna ile Sheria ya *axle weight* ambapo mteja wetu namba mbili wa bandari, mteja wa bandari wa nje wa kwanza ni *DRC* Kongo, wa pili ni Zambia, lakini Zambia sasa inajiandaa kususia Bandari ya Dar es Salam kwa sababu ya Sheria ya *axle weight*. Kwa hiyo tunapotunga Sheria, kama nilivyosema mwanzoni tuiangalie *SADC* badala ya kuiangalia Afrika Mashariki tupu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la *TEHAMA*, ukiangalia ule wepesi wa kufanya shughuli *easily of doing business,* eneo ambalo Tanzania tunafanya vibaya sana ni *cross border business*, *cross border business* inaanzia bandarini na tatizo mojawapo ni kwamba mifumo ya bandari ya kuhamisha bidhaa haisomani, *TEHAMA* hazisomani, yule anayetoa mzigo bandarini, anayelipisha anayetunza mzigo, hawasomani. Kwa hiyo ninachotaka kuzungumza ni kwamba tu-*improve* upande huo kusudi bandari yetu tuweze kuifanyia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwekeza kwenye magati, suala lingine ni kuwekeza rasilimali watu, watu wenye weledi na watu wenye motisha. Tukiweza kuwekeza kwenye weledi wa watu wetu tutaweza kuiwezesha bandari yetu. Bandari ya Dar es Salam, ile *geographical location advantage* inaondoka; Beila, mtu ambaye alikuwa na *disadvantage* anatumomonyoa taratibu, lakini watu wengine wana-*opt* kwenda Durban, lakini fursa za nchi tulizonazo, ukiangalia Tanzania inayokuja hali ni nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba kuunga mkono hoja yangu ya *PIC*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwijage. Tunaendelea na Mheshimiwa Bashe, baadaye Mheshimiwa Sandda na Mheshimiwa Peter Msigwa wajiandae.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia. Jambo la kwanza ambalo nataka niseme, Taifa letu kama alivyosema Dkt. Kamala linafanya *radical changes* katika baadhi ya maeneo, lakini *radical changes* zozote ambazo tunazifanya kama Taifa, bila kuwa na *inclusive plan* ya sehemu kubwa ya *population,* hazitoweza kutuletea matokeo mazuri huko mbele tunakokwenda. Tumekuwa na Wizara ya Fedha katika Kamati yetu ya Bajeti na nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Wataalam waliotoka Wizara ya Fedha na naweza nikasema *honestly* kabisa kutoka moyoni *for the first time* nimemwona Mheshimiwa wa Fedha amekuwa *very accommodative* na anafungua milango ya ushauri na hapa ni lazima tuishauri Serikali kwa ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatumia takwimu za *BOT* za mwezi Novemba. Ukiangalia takwimu za Benki Kuu kati ya mwezi wa nane, mpaka mwezi wa 11 *our forex* zimeshuka kwa zaidi ya dola milioni 500, fedha zetu za kigeni zimeshuka kwa kiwango hicho. Pia ukiangalia *pressure* kwenye shilingi yetu, leo dola kwenye soko inakwenda karibu Sh.2400, maana yake *the cost of imports* zinakwenda juu, shilingi inakuwa dhaifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *forex* tunapata kutoka wapi? Ukiangalia mazao yote yanayotuingia fedha za kigeni, *our exports* zimeshuka,. Kwa hiyo, tafsiri yake ni kwamba, fedha za kigeni kuingia kwenye soko letu kuna upungufu na *trend* hii imeendelea kuwepo toka mwaka 2016. Hata hivyo, lakini ukiangalia taarifa ya *TRA* juu ya makusanyo ya kodi waliyoileta kwenye Kamati, malengo ilikuwa ni kwamba ukuaji wa makusanyo ya mapato yalikuwa ni asilimia

18.5, ndiyo yaliyokuwa malengo yetu, kwa miezi sita makusanyo yetu yamekuwa kwa asilimia mbili tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ambalo kwa mtazamo wangu naliona ni *challenge,* mapato ya kodi ya *customs* yamekuwa kwa *negative one percent* maana yake yameshuka kwa asilimia moja, tafsiri yake ni kwamba *component* inayotuingizia asilimia 30 ya mapato, haiendi vizuri. Haya ni *indication*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye *landing,* amesema Dkt, Kamala, *segment* pekee inayokua ya kukopesha katika *commercial banks* ni *personal landing*, mikopo ya wafanyakazi na Waheshimiwa Wabunge tunayokopa ambayo ni *one hundred percent* haiendi kwenye *production*. Ukiangalia *commercial landing* kwenye *Agro sector* imeshuka, ukiangalia *landing* kwenye *manufacturing* imeshuka. Sasa nini ushauri wangu, *radical change* tuliyofanya kama nchi, tumewekeza kwenye *airline,* tunajenga barabara, tunajenga viwanja vya ndege katika hifadhi zetu na *tourist destination*. Ushauri wangu, Wizara ya Fedha, Wizara ya Miundombinu, Wizara ya *Tourism*, kwa sababu *GDP contribution* ya Sekta ya Utalii ni asilimia 17, ni lazima Wizara hizi tatu zikae pamoja zije na mkakati wa *growth*, kwa sababu ukisoma taarifa zote za Wizara ya Fedha hakuna mpango wa kukuza biashara ni mipango ya *administrative* tu *and this is counterproductive.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze ku-*yield* mapato kutokana na kwanza nawashangaa watu wote wanaofikiri kwamba tutapata faida kwenye *ATC*, leo *Airline Business* kwa Afrika inakuwa *projected* itapata hasara ya *three million US* Dola, Sekta ya *Airline*. Kwa nini nchi zinawekeza kwenye *airline*, zinawekeza kwa sababu *it is means to stimulate growth* kwenye sekta zingine. Kwa hiyo ushauri wangu, Wizara ya Fedha na *end of the day* anayeandika *cheque* ya kulipa ndege na kulipa *cost* zote ni Wizara ya Fedha, nimemwambia kwenye Kamati Mheshimiwa Waziri wa Fedha na narudia ndani ya Bunge, *its time* awe kaka mkuu ni lazima tuone *tourism* ina-*grow* kwa zaidi ya asilimia 22 ili iweze kuchangia

kwenye *GDP* ya Taifa letu tuweze kurudisha *investment* tuliyowekeza kwenye ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo ni muhimu sana tuelewe na mimi nataka niwaombe Serikali kwa heshima, Tanzania Kariakoo ilikuwa ni *trading center* ya nchi za *SADC.* Leo tuna *advantage* kubwa sana na nataka niwaombe Serikali, tunapokuwa kwenye hizi Jumuiya *blocks* mfano hii *EAC, the most important question* ya kujiuliza, who *is our cash carry? Cash carry* yetu ni Kenya *the trading partner, cash carry* yetu ni Uganda au ni Rwanda? *Our cash carry* ni Kongo na Zambia. Kwa hiyo *all our economic policies* ni lazima tutazame soko hilo. Tusipofanya namna hiyo hatutoweza kupata *benefit* ya kuwepo kwa eneo la Bandari ya Dar es Salam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo ambalo ni muhimu sana tulitazame, *Eastern part* ya Congo kuna zaidi ya watu milioni 25, *how we are taking advantage of that?* Leo amesema Mheshimiwa Mwijage, tunapitisha hii Sheria mnaita sijui *axle***,** kwamba malori ya uzito, atakayekuwa *disadvantaged* ni sisi kwa sababu *our trading partner* ni Zambia, watahama wataenda Beila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitolee mfano kampuni kama *PUMA. PUMA* Serikali ina-*own fifty percent, PUMA* kwa mwaka 2011 mpaka 2017 wamelipa *dividend* Serikalini *sixty billion shilling.* Naomba msikilize, *PUMA* wamelipa tozo na kodi kwa miaka miwili *for hundred and eighty billion shilling,* halafu huyu anaomba leseni ya *aviation industry* mnamnyima, jamani *what is this?* Yaani *PUMA* ambaye tuna asilimia 50, ametulipa kwa miaka miwili bilioni 480 kodi, anaomba leseni ya *aviation* hapewi, *why?* Nashindwa kuelewa kwamba tunatafakari namna gani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Kariakoo *is dying*...

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu kumpa taarifa ndugu yangu Mheshimiwa Bashe kwamba pamoja na mchango mzuri alioutoa kuhusu *PUMA Energy* ni kwamba kampuni hiyo ya *PUMA Energy* ambayo Serikali ina hisa asilimia 50 imekuwa ikilipa *dividend* tangu mwaka 2009 lakini ndiyo hiyo hiyo Serikali wanajichanganya wanataka kuwanyang'anya leseni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bashe, taarifa hiyo.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea, narekebisha siyo 2011 ni 2009. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachotaka nishauri ni nini? Ni lazima Wizara ya Fedha, *fiscal measures* zinazotengenezwa na Wizara ya Fedha ziwe *production oriented* badala ya kuwa *more control measures.* Mimi ni muumini wa aina moja ya ajabu sana ya falsafa. Naamini kwamba Mchaga wa Kariakoo akikwepa kodi haipeleki Ulaya, hafungui akaunti Uswiss, atakwenda kununua mfuko wa *cement* upata *indirect*. Kwa hiyo, *why are we controlling these small businesses,* tunazi-*suffocate? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo lilinishtua sana na namshukuru Waziri wa Fedha aliahidi kulifanyia kazi. Tulipitisha *measure* hapa ya kuongeza kodi kwenye *crude oil,* tukaongeza *35%* matokeo yake zaidi ya 90% ya mapato katika kipande hicho imeshuka. Tukauliza swali, mbona hamna matatizo ya mafuta nchini? Tukaambiwa wana-*import* zaidi *refined oil.* Tafsiri yake ni nini? Viwanda vya ndani, *re-export component* na taarifa za *BoT* zimeonyesha *re-export* imeshuka. *One the product* ambayo tulikuwa tunafanya *re-export* ilikuwa ni *crude oil* tukiingiza nchini, tukisafisha yakawa *refined* tunayauza Congo na mataifa ya nje. Matokeo yake sasa hivi sisi tunaokaa kwenye *boader* mafuta yanatoka nchi za jirani, *it is counter productive.* Kwa hiyo, ushauri wangu kwa Wizara ya Fedha,

umefika wakati wa ku-*come up* na mpango wa kikodi ambao uta-*stimulate production.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu kilimo. Kilimo kinachangia *almost 30%* ya *GDP* yetu ukiacha *tourism*. Umefika wakati kama nchi ni lazima tuje na mkakati wa ku-*protect agro-sector.* Tusipokuja na mkakati wa kulinda sekta ya kilimo tutarajie maafa huko mbele kwa sababu kilimo kinatuletea mambo mawili; moja *food security* lakini mbili ni *component* inayotuingizia *forex.* Leo tumbaku imeshuka, zao pekee la kilimo linalo-*grow* kwenye *export* ni *cotton* peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa mwisho kwa Serikali, *just a minute,* mazao ya mahindi, karanga na kadhalika yaacheni katika *regional level.* Wizara ya Kilimo ichukue mazao *strategic* kama Korosho, katani, kahawa, tumbaku ili tuwe na *big plan* kwa ajili ya ku-*increase the export* yetu. Bila ya hivyo, *traditional crops* na *non-traditional crops* zinashuka *export* matokeo yake tutapata shida kama nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bashe. Tunaendelea na Mheshimiwa Edwin Sannda baadaye Mheshimiwa Peter Msigwa na Mheshimiwa Othman Omar wajiandae. Mheshimiwa Peter Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nijaribu kutoa maoni yangu kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania siyo kisiwa. Tanzania ni miongoni mwa nchi nyingi zilizoko duniani na kwa kuwa Tanzania siyo kisiwa kwa hiyo ni taifa ambalo tunategemeana na mataifa mengine. Muda siyo mrefu sana na miaka ya nyuma kama Wabunge na kama Kambi ya Upinzani tumetoa ushauri mwingi sana, sana, sana hasa kwa

Mheshimiwa Mpango. Kabla sijaendelea kuchangia nilitaka nipate majibu kwa sehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua Mheshimiwa Mpango, tumekuwa tukiambiwa mara kwa mara kwamba uchumi unakua, ukiangalia *exchange rate* kwa sasa hivi (ukwasi) kati ya Shilingi na Dola, ameondoka Mheshimiwa JK hapa Dola moja tunalipa kwa Sh.1,600 na tukawa tunakusanya shilingi bilioni 800 lakini leo tunaambiwa uchumi umekua makusanyo yako shilingi trilioni 1.3 mpaka 1.4 lakini *exchange rate* kwa mfano jana ilifika mpaka Sh.2,400. Hii inamaanisha nini katika masuala ya uchumi wakati tunambiwa uchumi unakua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye masuala ya mapato, tumeambiwa mapato tunakusanya sana na suala la *GDP* kwamba linaongezeka. Nilitaka nijiulize au tujiulize wote kwa pamoja tunapojadili haya masuala, masuala ya *revenue,* ni kweli hiki tunachokusanya ni *revenue* kwa wafanyabiashara wetu? Vyanzo vya mapato ni vipi ambavyo tunakusanya hii pesa? Au tunakusanya tozo na faini? Kwa sababu kuna uwezekano mkubwa...

**TAARIFA**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Goodluck.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa nataka nimpe taarifa kaka yangu Mheshimiwa Mchungaji Msigwa kuwa masuala ya ukuaji wa uchumi hayahusiani na *exchange rate. Exchange rate* inapanda na kushuka kutokana na *export* na *import* na ajue sisi tunapopambana uchumi wetu ukue na hata Marekani na wenyewe wanapambana na uchumi wao ukue.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Peter Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua Mheshimiwa Waziri haya mapato tunayoyakusanya ni tozo au kweli ni vyanzo vya biashara tulivyonavyo? Kwa sababu takwimu zinazoonyesha kwamba biashara nyingi katika nchi yetu zinafungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi navyozungumza kwa mfano Arusha Mjini kuna watu zaidi ya 650 wanafunga biashara, hawafanyi biashara. Sasa hizi tunazitegemea ni tozo au ni *revenues* na ni *sustainable* kwa siku zinazokuja au tunapiga kelele tu kwamba uchumi unakua? Mnatoza faini nyingi kwa wavuvi halafu tunasema tunakusanya kodi, hivi ni vitu ambavyo siyo *sustainable.* Lazima haya mambo tutafakari kama Wabunge na kama Silinde alivyosema tusiletewe taarifa ambazo ni za kubumba hazitusaidii kama Taifa ili tuweze kulishauri Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni kweli uchumi unakua? Hilo ndiyo suala la kujiuliza. Kwa nini kuna tofauti kati ya *economic growth* na *development growth?* Kwa sababu kama kuna *economic growth* tungeona *development growth* inakuwa *reflected* lakini katika maisha ya watu hatuoni hayo mabadiliko pamoja na pambio na nyimbo nyingi za kwamba uchumi unakua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona vyumba vya madarasa mashuleni hakuna kama uchumi unakua? Sasa hivi tunahangaika kwenye Halmashauri zetu vyumba vya madarasa tunashindwa kupeleka watoto kama huo uchumi unakua kwa nini hatupeleki hizo pesa? Kwa nini huduma za afya zinadidimia kama uchumi unakua? Haya ni mambo ambayo yanatugusa moja kwa moja. Kwa nini matatizo ya maji yameendelea kuwepo kama uchumi unakua? Haya masuala lazima tujiulize kama wawakilishi wa wananchi. Uchumi unakua kwenye makaratasi lakini kwenye mazingira ya uhalisia hauonekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la lingine tunaambiwa kwamba uchumi unakua kama ambavyo nimesema Mheshimiwa Mpango tumemshauri sana miaka

iliyopita, twende kwenye Halmashauri zetu ndugu zangu Wabunge sijui wengine, mimi kwenye Halmashauri yangu ya Iringa pesa inayokuja ni ile ya kusukumasukuma elimu bure lakini pesa zote za maendeleo hazirudi. Mheshimiwa Mpango tulikukataza hapa usichukue mabango tuliyokuwa tunayategemea kwenye Halmashauri, tulikukataza hapa usichukue *property tax,* mlisema hapa kwa mbwembwe nyingi kwamba tunachukua vyanzo vya mapato, *property tax,* mlisema mnachukua mabango, mkasema hiyo hela itakuwa inarudi saa hizi hamjarudisha hiyo hela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TRA* tuliwaambia hapa hata mimi nilisema hawana *capacity* ya kukusanya hizo pesa, hawawezi kukusanya pesa, hela hairudi, mmerudisha mara moja. Haya ni mambo tunatakiwa tujadiliane sasa huo uchumi unakuaje na hiyo hela hamrudishi kule? Utaratibu huu una-*cripple D by D,* Halmashauri zinashindwa kujiendesha halafu tunafichama hapa tunapongezana pongezana kitu gani? Huo uchumi unaokua unakuaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema mwanzoni kwamba sisi siyo kisiwa tunahitajiana duniani. Haya yote tunayapata ni kwa sababu tumeshindwa kuwa na mahusiano ya kimataifa. Haya ni matokeo ya kutokuwa na mahusiano mazuri, *diplomacy* yetu imeporomoka kwa kiwango kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti yetu ya Taifa asilimia 40 tumetegemea wafadhili ambao mara nyingi kwenye chama chenu na kwenye *tv* yenu mmekuwa mkiwabeza, mkiwaita mabeberu lakini asilimia 40 ya bajeti yetu tunategemea mabeberu. Jambo analolifanya Mheshimiwa Rais la kusema tujitegemee ni jambo jema lakini tunajitegemeaje? Tunajitegemeaje wakati muda wote tumekuwa tukiwatukana na kuwakebehi wafadhili.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa ya mwisho hiyo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Msigwa ambaye pia ni mtumishi wa Mungu kwamba Tanzania ina maadili yake. Kwa mfano, mojawapo ya wafadhili wetu wanaweka vikwazo kwamba ni vizuri wanaume wakaoana, wanawake wakaoana na wenzetu hawa wanakwenda huko nje wamesema wanaunga mkono ushoga. Sisi kama Watanzania tumekataa kwa maadili yetu hairuhusiwi na hatutaunga mkono jambo hilo. Sasa wakiamua kutotoa misaada hiyo kwa sababu tumekataa ushoga hivi kuna kosa gani? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Peter Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *donors* wetu ambao toka tumepata uhuru nchi za Ulaya zimetusaidia sana katika maeneo mbalimbali ya elimu, afya ambao kwa sasa hivi wametoa masharti kwamba nchi yetu haina masuala ya kidiplomasia, nchi yetu haina utawala bora na demokrasia katika nchi yetu haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba mnasema sisi tunataka tujitegemee nakubaliana lakini ushahidi kuonyesha kwamba hatuwezi kujitegemea na matusi mnayowapa wafadhili na kila siku Waziri wa Mambo ya Nje hapa akisoma bajeti yake huwa anataja nchi wafadhili, wahisani waliotusaidia katika nchi hii, sipingi kujitegemea lakini namna gani tunahama kutoka kutokujitegemea kwenda kujitegemea. Hawa wahisani ambao wamekuwa wakitusaidia leo tunasema mabeberu lakini demokrasia haifanyiki, nani atakuwa na ujasiri wa kuja kuwekeza katika nchi yetu. Serikali ambayo haiwezi hata kumheshimu Kiongozi wa Kambi ya Upinzani ambaye ana kura milioni sita inamweka ndani kwa ajili ya *bail,* ni mwekezaji gani kutoka nje atakuwa na *confidence* ya kuja kuwekeza katika nchi hii? Anayekuja kuleta mamilioni kama *bail* ya mtu mwenye wafuasi milioni sita anawekwa kienyeji kienyeji ndani?

*Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mnaongea kwa ujasiri hapa, mtuambie ni kwa nini Waziri wa Mambo ya Nje, Profesa Kabudi na Dkt. Slaa walienda kupiga magoti kule nchi za Ulaya kama mnaweza kujitegemea?* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Taarifa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Kwa nini walienda kupiga magoti kuomba wahisani warudi?

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Taarifa.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Kama tunaona tunaweza kujitegemea, tumesema masharti hatuwezi, hawa ni watu ambao tunatakiwa...

**KUHUSU UTARATIBU**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu Utaratibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1)(a) inamtaka Mheshimiwa mchangiaji na Mbunge humu ndani aseme ukweli. Sasa kwa kauli za Mheshimiwa Msigwa kwamba Mheshimiwa Profesa Kabudi alienda kupiga magoti Ulaya, naomba nipate mwongozo wako athibitishe au afute hiyo kauli kwa sababu hana ushahidi wa kutosha kama alienda kupiga magoti.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako juu ya jambo hili kama inaruhusiwa kusema uongo Bungeni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Peter Msigwa haifai kusema uongo ndani ya Bunge kwa hiyo unapozungumza, zungumza kauli zenye ukweli.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisema nasema uongo unanionea. Vyombo vya habari vimesema na hawajakanusha na kanuni zinataka kwanza yeye aseme kama mimi nasema uongo. Yeye athibitishe kama mimi nasema uongo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Peter Msigwa usiende na vyombo vya habari.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Ninachosema…

**MWENYEKITI:** Ndiyo.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachosema, uchumi wa nchi hii tutaimba pambio hapa, tutapongezana, *TBC* itawasifu sana, lakini duniani kote nimesema Tanzania siyo kisiwa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Kuhusu Utaratibu.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Ili uchumi wetu uweze kukua…

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Kuhusu utaratibu.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: …**tuimarishe demokrasia, na utawala bora…

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Tusikilizane jamani, tafadhali. Mmoja mmoja siyo tunazungumza kama tuko sokoni watu wote.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara kuhusu utaratibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma Kanuni ya 64(1)(a). Mheshimiwa Msigwa amesema humu kwamba Profesa Kabudi amepiga magoti Ulaya kuomba misaada. Mimi nachosema ni kwamba hakupiga magoti kuomba misaada Ulaya. Sasa kwa sababu amesema uongo ni aidha afute kauli au athibitishe kauli hiyo.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Peter Msigwa kwa vile huna ushahidi na hilo naomba ufute kauli yako.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Dkt. Kabudi, Dkt. Slaa na Mheshimiwa Mahiga walisimama walipokwenda Ulaya kuomba misaada, hawakupiga magoti. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kusema...

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Peter Msigwa...

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Naomba utulivu jamani.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Peter Msigwa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo kauli yako ya mwanzo umefuta? Haya sema nimefuta kauli yangu ile ya kupiga magoti.

**MBUNGE FULANI:** Afute kauli yake.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Hiyo ya mwanzo nimefuta, imebaki ile ya kusimama. *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mpango, Mheshimiwa Silinde hapa amezungumza hapa kwamba atayekuwa wa kwanza kwenda gerezani ni Katibu wa Hazina, lakini hata wewe Mheshimiwa Mpango hakitakukosa kikombe hiki kwa sababu mambo mnayoyafanya nje ya utaratibu katika Serikali hii yamekithiri kuliko kawaida na jinai huwa haifi. Msishangilie tu mambo haya kama hatuwezi kufuata utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe hii bajeti mnayohangaika na kusema haiendi vizuri, naomba nikuulize Mheshimiwa Mpango, kama wafadhili wanatoa hiyo asilimia 40 wanaotuletea pesa mnawaita mabeberu na huko barabarani ukipita unaona barabara kwa hisani ya watu wa Marekani, ukikuta daraja kwa hisani ya watu wa Marekani, UKIMWI kwa hisani ya watu wa Marekani, *condom* hisani ya watu wa Marekani, malaria hisani ya watu wa Marekani, mama na mtoto hisani ya watu wa Marekani, kama wafadhili wakiondoa asilimia 40 kwa moyo mweupe kabisa, hiyo asilimia 40 kwa mpango wenu wa Serikali mnaitoa wapi ili tuweze kujitegemea? Kweli tujitegemee hamna mtu

anayekataa lakini mnajitegemea, mnaondoka kwa mbwembwe na matusi wakati uwezo huo wa kupata asilimia 40 hatuna. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Peter Msigwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Othman Omar kwa dakika nane.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Halafu Msigwa umevaa suruali ya *pink* kwa Marekani ni ishara ya mambo yetu yale.

**MBUNGE FULANI:** Angalia wewe ulivyovaa hiyo gauni yako.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, zimeni *microphone* zenu. Mheshimiwa Othman dakika nane.

**MHE. OTHMAN OMAR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme tu kwamba ni Mjumbe wa Kamati ya Uwekezaji, kwa hiyo, mchango wangu utajikita zaidi kwenye eneo hilo la uwekezaji.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1), kauli ambazo siyo za Kibunge haziruhusiwi katika Bunge hili. Mheshimiwa Msongozi amesema washenzi sisi ambao tunamuunga mkono Mheshimiwa Mchungaji Msigwa. Naomba umtake afute hiyo kauli yake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline kama umesema hivyo naomba ufute kauli yako.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Hansard* ipo, iletwe *Hansard* tuone kama nimetaka neno mshenzi hapa. Kwa nini *Chief Whip* wa upande wa Upinzani anasema uongo Bungeni?

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mimi sijasema neno hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Chief Whip,* kwa vile hilo jambo sijalisikia kwa masikio yangu naomba...

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Selasini ni Mheshimiwa Maryam huyo.

**MWENYEKITI:** ...turudi kwenye *Hansard* kama atakuwa amezungumza hivyo atafuta kauli yake.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Nitoe ushahidi.

**MBUNGE FULANI:** Hilo neno hajaongelea kwenye *microphone*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline aliwasha *microphone,* kwa hiyo tutasikia alichokizungumza, Mheshimiwa Othman naomba uendelee.

**MHE. OTHMAN OMAR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika zangu uzitunze. Ni Mjumbe wa Kamati ya Uwekezaji *(PIC)* na ninapenda mchango wangu uelekee huko kwanza. Kama tunavyofahamu kwamba lengo kubwa la mashirika ya umma haya ni kukuza mtaji ni kukuza ajira, kupunguza umasikini na kukuza uchumi wa Taifa. Tulitegemea kwamba kwamba mashirika haya yale ambayo siyo ya Muungano, mambo haya ya fursa hizi za ajira hupunguza umaskini utaenea kwa Tanzania nzima. Lakini bahati mbaya

kwa masikitiko taasisi nyingi za Muungano ambazo tunategemea kueneza ajira hizi Tanzania nzima zimejikita kwenye upande mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natolea mfano, tuna taasisi ya Kituo cha Mikutano ya Kimataifa *(AICC)* kituo hiki kiliazishwa mwaka 1977 mpaka leo tunavyosema kituo hiki kina umri wa miaka 42, kituo hiki dhamira yake ni utalii wa mikutano ya kimataifa. Rasilimali kubwa za kituo hiki ziko upande mmoja wa Muungano, ajira kwa upande mkubwa unatoka upande mmoja wa Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile fursa au tunasema fursa za tunaweza tukasema huduma za kijamii zinazotolewa na kituo hiki zinatoka upande mmoja wa Muungano. Sasa tulitegemea kwamba kituo hiki kwa sababu shughuli yake kubwa ni mikutano ya kimataifa na kwa sababu kule Zanzibar kuna fursa nyingi, kuna maeneo mazuri, kuna mazingira mazuri ya kuweka uwekezaji, nilitegemea kwamba kituo hiki cha kimataifa kitatoa *branch* yake kule ili na wale wa upande wa Zanzibar wapate fursa nao za kupata ajira, kupunguza umaskini na kukuza uchumi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bahati mbaya tukihoji hapa kwa nini fursa kama hizi hazipelekwi, kwa nini hatutajengewa hili jengo la mikutano angalau ya kimataifa Serikali inasema kwamba mata tunakuja kujenga Dodoma, mara tunajenga Mwanza mara Mtwara sasa tunauliza kujengwa kituo hiki Dodoma kama siyo Zanzibar kitatusaidia kitu gani? Tunaomba sana Serikali huduma hizi za mashirika ya Muungano yapendelee pia kwenda kule Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye Bodi ya Wakurugenzi, nipo katika Kamati kwa muda wa miaka mitatu sasa nikiangalia Bodi za Wakurugenzi kwa kiasi kikubwa bodi zinazokuja katika Kamati hatuoni kwamba inawakilisha Muungano. Wajumbe wote wa Kamati wanakuwa upande mmoja wa Muungano, sasa tulitaka na wale wajumbe kutoka Zanzibar ambao wamo katika bodi ya Muungano wawe pia katika Kamati wanapoitwa na Kamati ya Uwekezaji ili waje

washuhudie yale mambo ambayo yanaelezwa na wenzi wao kutoka huku Tanzania Bara, je, ni sahihi au siyo sahihi? Ili na sisi tupate kuwahoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoka hapa nakwenda kwenye masuala ya *TBS* (Mamlaka ya Viwango), kazi ya shirika hili ni kukuza uchumi kupitia kulinda usalama wa Tanzania kwa kuhakikisha kwamba wanatumia chakula ambacho kiko salama. Lakini tatizo linalowakabili Shirika hili la *TBS* ni kwamba lina upungufu wa wafanyakazi, mpaka kufikia mwezi Novemba, 2018 shirika hili lilikuwa na wafanyakazi 456, shirika hili linahitaji wafanyakazi takribani 750 ukiangalia kazi ya shirika hili ukubwa wa eneo la Tanzania mahitaji wanayostahiki kuhudumiwa watanzania ni kwamba kiwango hiki cha wafanyakazi ni kidogo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. OTHMAN OMAR HAJI:** ... vijana tunao wengi wanaomaliza kwa hivyo wapewe fursa za ajira kwenye shughuli ili hili shirika liweze kufanya kazi yake kiufanisi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Othman. Tunaendelea na Mheshimiwa Mbogo atafuata na Mheshimiwa Marwa Ryoba.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi, kwanza naomba nipongeze Wajumbe wenzangu wa Kamati ya *PIC* kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ya kuweza kuishauri Serikali katika utendaji kiujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na jambo la kwanza ya masuala machache ambayo yamejitokeza hapa ndani; kwanza kuna mchangiaji mmoja ameeleza hajui tofauti ya *revenue* na tozo, lakini naomba tutambue kwamba tuna mapato ya aina mbili katika bajeti yetu ya Serikali. Tuna

mapato yanayotokana na kodi na tuna mapato ambayo hayatokani na kodi. Kwa hiyo, unavyotuambui *revenue* na utambui tozo nazo ni *revenue* ni mapato kwa hiyo tusiwe tunachanganya kidogo masuala haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine limejitokeza suala la kwamba faida kutoka Serikali inayopata katika uwekezaji kwenye taasisi na baadhi ya mashirika ya umma imepungua kutoka bilioni 800 na ushehe mpaka bilioni 600. Serikali katika hizi taasisi na mashirika ya umma ambapo imewekeza inapata aina mbili za mapato; kuna mapato ghafi ambayo ni 15% kutoka kwenye mauzo na pia kuna mapato yanayotokana na gawio baada gawio la kwenye faida yaani *dividend. (Makofi)*

Sasa baada ya kutoa haya unakuta bado kuna masalia ya ziada yamebaki, kwa hiyo kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti ambayo ni 70% inachukuliwa na Hazina na 30% inabaki inaendelea kwa ajili ya kuendelea hayo mashirika kufanya uwekezaji. kwa hiyo kushuka kutoka bilioni 800 mpaka bilioni 600 ilitokana na kwamba kulikuwa na malimbikizo ya miaka ya nyuma kulikuwa na *cummulative figure retained earnings* ndiyo ambayo ilichukuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo alilisemea rafiki yangu Mheshimiwa Silinde ni kuhusiana na miradi ya maji. Mwaka jana tumepitisha bajeti ya maji takribani bilioni 673 ambayo ni ya miradi ya maendeleo katika hizi bilioni 673; shilingi bilioni 443 zinatokana na mapato ya ndani na zinazobaki zinatokana na mikopo pamoja na ruzuku za wafadhili mbalimbali yaani fedha za nje.

Sasa kwenye hizo shilingi bilioni 443 hapo ndani pia tuna mfuko wa maji ambapo una bilioni 158 na siyo ile bilioni 249 aliyoisema na katika hiyo bilioni 158 Serikali imeshatoa bilioni 67 ambayo ni sawasawa na 43% ambayo imeshapatikana. Na wengi katika Halmashauri zetu tunajua kabisa miradi ya maji inatekelezwa na Halmashauri zinatuma *certificate* Wizarani ikishatuma *certificate* Wizarani ndipo Serikali inapeleka pesa na hatua hii ilichukuliwa kwa sababu

fedha zilikuwa zinaliwa na miradi haitekelezwi kwa wakati, ndiyo maana Serikali ilibadilisha utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine ambalo limeweza kuzungumziwa ni kuhusiana na masuala ya madeni. Ndugu zangu tunajua taasisi ya kufanya kazi kuna madeni na sisi kwenye Kamati yetu tumekuwa tukisisitiza sana ulipaji wa madeni na pia katika kuongeza mitaji baadhi ya taasisi na mojawapo ambapo tunaiona katika ulipaji wa madeni yasipolipwa kwa wakati kulingana na kanuni za kiuhasibu zinavyohitaji lazima ufanye *provision for doubtful debts* yaani unafanya *in payment* ya *receivable* kwamba endapo isipokusanywa tutakuwa na gharama ya hasara kiasi gani, kwa hiyo, tumekuwa tukisisitiza kwenye jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia hapo naomba nirudi kwenye usimamizi Ofisi ya *Treasury Register (TR).* Serikali kama tulivyosema awali kuna mapato yanayotokana na kodi na mapato ambayo hayatokani na kodi katika moja ya mapato ambayo hayatokani na kodi ni kutoka Ofisi ya *TR.* Sasa ili aweze tuweze kuongeza mapato ambayo hayatokani na kodi maana yake tukaboreshe usimamizi wa hiyo Ofisi ya *TR* na katika kuboresha ofisi hii kimsingi haya makampuni/taasisi zote ziko nchi nzima na watumishi wako kwenye kama 105 maana yake ni kada mbalimbali wa chini mpaka wa juu. Sasa niombe Serikali ikaweze kumwezesha *TR* kibajeti ili akawekeze kwenye TEHAMA na kwamba kila mwezi mashirika yote haya *report* zao za mahesabu za kila mwezi wanaziingiza katika mfumo ambapo mtu amekaa ofisini kwake kama ni Mwanza kama ni Mbeya anaingizwa kwenye mfumo ofisi ya *TR* kutokea Dodoma Makao hapa wana *monitor*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *reporting system* inaitwa *work based reporting* kwa hiyo inatumika ile na mna-*control* mashirika yetu na makampuni ya nje yana-*control* dunia nzima kwa kupitia mfumo na hii itamsaidia *TR*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sisi kama Kamati ya *PIC* ili tuweze tukasimamie vizuri haya mashirika tunahitaji kufanya

kazi kwa ukaribu vizuri kabisa na Ofisi ya *TR.* Sasa ni vyema tukaboresha namna ya kiutawala Ofisi ya *TR* kuwasiliana na Bunge, *TR* awasiliane moja kwa moja na Bunge maana mlolongo wa kupitia kwa Katibu Mkuu halafu ndiyo ije kwa Mheshimiwa Waziri halafu ndiyo ije sasa Ofisi ya Bunge tumekuwa na mawasiliano yanachelewa na maamuzi pengine yanachelewa. Wajumbe wanahitaji kuchangia uwezo semina hazifanyiki, Wajumbe wanahitaji kwenye kukagua miradi tumealikwa hatujaenda kwa sababu ya mawasiliano. Kwa hiyo, tunaomba *TR* apewe madaraka ya moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ili tuweze kuongeza ufanisi katika taasisi na mashirika yote haya tunahitaji *TR* akazingatie sheria; 60% ya gharama ikaende kuzingatiwa na kuweza kusimamia na tukifanya hivyo tutaondoa uwalakini wa mashirika ambayo yatakuwa yanafanya biashara au kazi kwa hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kamati yetu tumesisitiza uongezaji wa mitaji na tunapongeza sana Serikali kwa kufufua Shirika la *Air Tanzania*. Nina imani kabisa miaka mitanomitatu ijayo au minne *Air Tanzania* itaanza kufanya kazi kwa faida kwa sababu uwekezaji huu ambao umefanywa na Serikali tutaenda kuongeza biashara, abiria wengi watabebwa na ndipo ambapo gharama zitaenda zinashuka ukilinganisha na mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na pia kama wachangiaji wengine walivyosema kwamba kwa kufufua *Air* Tanzania tutaenda na kuboresha sekta zingine ambazo ni sekta kubwa sana ya utalii, tutaenda kuongeza ajira na maeneo mengine ya Tanzania yatafikika. Kwa mfano Mkoa wetu wa Katavi tuna Mbuga ya Katavi ambayo ni nzuri sana na wanyama wakubwa wazuri sana, lakini ni kwamba *Air Tanzania* ikifika kule na uwanja wa ndege upo tutaongeza watalii wakuja kutalii kwenye nchi yetu na mapato ya Serikali yataongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile shirika letu la *Air Tanzania* hebu kwenye kulinyanyua tulipe *discount* kwenye baadhi ya *charge* Serikali kwa mfano *charge* za *airport*, *landing fee*, kwenye *charge* cha *TCIAA* tuwape *discount*. Na pia *TTCL* wanahitaji mtaji wa dola kama 230,000 kama mchango wa Serikali ili iweze kushindana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbogo tunaendelea na Mheshimiwa Marwa Ryoba.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana na kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama nikiwa upande huu wa pili, naomba nichukue nafasi hii kumshuruku Mungu kwa neema aliyonipa kuwa upande huu. Ni bahati sana unajua kuwa Mbunge wa pande zote wakati kama huu nimekuwa upande wa kule ng'ambo na leo niko hapa, *I can taste the difference*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu nimejifunza na nitaomba nikiseme, kazi ya Bunge au kazi ya Mbunge ni kuikosoa, kuishauri na kuisimamia Serikali. Lakini nimegundua kumbe kipindi nikiwa ng'ambo ile nilikuwa nakosoa tu nilikuwa sishauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitakosoa, nitashauri na naomba nianze kwa kunukuu maneno aliyoyasema Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mwaka 1969 alisema hivi; "Taifa lisilokubali kutaabika kwa maendeleo yake lenyewe, bila shaka Taifa hilo litataabika kwa maendeleo ya mataifa mengine, anasema maendeleo ni mtoto wa taabu." *(Makofi)*

Naomba nirudie hawajasikia vizuri; "Taifa lisilokubali kutaabika kwa maendeleo yake lenyewe, bila shaka Taifa hilo litataabika kwa maendeleo ya mataifa mengine, maendeleo ni mtoto wa taabu." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuendelea kwa kutegemea *donors,* kama ingelikuwa mataifa yanaendelea kwa kutegemea *donors* tungeona kwa China, tungeona kwa Amerika na mataifa mengine. Lakini ni mataifa ambayo yaliamua kutumia rasilimali zao wenyewe na leo wako hapo walipo wanasaidia watu wengine na nampenda sana Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli yeye hataki tujiite sisi maskini na kweli sisi siyo masikini, Tanzania siyo masikini. *(Makofi/ Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kuna maeneo naomba nishauri eneo la kwanza...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MBUNGE FULANI:** Tulia wewe.

**MWENYEKITI:** haya taarifa ya kwanza hiyo.

**TAARIFA**

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa tu Mheshimiwa Marwa yeye mwenyewe baada ya kuona kwamba amechoka kabisa ilibidi ajisalimishe kwa *donors.* Kwa hiyo, asiseme kwamba tunavyozungumza tunavyoishauri Serikali kwamba ijitahidi kuwasiliana na kukaa na *donors* tunakosea yeye mwenyewe ni mfano.*(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakajoka kwa ma-*donors* wa nje wa ndani? Mheshimiwa Ryoba Chacha.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee.

**MBUNGE FULANI:** Endelea leta maneno.

**MWENYEKITI:** Basi nilishaelewa.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa leo niongelee mwenendo wa thamani ya shilingi. Ukiangalia kwa mujibu wa taarifa ya Kamati ambayo mimi pia ni Mjumbe wa Kamati thamani ya shilingi inashuka na kuna mapendekezo yametolewa nini kifanyike ili ku-*stabilize* shilingi yetu. Sasa kama nilivyosema leo nitakosoa kwamba ni kweli tumeendelea kushuka shilingi yetu imeendelea kushuka, lakini nini kifanyike ili shilingi yetu iendelee kuwa *stable*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza, lazima tukubali kama Bunge kuisimamia Serikali ipeleke fedha za kutosha kwenye kilimo. Kwenye kilimo wenzangu wameshauri kwenye yale mazao ya kimkakati kwa mfano tumbaku, korosho na mazao mengine ambayo yanatuingizia fedha za kigeni lazima tuhakikishe tunawekeza huko, sasa huo ndio ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili, nina kiatu hapa, hebu kiangalie vizuri kwanza, hiki hapo, kiangalie vizuri hicho kiatu, hiki kiatu ukikiangalia utadhani kimetoka Ulaya, kinatengenezwa hapa Dodoma.

**MBUNGE FULANI:** Nyoosha juu tukione. *(Makofi)*

**MHE. MARWA R. CHACHA:** ...hapa Dodoma, hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tu-*discourage importation* ya vitu tunavyoweza kuvitengeneza wenyewe. Leo tuna ng'ombe kila kona, tuna ngozi ya kutosha, lazima Serikali ichukue hatua ikiwezekana ya kuondoa kodi kabisa kwenye mashine za uchakataji wa ngozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda kwa huyu mtu ambaye anatengeneza hivi viatu, yuko hapo karibu na Chuo cha Mipango, ni mjasiriamali mdogo tu, lakini unaweza ukaangalia ukadhani kimetoka Ulaya. Sasa tutawawezeshe tuwasaidie watu wetu wazalishe vitu vyetu, soko la ndani ni kubwa. Badala ya kuagiza nje tuzalishe vya kutosha na tuuze nje shilingi yetu itakuwa imara kwelikweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ushauri mwingine ni kwenye mafuta. Tupige kodi kubwa kwenye mafuta ya kutoka nje ili watu wetu walime alizeti, walime michikichi, tuzalishe mafuta yetu wenyewe. Haiwezekani shilingi yetu ikawa *stable* kama mafuta tunatoa nje, haiwezekani. Hivi ni kweli tumeshindwa kulima alizeti? Tumeshindwa kuzalisha mafuta ya alizeti? Haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima tuchukue mkakati wa makusudi na mimi namshukuru sana Rais John Pombe Magufuli, alisema kama hamlimi sitoi chakula, umesikia watu wanalia njaa saa hizi? Wamenyooka, watu wanalima, watu wanalima, hakuna cha dezo kila mtu afanye kazi fursa zipo. Kwa hiyo lazima tukubali kuzalisha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine, tuwasaidie wachimbaji wadogowadogo wa madini. Nichukue hatua hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Madini, Mheshimiwa Doto Biteko ameanza vizuri. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kukubali kukaa na wachimbaji wadogo wadogo na wachimbaji wakubwa, ni hatua nzuri, tumuunge mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuwasaidie wakandarasi wa ndani kwa sababu hapa ndipo pia tunalipa fedha nyingi za kigeni kwenda nje. Leo tungekuwa tumewezesha watu wetu wakandarasi wa ndani kufanya miradi yetu fedha zinabaki humu ndani, zinazunguka humuhumu. Kwa hiyo, tuendelee kuwawezesha wakandarasi wa ndani. Nimshukuru pia Mheshimiwa Rais Magufuli kwa sababu ndiye mwanzilishi wa kusaidia wale wakandarasi wa ndani waliojenga Daraja la Mbutu kule Igunga, na sasa hivi wako kule wanatengeneza barabara, wanaenda vizuri na wametengeneza Daraja la Mto Mara ambalo liko mpakani kati ya Jimbo la Serengeti na Jimbo la Tarime na Mheshimiwa Heche anafahamu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Chacha.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia, naomba nimalizie. Nilikuwa naomba nishauri kwenye eneo lingine ni *TARURA,* tumeunda chombo hiki *TARURA* ili kusaidia barabara za vijijini, tunaomba Serikali ilete chanzo kingine cha kui-*finance TARURA* ili ifanye kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda nashukuru, lakini niseme nilimsikia mtu mmoja anasemasema pale ni Mchungaji, sijui mchungaji? *Are you a Pastor or Poster?*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Chacha, tunaendelea na Mheshimiwa Mashimba.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Peter kwani kakutaja wewe?

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo.

**MWEYEKITI:** Mwongozo wa nini tena?

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unisikilize. Naomba unisikilize.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Peter.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia kuna Mheshimiwa Jacqueline hapa alinitolea lugha ya kashfa, kwamba mimi nimevaa nguo ya *pink* kwa kuwa, hii nguo ya *pink* kule Marekani wanaovaa nguo hizi ni watu wanaofanya mambo ya ushoga.

Sasa nilitaka Mwongozo wako, mimi hapa nimekuja kama Mbunge, ninayo haki ya kuzungumza, tabia zetu za Tanzania ni tofauti na Marekani, niliomba kama aliyoyazungumza ukilinganisha na Mwongozo aliouomba Mheshimiwa Selasini kama ndio lugha za Kibunge au yanakubalika...

**MBUNGE FULANI:** Tukapime.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** ...ndani ya Bunge. Vinginevyo kama hatathibitisha ningeomba Kiti chako kiniongoze, vinginevyo apelekwe kwenye Kamati ya Maadili kwa sababu ananivunjia heshima bila kosa lolote nililolifanya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Peter, Mheshimiwa Jacqueline alipokuwa anazungumza hayo alikuwa amekusudia hivyo unavyosema wewe?

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio aliwasha *microphone.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline naomba u-*clarify* Mheshimiwa Jacqueline.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nakushukuru sana. Mimi sijatamka neno ushoga, nashangaa na *Hansard* ipo, sijatamka neno ushoga asiniwekee maneno mdomoni, *Hansard* ipo. Chukua *Hansard* halafu ndio baadae utatoa maamuzi, mimi sijatamka neno ushoga.

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante Mheshimiwa Jacqueline umeeleweka. Kama ambavyo nimezungumza kwa Mheshimiwa Selasini, basi tutarudi kwenye *Hansard* tuangalie kama ni kweli.

Tunaendelea Waheshimiwa, Mheshimiwa Mashimba Ndaki. Baadae Mheshimiwa Hasna Mwilima na Mheshimiwa Balozi Adadi wajiandae.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mimi labda nianze kwa kusema machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, sisi kama nchi lazima tufikirie kujitegemea zaidi hapa ndani kwetu kuliko kutegemea watu wengine. Wakati wa kuanza kufikiria kujitegemea ni wakati huu. Sasa kama fikra zetu bado zitaendelea kudhani kwamba kuna mtu atatusaidia ili kama nchi tuweze kusonga mbele kimaendeleo mawazo hayo hayapo kwa ulimwengu wa sasa. Kwa sababu hata waliokuwa wakitusaidia na kutuonea huruma zamani mazingira yao yamebadilika sana. Yamebadilika kwa kiasi kikubwa na wao wakati huu wanaanza kufikiria nani atawasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu kwamba lazima tuanze kuwaza kujitegemea wenyewe badala ya kufikiria kwamba kuna mtu atatusaidia kututoa hapa tulipo. Ukisikiliza mazungumzo yanayosemwa bado tunafikiri sana kwamba labda tuko miaka ya 1970, miaka ya 1980, wakati ambapo tulikuwa tunalelewa tu mpaka asilimia 60 ya bajeti zetu zilikuwa zinategemea misaada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakumbuka wakati Mzee Mwinyi anachukua madaraka nchi ilikuwa kwenye hali isiyo nzuri, mbaya. Mzee Mwinyi alitoa hotuba wakati fulani akasema, baada ya kupata urais nimekuta kwenye chungu cha Hazina hakuna kitu. Sasa nimejaribu kutembea Ujerumani, Marekani na nchi mbalimbali kote huko wananiambia nenda kakubaliane na *IMF* au *World Bank.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unaweza kuona ni kwa namna gani ikiwa unataka kusaidiwa kila wakati masharti utakayoongezewa, utakayopewa ili uyatimize kupata huo msaada ni masharti ya namna gani. Sasa katika dunia ya leo masharti yameongezeka zaidi, zaidi ya kukubaliana na *World Bank,* zaidi ya kukubaliana na *IMF,* kuna masharti mengine ambayo hayaruhusu kabisa tabia, mienendo na

tamaduni za Kitanzania. Sasa tukiendelea kufikiria kwamba lazima tu tusaidiwe ili tutoke hapa tulipo basi mimi nachelea kusema inawezekana tukaamua kuuza uhuru wetu, uhuru unaotunza utamaduni wetu, uhuru unaotunza mienendo na desturi na mila zetu, tukauza ili tupate hiyo misaada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, misaada tunaihitaji, lakini iwe katika misingi ile inayokubalika katika utamaduni na mila zetu, ndiyo maana hata kwenye kipindi tunachokijadili, kwenye taarifa hii, bado kuna misaada tuliyopata kutoka kwa wasamaria wema, misaada ambayo haikuambatana na masharti ambayo ni hasi kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ukurasa wa 29 wa taarifa ya Kamati ya Bajeti tulitarajia tungeweza kupata misaada ya trilioni 2.6, lakini tulipata bilioni 878. Mimi niseme kama tulipata misaada ya namna hii basi ndiyo misaada iliyokuwa haina masharti ya kutufanya tuuze uhuru wetu, tulipata, si kwamba hatukupata kabisa kama wenzetu wanavyoweza kusema. Misaada tunapata, lakini ni ile ambayo wanakubaliana na masharti yetu sisi pia, sio tu tuuze kila kitu, tukubali kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu habari ya mikopo hiyo kila mtu anakopa. Mtu binafsi anakopa, nchi inakopa na unakopa kwa kulinganisha na hali yako ya kulipa. Sasa ukiona hali yako ya kulipa haiendi sawasawa basi unakwepa huo mkopo kwa hiyo, kama nchi kwa kweli, lazima tufikirie kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niseme tu kwamba ninamuunga mkono sana Mheshimiwa Rais anaposema tujitegemee, lazima Watanzania tuamue kujitegemea. Anasema tutaumia kidogo, lakini tutakwenda. Kwa hiyo, ni lazima tukubali na sisi ndani ya Bunge lako ndio watu wanao...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa…

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunaendelea na Mheshimiwa Hasna Mwilima, baadae Mheshimiwa Balozi Adadi na Mheshimiwa Sonia Magogo ajiandae.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kwa kupata nafasi ya kuchangia kamati hizi mbili, hasa Kamati yangu ya Bajeti kwa sababu mimi ni Mjumbe kwenye hiyo kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia, leo asubuhi nilimsikia mdogo wangu Mheshimiwa Ester Bulaya anasema tuongee kama Taifa tusiongee kama Wabunge wa vyama tofauti, lakini Mchungaji Msigwa hapa ametuambia kama tunawatukana *donors* tutapataje ile asilimia 40 kuiingiza kwenye bajeti yetu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi napata mashaka kidogo. Juzi tukiwa kwenye kamati Mheshimiwa Waziri wa Fedha alituambia kwamba Serikali ya Ubelgiji imesema haiwezi kutupa misaada kwa ajili hatuungi mkono masuala ya ushoga.

Sasa najiuliza maswali kama tunazungumza kama Taifa, yeye leo ameambiwa na Mheshimiwa Jacqueline hapa kuhusiana na suruali, ameomba Mwongozo, ina maana hapendezwi na hayo masuala. Tunawezaje kukubaliana na *donors* ambao wanataka vizazi vyetu ambavyo tumevizaa huko baadaye vije kuwa ni vizazi vya asilimia 80 vya ushoga, haiwezekani. *(Makofi)*

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa ya kwanza.

**TAARIFA**

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna upotoshaji mkubwa sana unaendelea katika mjadala humu ndani ya Bunge. Barua ya *EU* na Amerika, mambo waliyoyataja kwa nini yamekuwa ni kikwazo kuisadia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni pamoja na utawala bora, uminywaji wa demokrasia na mambo ya vyombo vya habari.

*Hili la LGBT wala halikuwepo, hili limeletwa na Makonda na lilipoletwa na Makonda, Mheshimiwa Kangi akawahakikishia mashoga usalama. Kwa hiyo kimsingi wanaowahakikishia mashoga usalama ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Kangi alisema Bungeni...***[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hayo siyakubali aah, Chama cha Mapinduzi ama Serikali haijakubali mambo ya ushoga, hilo naliondoa kabisa. Mheshimiwa nani...

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pilipili usiyoila inakuwashaje?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu Utaratibu, Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro.

**KUHUSU UTARATIBU**

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1)(a). Mheshimiwa Lema ametoka kuongea sasa anasema waraka uliotolewa na Bunge la Ulaya hawajaongea kuhusiana na ushoga. Taarifa hiyo ni ya uongo, waraka ule wenye *page* 15 umeongelea ushoga, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndumbaro kuhusu huo utaratibu nilishasema kwamba yale ambayo ameyazungumza Mheshimiwa Lema nimeyaondoa, hayatakiwi yote.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lema ni mdogo wangu, lakini kama pilipili usiyoila huwezi kujua muwasho wake ukoje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme hivi, kwamba sisi kama Serikali ya Chama cha Mapinduzi tunatekeleza miradi mbalimbali kwa pesa zetu za ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hii imejionesha. Leo kuna mtu alisema kwamba, huwezi kuweka tozo kwamba ni sehemu ya *revenue,* lakini kwenye taarifa ya *REA,* kwenye taarifa ya maji, waliyoleta Waheshimiwa Naibu Mawaziri wameonesha ni jinsi gani Wizara ya Fedha imepeleka tozo zote zilizotolewa na miradi imetekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hiyo bilioni *67 point something* iliyopelekwa kwenye miradi ya maji imetokana na nini? Imetokana na *revenue* ya tozo ya lita ya mafuta shilingi 50, petroli na dizeli. Kwa hiyo, pesa zetu za ndani zinatusukuma na miradi, lakini wale wafadhili ambao wanaona hawataki kutuletea masharti yasiyokuwa na msingi na taifa letu wanaendelea kuisaidia Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo tuache upotoshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijikite kwenye taarifa yetu ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba tuna ile miradi ya mkakati, naomba unilindie muda wangu maana Mheshimiwa Lema aliniharibia muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua tuna ule mkakati wa miradi ya kimkakati kama vile *SGR* pamoja na mradi wa Mchuchuma na Liganga. Niishauri Serikali, hebu iangalie hii

miradi kwa sababu, deni letu la Taifa ni himilivu tuone ni jinsi gani tunaweza tukakopa tukaangalia miradi mikubwa miwili kama *SGR,* Liganga na Mchuchuma, ili tuwe na uhakika wa kuongeza kipato katika makusanyo yetu ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivi kwa sababu Mradi wa *SGR* tumeuanza kwa pesa zetu za ndani, lakini tuangalie matawi ambayo yana umuhimu zaidi kiuchumi kuliko kuangalia tawi linalokwenda Isaka mpaka Mwanza huku tunaacha kutoka Tabora kwenda Kigoma kama alivyosema mdogo wangu Mheshimiwa Bashe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tuangalie vilevile njia ya kutoka Isaka kuelekea Kigali, ili tuweze kupata mapato zaidi na hatimaye Taifa letu litekeleze miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwe mkweli, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Mheshimiwa Rais ana miaka mitatu, leo ameingiza ndege sita, tunakosa kumpongeza! Hizi ndege, tunayo *Dreamliner* moja, *Airbus* mbili, tukitoa *direct flight*, *Dar es Salaam to Guangzhou, Dar es Salaam to New Delhi,* hatuwezi kuingiza mapato? Watalii watakuja *direct* kwa kutumia *ATCL.* Sasa tusikashifu hapa *as if* kwamba hizi ndege zilizonunuliwa hazina thamani yoyote ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana tuache upotoshaji, Serikali inafanya kazi. Mheshimiwa Rais ameshasema, hata wewe nyumbani kwako ukitaka ukiwa na maisha mazuri, lazima ujibane. Tutaendelea kujibana ili Taifa lisonge mbele,

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja Kamati yetu ya Bajeti pamoja na hiyo Kamati nyingine.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hasna, tunaendelea na Mheshimiwa Balozi Adadi baadae

Mheshimiwa Sonia Magogo na Mheshimiwa Albert Obama wajiandae.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuchangia hoja hii ambayo ni muhimu sana. Kwanza nawapongeza Wenyeviti wote wawili; Mwenyekiti wangu wa Bajeti na Wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kumshukuru na kumpongeza Waziri Mpango. Waziri Mpango ambaye tulikuwa tunamjua miaka miwili iliyopita, siyo huyu Waziri Mpango wa leo. Huyu ni Waziri Mpango mpya kabisa, ni Waziri Mpango ambaye anasikiliza sasa hivi na ni Waziri ambaye anatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya kwa sababu nimeona jinsi ambavyo ameweza kuchukuwa mawazo mbalimbali ya Wajumbe wa Kamati ya Bajeti na kuweza kutekeleza mengi ambayo ameyafanya. Ni kweli kabisa ameweza ku-*stabilize,* unaona kabisa jinsi uchumi unavyoweza kupanda. Unaweza kuona jinsi ambavyo ameweza kuteremsha na kudhibiti mifumuko ya bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujawahi kufikia mfumuko wa bei wa kiwango cha bei 3.0. Hii ni historia katika nchi hii. Mimi nimekaa kwenye nchi ambayo ilikuwa na mfumuko wa bei *1.5 million,* sasa hivi tuko kwenye 3.0, kwa nini tusimsifie? Kwa nini tusiisifie Serikali ya Awamu ya Tano? Sasa hivi miradi mikubwa sana inafanyika, nyie wote mnajua Waheshimiwa Wabunge. Pamoja na miradi yote mikubwa hiyo, Wizara hii imeweza ku-*stabilize* mfumuko wa bei na kubaki kwenye kiwango hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru sana tena Mheshimiwa Silinde yuko pale, Mjumbe wa Kamati ya Bajeti. Mambo aliyoyaongea hapa, mengi jana tumeyamaliza. Kaongea suala la maji, ndiyo maana hakuwepo kwenye taarifa ya mwisho ambayo tumeiwasilisha hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji, ni kweli. Mheshimiwa Waziri wa Fedha hajagusa hata senti tano kwenye fedha za tozo ambazo zimekwenda kwenye Mfuko wa Maji, zote zimekwenda kwenye nani...

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Haya, Taarifa ya kwanza hiyo.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Silinde tulia!

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Tulia upewe taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Balozi Adadi kaa chini.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Adadi kaa chini. Halafu zima *microphone* hiyo.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwape taarifa Wajumbe wote wa Kamati ya Bajeti ambao ndiyo ukweli, tunajua wote, vyazo vya Mfuko wa Maji kwenye kuhudumia miradi ya maendeleo, vipo vitatu; tozo ya mafuta, ambapo Serikali ilikuwa imekadiria kwa mwaka mzima kukusanya shilingi bilioni 158.5; nusu mwaka shilingi bilioni 79. *Out of 79 billion* ya nusu mwaka, Serikali imekusanya shilingi bilioni 67 ambazo zimekwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo cha pili ni fedha kutoka Hazina, shilingi bilioni 299.9, wamepeleka shilingi bilioni 1,600 sawa sawa na silimia 0.6; na chanzo cha tatu ni Wahisani, shilingi bilioni 284, imetolewa shilingi bilioni 4.3 sawa sawa na 2%. Sasa haya yapo kwenye *Hansard* za Bunge za Kamati ya Bajeti.

Mhshimiwa Mwenyekiti, nimeona mnahangaika wakati huu ndiyo ukweli. Ndiyo maana nilisema, Mheshimiwa Rais amezungukwa na watu wanamwamiba uongo.

**MWENYEKITI:** Basi umeshafahamika. Mheshimiwa Balozi.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la SHILINGI bilionI 999 lipo na tumelijadili. Jana Waziri wa Fedha amekubali kupeleka fedha. Ndiyo maana nakwambia kwamba Mheshimiwa Silinde ukuwepo, naendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Silinde ni rafiki yangu sana, lakini taarifa yake siipokei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ni kwamba juhudi kubwa sana zinafanyika kwa kweli na ukiangalia hii nusu ya bajeti, fedha ambazo zilipelekwa kwenye miradi mbalimbali, ni nyingi sana. Nyingine zimezidi kiwango na ndiyo maana hapa baadhi ya Wajumbe wanasema kwamba lazima tuwe na uwiano. Fedha nyingine zimezidi viwango kutokana na mahitaji ya zile Wizara. Hili suala tulimwambia Mheshimiwa Waziri na ninaamini kabisa amelichukua na anakwenda kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli deni la Taifa limeendelea kukua na limefikia karibia shilingi trilioni 61.8. Hili suala tumemtahadharisha kabisa Mheshimiwa Waziri kwamba pamoja na deni la Taifa kukua, lakini Serikali imekuwa inalipa sana madeni ya nje kuliko madeni ya ndani. Sasa tulimwomba aangalie uwiano na aweze kulipa madeni mengi ya ndani ambayo yamekuwa ni kero kubwa kwa watu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo, kuna *blue print* nzuri sana imetengenezwa na ime-*cover* mambo mengi sana, lakini haijasema ni lini itaanza kutumika? Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Waziri suala hilo aweze kulifanyia mkakati na kuhakikisha *blue print* hiyo inafanya kazi kwa haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la diplomasia ya uchumi, sasa hivi ndiyo kwanza Serikali imenunua ndege. Sasa huwezi kutegemea hizi ndege zikupe faida. Ndege ni *facilitation.* Shirika lolote la ndege ambalo linapata faida ni shirika moja tu. Angalia labda *Emirates,* lakini mashirika yote

yanaungwa mkono na Serikali zao kuhakikisha kwamba linaleta wawekezaji, linaleta watalii na kuhakikisha kwamba inakaribia kufanya usafiri ule wa haraka.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa ya mwisho hiyo.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anaweza akawa yuko sawa, lakini kauli ya Mheshimiwa Rais, amesema kwamba ndege hizi zisipoleta faida, wanaozisimamia wanaona cha mtema kuni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Adadi, taarifa ya hiyo.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amesema kwamba ndege hizi zisipoleta faida, watakiona cha mtema kuni. Siyo ndege zenyewe tu, ni pamoja na wanaobebwa mle, ni pamoja na watalii watakaoingia mle, ni pamoja na wawekezaji ambao watakakuja. Kwa hiyo, ninachoweza kusema ni kwamba katika huu nusu mwaka kwa kweli Wizara ya fedha imejitahidi sana kutoa fedha zake na ndiyo maana unaona kwamba hata kwenye utekelezaji wa Sheria ya Fedha ambayo tuliipitisha hapa, tumeweza kujenga viwanda vya madawa karibu vitano. Hii ni kwa sababu ya kupunguza kodi ya mapato kutoka 30% mpaka 20%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanza kutumia *electronic stamp (ETS).* Wamenunua mitambo na tunategemea kwamba utekelezaji wake utakuwa ni mzuri na utaenda kuleta faida kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni suala na misaada na mikopo kutoka nje. Tulishazungumza na tumemshauri Mheshimiwa Waziri. Nimekuwa nikizungumza kila mara, hakuna faida ya kuingiza misaada hii kwenye bajeti na ndiyo kinachotokea sasa hivi kwamba wafadhili wamegoma kuleta fedha. Kwa nini hii misaada isiwekwe pembeni nje ya bajeti,

twende na bajeti ya pesa ambazo tunazo; tuachane na wafadhili wanaokupa ufadhili kwa masharti?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJABU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Sonia na baadaye atafuata Mheshimiwa Albert Obama na Mheshimiwa Peter Serukamba, ajiandae.

**MHE. SONIA J. MAGOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na leo tena nimeweza kusimama mbele ya Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati ya *PAC* na ningependa kuchukuwa fursa hii kumpongeza Mwenyekiti wangu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa kuwasilisha vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza, nilikuwa na ushauri kidogo kwenye haya Mashirikia na Taasisi ambazo Serikali inawekeza fedha zake. Ninachoona hapa kwanza haya Mashirika yenyewe kwa yenyewe wanatakiwa yawe na mahusiano mazuri. Ikiwa haya mashirikia yatajitangaza vizuri na ikajulikana yanafanya nini na wenyewe kwa wenyewe wakawa wanapeana huduma, kwa mfano SUMA JKT, wanatengeneza *furniture* nzuri sana, wanatengeneza *product* ya maji ambayo walileta kwenye Kamati yetu na tuliyaona ni mazuri na bei yake ni nzuri. Hivyo kama Serikali itaunga mkono na wenyewe kwa wenyewe wakasaidiana, kwa mfano, kukawa kuna maelekezo kwamba *furniture* zote zinunuliwe kutoka SUMA JKT, ama sehemu kubwa *furniture* za

Serikali ziwe zinatoka SUMA JKT, itawasaidia kutengeneza faida zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa bandari, tukiangalia bandari yetu ya Dar es Salaam, ina mlundikano wa mizigo mingi sana; lakini kuna bandari ya Tanga na bandari ya Mtwara. Kama kutakuwa na *categorization* ya mizigo mingine inakwenda Tanga, mingine inakwenda Mtwara, itasaidia na zile bandari nyingine kuweza kujiendesha vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunaona Serikali yetu inavyotumia fedha nyingi katika kutengeneza miundombinu ya barabara. Bandari wanaweza wakawatumia zaidi *TRC* kusafirisha mizigo kuliko kutumia malori ambayo yanapita na mizigo mikubwa kwenye barabara na kuharibu miundombinu ya barabara zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni bajeti ya Ofisi ya Msajili wa Hazina. Kama tulivyoona, hii Ofisi ina mashirika mengi sana ya kusimamia. Kama watapewa bajeti nzuri ya kutosha na ikaenda kwa wakati na wakawa wanafanya *performance contract* na zile Taasisi, pia wakawa na ufuatiliaji wa *expenditure* kwenye zile taasisi mara kwa mara, itasaidia kufanya zile taasisi ziwe na uwoga na kutengeneza faida kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo tunaona kuna madeni mengi sana hizi taasisi zinadai. Serikali ingeweza kuwasaidia ili waweze kukusanya yale madeni yao pale ambapo wao wamefikia ukomo. Kwa mfano, tunaona wengine ni waajiriwa Serikali na wengine wanajulikana wako wapi, wanaweza kutaifishiwa mali zao. Serikali iwasaidie kama vile ilivyowezekana kwenye Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na wenyewe wasaidiwe ili hizi fedha zirudi ziwadaidie kuendesha shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni suala la kukaimu. Mtu anapokuwa anakaimu, anakuwa na hali ya uwoga. Yaani anakuwa hana ile *full mandate,* anakuwa na

wasi wasi kwenye kile kitu anachokifanya, hasa kwenye zile level za *Management.* Kwa hiyo, kama watasaidiwa kuondoa hili tatizo la kukaimu na wakawa wanawapa wale watu wanaokaimu madaraka au kuziba zile nafasi kwa wakati, itasaidia sana kuchochea maendeleo katika zile taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sonia. Tunaendelea na Mheshimiwa Albert Obama. Mheshimiwa Peter Serukamba na Mheshimiwa Hawa Ghasia wajiandae.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nami nichangie kwenye taarifa hizi mbili. Kwanza nawashukuru Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote hizi mbili kwa ripoti nzuri ambayo wameweza kutuletea hapa mbele yetu; lakini pili niendelee kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa inayofanya kutuletea maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuanza na moja hili la Mheshimiwa Msigwa ambalo alisema, *economic growth* haiendani na *development growth;* ikiwa na maana kwamba anaongelea pato la Taifa. Kwanza tuipongeze Serikali yetu kwa miaka mitatu mfululizo kuanzia 2015, 2016 na 2017 uchumi umeendelea ku-*grow* kwa 7% ambapo ni kitu kikubwa sana, lazima tujipongeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mchungaji Msigwa ameendelea kuchanganya, haelewei maana ya pato la Taifa kukua. Viashiria vya uchumi kukua ni kuongezeka kwa miundombinu hii ambayo inaendelea katika nchi yetu. Kwa hiyo, unapoona miundombinu inaendelea kukua, ni moja ya kiashiria kwamba uchumi umekua na maendeleo sasa yanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya kupatikana umeme wa uhakika kuliko tulipotoka, vilevile ni kiashiria cha kwamba pato limeongezeka na huduma ya umeme sasa inakuwa nzuri vilevile na huduma za jamii. Hivyo, vyote ni viashiria ambavyo vinaonyesha uchumi wa nchi kukua. Kwa

hiyo, haina uhusiano wa moja kwa moja na fedha zake za mfukoni kama hufanyi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niendelee kuipongeza Serikali kupitia *TRA,* wamefanya kazi nzuri chini ya Mkurugenzi, Mheshimiwa Kichele. Ukiangalia mwenendo wa makusanyo ya nchi yetu, mapato yameendelea kuwa mazuri. Naendelea kumpongeza Waziri wa Fedha na timu yake ya wataalam wamefanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, wamekuja kwenye Kamati yetu, wamejaribu kuonyesha mapato ya nusu mwaka: Je, wameweza kufanyaje katika makusanyo? Ukienda kwenye mapato yanayotokana na kodi, jumla yake wameweza ku-*achieve* kwa asilimia 91, lazima tuwapigie makofi kwa namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma namba mbili, kuhusu ushuru wa forodha lengo la mwaka ni shilingi bilioni 1.2, lakini wameweza kukusanya shilingi bilioni 588 ambayo ni asilimia 88.7. Ni jambo kubwa ambalo inabidi tuwapongeze. Kwa hiyo, *TRA* mnafanya kazi nzuri, hongereni sana na Waziri wa Fedha mnafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye mwenendo wa misaada na mikopo nafuu hadi Desemba, ukiwapima kwa miezi sita ufanisi wao ukoje? Watu wanasema wafadhili hawatupi fedha, mikopo haiji; naomba niwaambie wameweza ku-*achieve* kwa lengo la nusu mwaka, wamefikia asilimia 66.4. Wapigieni makofi kwamba Serikali inafanya kazi nzuri. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuendelee kuwapigia makofi kwa sababu ukiangalia mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika Mashariki, sisi sasa Januari tumeweza kufika 3%. Mpaka Desemba, Kenya walikuwa 5.7% ambao wako juu, sisi tuko chini, ni lazima tuwe *proud* na tunachokifanya. Kwa hiyo, ni jambo zuri, tuendelee kuwapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimpima, Mheshimiwa Waziri Mpango, kaka yangu: Je, fedha anazokusanya anapeleka zinapoitajika? Kwa miezi sita mfano, kwa matumizi ya kawaida kwa lengo lake alivyojipangia kwa nusu mwaka amefikisha 62.7%. Kwa nini usimpe haki yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia na madeni mengine; ulipaji wa madeni ya ndani na nje, malipo na riba za ndani amefikia asilimia 32. Malipo ya riba na mitaji ya nje amelipa kwa asilimia 53 ya lengo. Kwa hiyo, naweza nikasema, Wizara ya Fedha ukiipima na nchi nzima kwa ujumla tunavyotekeleza bajeti yetu, Mheshimiwa Zitto unacho hiki kitabu umesoma, tunaenda vizuri na uende kwenye *media* na uwaambie Watanzania tunaenda vizuri. Kwa hiyo, ukiwapima, wanaenda vizuri kwa viashiria vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naishukuru sana Serikali kwa kazi nzuri sana inayofanya chini ya uongozi wa Jemedari JPM.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Obama, tunaendelea na Mheshimiwa Peter Serukamba, baadaye Mheshimiwa Hawa Ghasia na Mheshimiwa Munde wajiandae.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niwapongeze sana Mwenyekiti wa Bajeti na Mwenyekiti wa *PIC* kwa ripoti yao. Pia niipongeze Serikali kwa kazi kubwa wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu wa Malaysia alivyoshinda uchaguzi juzi Mahathir akiwa na miaka zaidi ya 90 aliulizwa swali moja, utafanya nini ili kuendeleza maendeleo ya Malaysia. Alijibu jambo moja tu alisema kazi yangu ni kuhakikisha asilimia 24 zinaendelea kuwepo. Maana yake ni nini? Anasema kila biashara iliyoko hapa nchini kwetu Serikali inapata asilimia 24. Kwa hiyo maana yake sisi ni *shareholder* wa kila biashara. Nami ningetamani niwaombe wenzangu Serikalini tuseme kila biashara ya Tanzania, sisi tuna

asilimia 30. Kwa hiyo tunalo jukumu la kulinda hii asilimia 30 iendelee kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu gani nasema haya, nasema biashara ikienda vizuri, kama kodi tumefika asilimia 88, tutafika asilimia 100 tutafika asilimia 180, hivi jambo likiongezeka ni mbaya? Kuna ziada mbaya kweli jamani. Mimi niwaombe wenzangu Serikalini tuanze kubadilika kwamba wafanyabiashara ni *partners* wetu. Wafanyabiashara ni *partners* wa Serikali hii. Ninayo mifano ya makampuni mengi sana ambayo ukiangalia kodi wanazolipa, ukiangalia wanavyoajiri watu, wanaleta fedha nyingi kwenye uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko tabia imeanza kukua kwamba tunadhani wafanyabiashara ni wezi, ni wahuni, ni watu wabaya, maneno haya yanasemwa na viongozi, hili siyo sawa. Juzi Mheshimiwa Rais amesema tunawahitaji wafanyabiashara. Kwa hiyo ningeomba na wale wengine ambao mnamsaidia Mheshimiwa Rais muanze kuona umuhimu wa wafanyabiashara. Leo Kariakoo imekufa, nitasema sababu chache za Kariakoo kufa. Ya kwanza ni *tariff,* Serikali yetu wafanyabiashara wadogowadogo anaenda India, anaenda China analeta *glass* ya shilingi elfu moja na kuna *glass* ya shilingi elfu kumi, akija mtu wa kodi anasema *glass* zote hizi ni shilingi elfu kumi, lakini watu wengi wanatumia glass za shilingi elfu moja matokeo yake *commoditie* zinazokuja ni bei ghali na matokeo yake watu wanaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili angalia, ni *harassment* tunayowapa, anakuja Mzambia anakuja na fedha zake, anafika Kariakoo anakutana na TAKUKURU, anakutaka na Polisi anakutana na *TRA,* huyu hawezi kurudi. Shughuli ya kodi inasomewa, watu wanakaa darasani wanapata *degree* ya kodi, hawa watu wanafanya *TRA,* tuwaombe Polisi na vyombo vyote vya ulinzi ya usalama wafanye kazi walizosomea. Yako madhara yako madhara ya kuwapa watu wakafanye kazi ambayo hawakusomea. Madhara haya ni makubwa, tunaharibu uchumi wetu wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Kariakoo mabenki yote yanafungwa, mnajua kwa sababu gani? Kila *branch* ya Kariakoo inafungwa, kwa sababu hakuna biashara tena, biashara yote imehamia wapi, Zambia, Kenya na Uganda. Hii siyo sawa, Mungu alituweka Tanzania *geographically,* Tanzania tuko mpakani ni kwa nia njema, tuutumie mpaka huu kwa maendeleo yetu lakini tunafanya nini. Tuangalie *trade* angalia *transit trade*, angalia vizingiti vya barabarani, lori mpaka lifike Zambia limesimamishwa zaidi ya mara 30, polisi wako *everywhere,* watu wa mizani wapo, sasa hizi tunaambiwa lazima tufuate sharia, lakini hii sheria ametunga nani, si sisi leteni tuibadilishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni suala la Afrika Mashariki, Kenya wanatudanganya, kwa sababu Kenya biashara yao haiko Zambia, haiko Kongo. Tanzania sisi wanaotuletea fedha ni Zambia, ni Malawi, ni Kongo, ndio watafuata Burundi kidogo, watafuata na Rwanda. Niwaombe sana Serikalini biashara hii isipokua, maana leo Waziri wa Fedha tutampiga maneno tu hapa, lakini Waziri wa Fedha tusipomsaidia biashara ikakua, hawezi kukusanya, hawezi kuleta hela ya maendeleo, tutaaanza kulalamika hapa. Kwa hiyo niwaombe wenzetu wazingatie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi kwenye *World Economic Forum* bosi wa *IMF* ameulizwa anasema ili nchi ifanye vizuri mambo machache sana, moja kubwa lililosemwa ni *growth,* kwamba lazima tulete fedha za kukuza uchumi, tukuze kilimo, tukuze biashara, tukuze kila jambo. La mwisho akasema ni suala la *private sector,* ndugu zangu tukidhani Serikali inaweza ikafanya kila kitu, kuna mtu tunamdanganya sio kweli. Nenda kuanzia China, nenda kote unakokujua ambako wameendelea juzi kilichofanya waendelee ni *private sector.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niwaombe sana, unajua niwaambieni hakuna nchi iliyoendelea kwa kuwa na maskini peke yake, haipo, *no single country* imeendelea kwa kuwa na maskini peke yake. Tufanye jukumu la kupunguza umaskini, tufanye jukumu la kuondoa wanyonge kwenye uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu mmoja akiwa na pesa, leo Mbunge mmoja akiwa amepata Ubunge na niwaulize Wabunge wenzangu kuna watu wamepata Ubunge ndio ameajiri dereva, ameajiri Katibu na kadhalika kwa sababu ya nini tuna *income* zaidi. Uchumi pia unafanya kazi hivyo hivyo, akitokea mtu akawa tajiri, huyu mtu ataajiri watu wengi. Bakhresa hajasoma, lakini ameajiri wenye *PhD* ni kwa sababu ana uwezo wa kifedha. Kwa hiyo, kudhani wafanyabiashara ni watu wabaya siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala hapa limesemwa na naomba sana amesema Mwenyekiti wa *PIC* tunayo mashirika zaidi ya 11 yametupa *dividend* bilioni 35. Nasema hizi hazitoshi, tuyasaidie mashirika haya yafanye vizuri zaidi. Nami ningemwomba Mwenyekiti atakapokuja mwaka kesho asiishie kwenye *dividend,* nataka atuonyeshe mashirika haya yamechangia shilingi ngapi kwenye uchumi. Watuoneshe maana kuna watu wanadhani ile Kampuni naweza nikaifuta tu, wewe unafuta kampuni *assume* leo watu wamesema hapa habari *PUMA,* tukiamua hapa leo kuifuta *PUMA* unajua maana yake ni nini? Unapoteza zaidi ya bilioni 400 kwenye uchumi wako, sasa unapata nini ukiifuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kusema jambo moja la *ATC*. Nataka nichukue nafasi hii kabisa kupongeza uamuzi wa kuwa na Shirika letu la ndege na niwaombe wenzangu tusiwe na haraka ya kupata faida, tunachotakiwa ni kuangalia *multiplier effect* ya kuwa na *airline*. Ukishakuwa na *airline* yako muuza mafuta atakupa *dividend,* muuza mafuta ya ndege utapata *corporate tax* utapata *tax* faida, lakini ameuza mafuta mengi kwa sababu una ndege, utapata ajira kwa sababu una ndege, utapata kodi kwa sababu una ndege, lakini utafanya biashara ichanganye Dodoma hukai masaa manane barabarani utawahi, uje ufanye biashara urudi. Hii ndio faida ya kuwa na *airline* in the *country.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pale *Airport* mtu akipita pale atanunua kitu yule mwenye *duty free* utapata kodi kule, matokeo yake ndio faida ya kuwa na *Airline*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru na naomba niwashukuru Wenyeviti kwa kazi nzuri waliyofanya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Serukamba. Tunaendelea na Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema nami kuweza kusimama mbele ya Bunge tukufu ili niweze kuchangia hoja mbili ambazo zimewasilishwa katika Bunge letu Tukufu. Pia napenda niwapongeze Wenyeviti wote wa Kamati kwa taarifa nzuri sana ambazo wameziwasilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia maeneo machache sana, kwanza nikianza na taarifa ya mwaka ya Kamati ya Uwekezaji Mitaji ya Umma *(PIC)*. Niwapongeze wote waliochangia nami niungane nao katika kuiomba Serikali kuziongezea mitaji taasisi zetu ambazo ziko chini ya Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndio maduka yetu, hivi ndio viwanda vyetu ambavyo Serikali inaweza ikatuongezea pato letu la Taifa na katika biashara yoyote ni lazima uwekeze ndipo uweze kuvuna. Kwa hiyo, kwanza nashauri Sheria ya Msajili wa Hazina ipitiwe upya ili kuweza kumwezesha Msajili wa Hazina kufanya kazi zake kwa ufanisi. Pia napendekeza ikama katika Ofisi ya Msajili wa Hazina iongezwe na pia katika kuipitia sheria napendekeza ikiwezekana tuanzishe Mfuko wa uwekezaji ambao wenyewe ndio utakuwa unatoa mitaji kupeleka katika mashirika yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo mashirika ambayo tumeingia ubia, *PUMA* tuna ubia lakini tunayo mashirika mengi kama *TPDC* imeingia ubia na mashirika mengi kama *MMP* na pia tumeingia ubia sigara, tumeingia ubia *ALAF,* lakini katika ubia ule uwekezaji wetu kidogo ni mdogo sana ukilinganisha na wabia wenzetu. Sasa kwa kuwekeza kidogo inapelekea mapato yetu au gawio letu kwa kweli kuwa kidogo kwa

sababu tunawekeza kidogo. Kwa hiyo napendekeza tuwe na mfuko wa uwekezaji ambao utamwezesha Msajili wa Hazina kuweza kutoa mitaji katika yale mashirika ambayo anayasimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo nataka nichangie ni kuhusu suala la *ATCL*. Niungane na wenzangu kuipongeza Serikali yetu kwa kuwa na Shirika letu la Ndege. Napenda niwaambie kwamba Shirika la Ndege tusiangalie *balance sheet* ya shirika kwamba, faida tumetumia kiasi gani tunapata kiasi gani, tuangalie faida katika uchumi mpana, idadi ya watalii walioletwa, uwekezaji utakaokuja. Katika kuthibitisha hilo nendeni mkaangalie Shirika la *Emirate* ambalo sasa hivi kila mtu analipigia mfano, wakati linaanza lengo lake kubwa halikuwa kuweka faida. Lengo lilikuwa ni kuifanya Dubai iwe kituo cha uwekezaji, iwe kituo cha utalii. Sasa hivi Dubai asilimia 20 ya mapato yake...

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba Shirika la ndege linapoanzishwa, wanakuwa na *business plan* na unapoanza unaporusha tu ndege huwezi kupata faida siku hiyo hiyo na kuna kipindi utapata unakwenda mpaka kwenye *breakeven point* ndipo unakwenda kupata nini faida. Jambo lingine kuna malengo mengine ya kuanzishwa kwa Mashirika ya Ndege ikiwepo kuboresha usafiri, lakini kuimarisha njia kuu zaa uchumi. Naomba apokee taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unitunzie muda wangu, taarifa naipokea, na ndio maana nilikuwa nasema naungana na Serikali kwa kununua ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu leo labda China hata Tanzania hawaijui, lakini siku ndege yetu ikitua

Guangzhou, watu wataanza kujiuliza, Tanzania iko wapi, kuna nini, kuna vitu gani vinapatikana huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dubai kuanzia Disemba mpaka inafika Machi hoteli zote zimejaa, mji umejaa na pato la Taifa la Dubai kwa mwaka 2018 asilimia 20 lilichangiwa na utalii na utalii huo ulibebwa au watalii hao walibebwa na Shirika la *Emirate* na walichangia katika uchumi mpana kwa watalii kwenda pale. Kwa hiyo, niwaombe ile habari ya kusema sijui tumenunua hivi, tumepata vile, hiyo ni biashara ya machungwa, lakini unavyoangalia biashara kama ndege unaangalia katika uchumi mpana, idadi ya watalii shirika litatangaza nchi yetu na italeta *multiplier effect* kubwa sana kuliko ambavyo watu wanafikiria, lakini pia nina imani kabisa shirika letu litakuja kufanya faida na kupunguza gharama za usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Mtwara ambako *Bombadier* zimekatiza kwa sababu ya Ruvuma, nauli ya ndege kwa kutumia *Precision* ni kubwa kuliko eneo lingine lolote ndani ya Tanzania hii. Kwa hiyo, kwa kuwa na Shirika letu pia tunasaidia kupunguza gharama za usafiri wa anga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Ghasia, tunaendelea na Mheshimiwa Munde.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuchangia. Kwanza kabisa nianze kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa ambayo anaifanya, wote tunaiona lakini nimpongeze kaka yangu Waziri Mpango, Naibu Waziri na menejimenti nzima ya Wizara ya Fedha kwa kazi kubwa wanayoifanya ya usimamizi mzuri wa bajeti ambayo waliileta hapa Bungeni. Tunaamini bajeti hiyo inasimamiwa vizuri na ndio maana mambo yote yanakwenda kwa sababu ya usimamizi na udhibiti wao mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye mjadala, nimesikia wanasema kwamba tusipokuwa makini Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha baada ya utawala huu wanaweza kufungwa. Niwaambie hafungwi mtu hapa, kwa sababu kazi zote zinaonekana zinavyofanyika.

Serikali iliyopita tulikuwa hapa Bungeni walikuwa wanasema Serikali hii haidhibiti rasilimali za nchi, Serikali hii ni dhaifu, leo tumepata Serikali inayodhibiti maliasili ya nchi yao, utafikiri maliasili zile ni za kwao wao binafsi, lakini leo hii wanakuja tena kuwaambia watu hawa watafungwa kwa kushindwa kudhibiti rasilimali za nchi yetu. Niseme hiki kitu siyo kweli, tumeona Mheshimiwa Rais amepambana kwenye madini, ameleta sheria tumebadilisha, yote hiyo ni kudhibiti rasilimali za nchi yetu ili Watanzania waweze kunufaika na rasilimali hizo. Tumeona Rais amepambana kwenye rushwa kwenye uwajibikaji, kwenye nidhamu ya watumishi na mambo yanaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii wanamwambia mtu atafungwa, unabaki unashangaa, atafungwa kwa kutoa bajeti ya afya bilioni 30 mpaka bilioni 260, atafungwa kwa kusimamia ujenzi wa reli ya kisasa kwa kutumia pesa zetu za ndani, atafungwa kwa ujenzi wa barabara, atafungwa kwa kusomesha watoto wetu elimu bure, atafungwa kwa ndege sita zilizonunuliwa kwa mpigo. Nimuombe Waziri wa Fedha na Katibu Mkuu wasikate tamaa, waendelee kuwafanyia kazi Watanzania kama wnavyowafanyia. Tumeona kabisa ndani ya miaka mitatu kazi kubwa iliyofanywa na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeonekana. Leo kule kwetu sisi Tabora, Mkuu wetu yule wa Mkoa, watu wanaona kama vichekesho lakini anaongea ukweli, anasema Tabora imekuwa kama Toronto, sio utani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifika saa 12 mitaa yote inawaka taa, mitaa yote ina lami, kule tulipozaliwa sisi Uswahilini kulikuwa hakuna lami toka tumezaliwa mpaka sasa ndio tumekuja kuiona lami. Nasema Serikali inafanya kazi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu hawa hawaeleweki, wasipofanya kazi wanawaita dhaifu, wakifanya kazi wanawaita madikteta, tabia zao sio za kiume wala sio za kike, hawa watu sijui ni wa aina gani, nashindwa kabisa kuwaelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Rais kwenye suala zima la korosho, tulikuja hapa Bungeni tukajadili sana kuhusu korosho, tukapata wanunuzi wanataka kununua kwa shilingi elfu mbili na kidogo. Rais wa wanyonge akakataa, akasema korosho hizo atazinunua yeye mwenyewe, lakini tunashuhudia amepatikana mnunuzi, amezinunua kwa shilingi 4,480, tunampongeza sana Rais amepambania wanyonge wake kwa vitendo. Ajabu leo unakuta mtu analaumu tu, anaona haya mambo ni mepesi, anaona haya mambo ni rahisi, huu ni uthubutu wa hali ya juu aliouonesha Rais. Rais wetu ni jasiri Rais ana maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata tabu sana, hawa watu kila siku wanatuambia hawauoni utawala bora, wanaona udiktekta tu. Mimi nashindwa kuelewa hawa watu wako huru, wanaita vyombo vya habari, wanaongea na vyombo vya habari, wanafanya wanavyovitaka, wanaisema Serikali, wanamsema Rais lakini bado wanasema hakuna utawala bora. Utawala bora kwao ni maandamano tu ndiyo wataona kwamba kuna utawala bora. Yapo wanayoyasema, wanaenda Mahakamani, wanashtaki, hatua zinachukuliwa, maamuzi yanatoka, lakini bado hawaioni Serikali kama ina utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wamekuwa wakitushawishi tukubali masharti ambayo kama nchi yetu na tamaduni zetu hatuwezi kuyakubali. Mimi niendelee kuipongeza Serikali iendelee kuwa na misimamo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote nimekuwa nikimwambia Rais wangu kupitia Bunge hili pamoja na viongozi waendelee kufanya kazi zao kama walivyojipangia, wasiyumbishwe na mtu yeyote, wasimfuate mtu yeyote maana hawa watu wanawayumbisha kwa makusudi ili siku

ya mwisho waje wawaambie kwamba wameshindwa kufanya kazi na waweze kusema. Tumeona miaka mitatu mapinduzi yaliyotekea ni makubwa, maendeleo yaliyotokea ndani ya miaka mitatu ni makubwa, mtu yeyote unayemwambia aangalie anaona, nashangaa wanapokuwa kila saa wanalaumu, kila ni watu wa kubeza...

**TAARIFA**

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nimpe taarifa mzungumzaji anayeendelea kuzungumza, inaonekana hivi vitabu vya hotuba za Kamati havipitii. Ukienda kwenye *para* 2.2.3, ukurasa wa 19, ukosefu wa Sera za Uwekezaji...

**MBUNGE FULANI:** Kamati gani?

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Kamati ya *PIC*. Inasema, ukosefu wa Sera za Uwekezaji na Mpango Mkakati wa Kibiashara kwa taasisi zinazofanya uwekezaji. Kwa hiyo, ina maana Kamati wanazungumzia kwamba shida kubwa ni ukosefu wa Sera za Uwekezaji na Biashsara. Hiki kinachosemwa hapa ndiyo tunaisaidia Serikali ili iweke Sera za Uwekezaji na Biashara ili haya yanayofanyika, hizo ndege na mambo mengine zilete mafanikio kwa ajili ya hii nchi, siyo kwa sababu ya ubishani, asome hiki kitabu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Munde.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimu sana aliyetoa hii taarifa lakini hawezi kunilazimisha hicho kipengele chake kwa sababu yeye ni mfanyabiashara, wote tuongelee biashara hapa ndani. Mimi naongelea kupongeza Serikali yangu kwa kazi kubwa inayoifanya, ndicho nachoongelea mimi na hawezi kuni-*drive*

anapotaka yeye. Tena namheshimu ni rafiki yangu, kutwa ananiambia anataka kurudi CCM huyu wewe muache tu. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kukutana na wadau wa madini, yote hii ni juhudi kubwa za kutaka kuongeza pato la nchi yake, za kutaka kuongeza uchumi wetu ili Watanzania waendelee kunufanika na matunda yao. Mheshimiwa Rais ambaye anahitaji amani kila siku amekutana pia na Viongozi wa Dini ili kuweka amani katika nchi yetu, kusikiliza kero zao na mambo kadha wa kadha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Rais akutane na wadau wa pamba, tumbaku na kahawa. Mazao haya tunayategemea sana kwa ajili ya kuingiza fedha za kigeni kwenye nchi yetu lakini yanategemewa pia kwenye viwanda vyetu vya ndani na yanatoa ajira kwa vijana wetu na sisi wenyewe. Kwa hiyo, niombe pale Mheshimiwa atakapopata nafasi akutane na wadau wa mazao haya makuu ya nchi yetu ili kuleta tija kama alivyoleta tija kwenye madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Munde. Sasa tunaendelea upande wa Mawaziri, tunaanza na Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro dakika tano, atafuatia Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Hasunga na *Engineer* Kamwelwe.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tulikuwa tunajadili taarifa hizi mbili za Kamati za Bunge. Nikianza na taarifa ya

Kamati ya Bajeti, katika ukurasa wa 10, kipengele 2.2.3 kimeongelea diplomasia ya uchumi. Nichukue fursa hii kuishukuru Kamati kwa kuipongeza Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kazi nzuri inayofanya kwenye diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya kujadili ripoti hii na mambo ambayo yameandikwa katika ukurasa wa 10 na 11 yanayohusu Wizara ya Mambo ya Nje, baadhi ya wachangiaji wamejikita kujadili mambo ya ushoga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Waheshimiwa Wabunge tunatumwa na wananchi kuja kuipa Serikali maagizo. Kwa ruhusa yako, naomba uniruhusu niwaulize Waheshimiwa Wabunge kama kuna Mbunge yeyote ametumwa na wananchi wake kuja kutetea ushoga humu Bungeni. Kama yupo anyooshe mkono juu au ajifanye kama anajikuna. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama huyo Mbunge hayupo ambaye ametumwa na wananchi wake, basi anyamaze milele kuanzia sasa. Ili nchi hii iweze kuendelea tunahitaji kujituma na kuchapa kazi sisi wenyewe. Tunahitaji kulipa kodi kwa mujibu wa sheria za nchi. Hakuna mwekezaji wa nje atakayekuja kuikomboa nchi hii. Wawekezaji watakuja kuchuma na ili wachume vizuri wanatuvuruga kwa kutupa masharti hayo mbalimbali kama vile ya kutaka tukubali mambo ya ushoga.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea *sovereignty of the country.* Watu wengi wanadhani *sovereignty* ni kitu chepesi sana. Suala la

*sovereignty* lilianza kukubalika mwaka 1648 kupitia *Westphalia Treaty*. Baada ya vita ya miaka 30 umwagaji mkubwa wa damu na majadiliano ya miaka minne ukapatikana mkataba wa *Westphalia* ambao ndiyo umeleta suala zima la *sovereignty*. Leo tunalichukulia suala hili kiwepesi wepesi sana. Tunataka uhuru wetu huu wa kujiamulia mambo tuukabidhi kwa watu wengine, hilo halitawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesemwa sana kwamba hatuna uhuru wa vyombo vya habari. Mimi naomba kusema kwamba Tanzania tuna redio 158, TV 34, magazeti 216 na tuna mitandao ya kijamii 224. Hii yote imeonyesha kitakwimu tuna uhuru wa vyombo vya habari. Pia tuko huko kuongea, kuikosoa Serikali na kutoa maoni pasipo bugudha yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono taarifa hizi za Kamati zote mbili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro. Tunaendelea na Mheshimiwa Waitara baadaye Mheshimiwa Hasunga ajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwenye taarifa hizi mbili, kuna mambo yanayohusu maboma na mimi nimepewa dhamana ya kusimamia elimu upande wa TAMISEMI kama Naibu Waziri, lakini nataka niseme tu kwamba huwezi kuwa unakula keki wakati huo huo tena unataka ibaki kama ilivyo. Kwa hiyo, kama unaamua kufanya miradi mikubwa kama kununua ndege sita, mradi wa umeme wa maji kule Rufiji, reli ya umeme na vitu vingine, lazima kuna baadhi ya mambo yapungue, tukubaliane hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, nilitaka niwaombe Waheshimiwa Wabunge, maboma ni kweli kazi imefanywa na Ofisi ya TAMISEMI, tuna maboma nchi nzima zaidi ya 8,110, ambayo inahitaji takribani shilingi bilioni 140.

Kazi imefanyika na mipango ya Serikali sasa ni kupeleka fedha kukamilisha maboma haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, maelekezo yametoka kwenye Halmashauri zote kwamba kila Halmashauri na ndugu yangu Mheshimiwa Silinde alikuwa anazungumza Momba imeelekezwa asilimia 40 ya fedha ya mapato ya ndani ziende kwenye huduma za kijamii ikiwepo elimu. Sasa Mheshimiwa Mbunge angetusaidia yeye amesimamia imeenda asilimia ngapi katika eneo lake. Kwa hisani ya Mheshimiwa Rais Magufuli, Momba imeongezeka uandikishaji darasa la kwanza kutoka asilimia 61 mpaka asilimia 83.1. Analeta fedha nchi nzima kila mwezi, zaidi ya shilingi bilioni 9 shule ya msingi, zaidi ya shilingi bilioni 20 sekondari, shilingi bilioni 5 ni posho ya watendaji kwa maana ya Wakuu wa Shule, Walimu Wakuu na posho ya madaraka kwa watendaji. Serikali hii pia imepeleka pikipiki kila Kata karibu nchi nzima ili wakasimamie elimu na kuboresha ubora wa elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa wanapozungumza habari kwamba kuna miradi imekwema, tumekataa misaada na mikopo ya masharti. Tutapokea mikopo ile ambayo haitutwazi utu wetu na haitudhalilishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunavyozungumza tangu tumeanza Mradi wa *EPforR* zimeshaenda fedha zaidi ya shilingi bilioni 98. Mwezi huu Waheshimiwa Wabunge mtaangaliaangalia kwenye Majimbo yenu, tumepeleka fedha shilingi bilioni 53.34 kwenye *EPforR* kujenga madarasa, mabweni, nyumba za walimu na vitu vingine kadha wa kadha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza tuna miradi mbalimbali nchi nzima inayotekelezwa na wafadhili na mabilioni ya fedha yanakuja mfano Mradi wa Tusome Pamoja na kadhalika. Wafadhili hao ni *World Bank,* Uingereza na Sweden ambapo wametoa fedha na tunaenda nao sawasawa. Kwa hiyo, miradi iliyopangwa chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe itakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niseme hapa jambo la msingi sana. Waheshimiwa Wabunge, mimi nimesikiliza michango hapa, hizi ni Kamati za Bunge na niwashauri ndugu zangu wa Upinzani na mnisikilize vizuri yako mambo ambayo ukiyasema vizuri Serikali itapokea lakini ukianza vibaya utamaliza vibaya, ukianza vizuri utamaliza vizuri. Unaweza ukawa na hoja nzuri sana lakini namna ambavyo unai-*present* kwa kukashfu haitapokelewa, watu wataipinga, ndiyo maana watu wana-*react* kwa sababu ya hoja ambazo zinakuja upande wa pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi katika hali ya kawaida kwa Mtanzania yeyote na hii lazima muifanyie kazi, kwa kazi ambazo anafanya Mheshimiwa Magufuli Watanzania wote wameshakubali mmebaki nyie tu na nyie ni wachache. Kwa mfano, alipokuwepo Mheshimiwa Kikwete alisemwa vibaya kama mnavyozungumza leo, leo mnasema Mheshimiwa Magufuli na wenzake wakitoka wataenda mahakamani haya maneno ni maneno ya kawaida, kelele za chura hazimnyimi ng'ombe kunywa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, hoja za upinzani zimeisha nchi hii, sasa hoja ni za kuungaunga, tuchape kazi, tujipange, tujifungie, tupokee maoni ya Kamati tukatekeleze. Tukienda kwenye uchaguzi tunataja hoja mnatoa maneno, Watanzania watapanga wanachagua maneno au wanachagua vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naomba niwasilishe. *(Makofi/Vigelegele)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waitara. Namkaribisha Mheshimiwa *Engineer* Kamwelwe na Mheshimiwa Mpango ajiandae.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kunipa nafasi na mimi niweze kujibu majibu ya Serikali kupitia mawasilisho ya Kamati

hizi mbili; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma *(PIC).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa michango mingi ambayo Wabunge wamechangia lakini nianze kwa kusema kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iko makini na imejipanga. Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Rais wetu mpendwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli inatambua ilipo, inatambua Tanzania iko wapi, inawajua Watanzania wote na mahitaji yao, inatambua inatoka wapi na inakwenda wapi lakini pia inatambua mahusiano ya nchi yetu ya Tanzania na dunia. Hilo huwezi kulijua kama utabaki huko uliko. Nimpongeze sana Mbunge wa Jimbo la Serengeti, Mheshimiwa Chacha Ryoba ni muda mfupi amekuja na ameshatambua tatizo alilokuwa nalo akiwa huko na sasa yuko huku anaelewa maana ya nchi nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Bunge ni kutunga sheria na sheria hizi utekelezaji unafanywa na Serikali. Pia kazi ya Bunge ni kusimamia na kushauri Serikali lakini inatekeleza hayo kupitia kwenye miundo ambayo imewekwa na Bunge lenyewe. Sasa hivi tunajadili Kamati hizi mbili na taarifa tunayoijadili iko ndani ya vitabu hivi vya Kamati, jana tulichambua taarifa za *CAG*. Sasa wakati mwingine unaona mtu anajadili kitu ambacho hakipo ndani ya hizi taarifa lakini ni kwa sababu tu ungekuwa umeshakuja huku haya usingeyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wameshayazungumza kwenye umma, basi nitayajibu. Nianze na *ATCL*. Wabunge wa Chama cha Mapinduzi nashukuru sana kwamba mmesaidia kulizungumza hili. Kwa sababu Shirika la Ndege usiliangalie kwenye kitu kimoja tu kwamba halijaleta faida, tena faida yenyewe bado haijapitiwa na *CAG* ili uweze kupewa taarifa kwamba kuna faida au kuna hasara. Shirika letu la Ndege limejipanga lina *Business Plan* na waendesha ndege *(pilot)* mpaka sasa hivi tunao 50 na ni

ndege zote kuanzia kwenye *Dreamliner* mpaka *Bombardier Airbus*.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Tutaendelea na ununuzi wa ndege.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niwape tu faida, kila ndege tunayonunua mikataba tunayoingia ni pamoja na ufundishaji wa ma-*pilot*.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Kwa hiyo, tunampango ambao ni endelevu.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewaambia kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi imejipanga.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Ndiyo maana sasa hivi inakarabati gereji ya KIA ambayo itakuwa gereji kwa ajili ya matengenezo ya ndege. Serikali ya Chama cha Mapinduzi imejipanga ndiyo maana Chuo cha *NIT* tunajenga ndiyo kiwe Chuo Kikuu cha *Aviation* ambapo mafundi wa kutengeneza ndege watafundishwa (*maintenance engineer)* lakini pamoja na ma-*pilot*.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ester Bulaya ametoa taarifa sijui amezipata wapi...

**MBUNGE FULANI:** Kwako.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Wewe shemeji yangu Mheshimiwa wewe, hatuchukui mambo ya mitaani, bado hatujaenda kutengeneza hizi ndege ili tuweze kujua tumetumia shilingi ngapi lakini bado *CAG* hajapitia haya ili tuweze kujua kama kuna faida ya shilingi bilioni 4, umeyapata kutoka kwenye kitabu kipi, hata mimi mwenyewe Waziri sijui. Haya ni mambo ya mitaani na wewe ni Mbunge mzoefu siyo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na taaarifa nazo naona kama ni za kutoka mitaani, watu wanazungumzia *PUMA*. *PUMA* sina taarifa kwamba yeye ndiyo ana *monopoly* ya biashara ya mafuta duniani. Vivyo hivyo sina taarifa kwamba *PUMA* ana *monopoly* ya mafuta Tanzania. Waheshimiwa Wabunge, Bunge limetunga sheria na sheria hizo zinatekelezwa na Serikali kwamba mtu anayepewa mkataba wa ku-*supply* mafuta ya ndege anapewa muda, kuna siku ya kwanza mpaka siku ya mwisho na ikifika siku ya mwisho anafanyiwa *evaluation* kama anaenda vizuri ataendelea, kama haendi vizuri basi sheria ndiyo zinazosema kwamba hawezi kuendelea. Sasa nitashangaa kama Bunge au Mbunge ndiyo anayesimamia kwamba *PUMA* apewe leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Waheshimiwa Wabunge acheni Serikali ifanye kazi yake, na Serikali hii ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, iko makini kama mnavyoona Mawaziri wake hawalali, kila mtu anafanya kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Kamwelwe, kabla ya...

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa naunga mkono hoja, taarifa zote mbili.

**MWENYEKITI:** Haya, kabla sijampa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba nimpe dakika tano Mheshimiwa Hasunga na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji dakika tano.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru sana kwa kupewa hii nafasi, na kwa sababu ya muda nitakwenda haraka haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa ambayo ameifanya katika kusimamia uchumi wetu, ambapo viashiria vyote vinaonyesha kwamba uchumi wetu unakuwa na unafanya vizuri. Haijawahi tokea katika historia mfumuko wa bei umeshuka mpaka hadi kufikia asilimia 3.0 kwa kweli ni kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ambalo nataka niliseme kidogo ni kwamba tunayo Benki yetu ya Kilimo ambayo inafanya vizuri na pengine hapa labda nitoe ufafanuzi kidogo benki yoyote, kazi ya benki, ni kutafuta fedha mahali ziliko nyingi na kuzipeleka mahali zinapohitajika na fedha hizo zinaweza zikapatikana kwa wenye mitaji, ama kwenye mikopo ama kwa Wawekezaji kwa hiyo, benki yetu ya kilimo, inazo fedha za kutosha, za kuweza kufanya kazi, na kusaidia kilimo. Na kutokana na hilo basi, ndio maana Serikali tuliamua tukaipa, tukaomba iikopeshe Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko fedha za kununua korosho na kwenda kuuza na imetoa fedha zote. Kwa hiyo, naomba niseme fedha za kununua korosho hatujatumia fedha tulizonunulia, fedha zilipatikana kwenye mkopo kutoka Benki ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitoe ufafanuzi, kumekuwa na taarifa za upotoshaji juu ya bei ambayo tumenunulia korosho, wengi wanasema tumenunua kwa shilingi 3,300. Nataka niseme hivi, bei tuliyonunulia sio hiyo, kwenye miaka ya nyuma utaratibu uliokuwepo ilikuwa ukinunua kwa shilingi 3,300 ndio unaanza kutoka gharama mbalimbali, gharama za magunia, gharama za maghala na vitu vinginevyo, ndio ilikuwa bei. Kwa sasa hivi, ile 3,300 ni ile anayolipwa mkulima, ni ile anayolipwa mkulima, kwa hiyo basi maana yake bei ya korosho, tuliyonunulia unaongeza magunia shilingi 62.50 kwa kilo, unaongeza usafiri kutoka kwenye *AMCOS* kwenda kweye maghala makuu. Unaongeza maghala shilingi, 38 unaongeza gharama za uendeshaji wa ushirika *AMCOS* shilingi 70 union shilingi 50 na gharama zingine, unaongeza *cess* ya Halmashauri ukizijumlisha bei yake tuliyonunulia ni zaidi ya shilingi 3,600. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulichokifanya tumelipa vingine na vingine bado, hatujalipa, tutalipa vyote, ukijumlisha na *export duty* ya shilingi zaidi ni asilimia 15 ya *FOB*...

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Taarifa

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni shilingi 560, ukijumlisha utapata ni zaidi ya 4,190,...

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WAZIRI WA KILIMO:** Kwa hiyo hizi gharama walizokuwa wanasema, naomba niweke hizo rekodi kwa wale wenzangu ambao hesabu zinapigwa hivyo...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo faida...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda hautoshi, kwa taarifa, naomba uendelee Mheshimiwa Hasunga.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Hoja, korosha inanunuliwa shilingi 2,600 sasa hivi ndiyo hoja hiyo tujibiwe.

**MWENYEKITI:** Kaa chini.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tukishamaliza sasa kulipa na kuuza, sasa tumeuza hizo tani laki moja tunaendelea kuuza, mwisho baadae tutapata sasa tumeuliza zote kwa shilingi ngapi, gharama yote wadau wanaohusika tumewalipa shilingi ngapi, ndio tutakuja kujua kama tumepata faida shilingi au kiasi gani, sio wakati huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niweke taarifa vizuri na nihakikishe kwamba Serikali tumefanya vizuri kwa kupitia Bodi yetu ya nafaka na mazao mchanganyiko, mpaka hadi juzi, uhakiki uliofanyika ni wa thamani ya bilioni 442.9 malipo yaliyofanyika hatujakopea hata hizo tulizouza bado, tuliofanya ni shilingi bilioni 424.8; wakulima waliolipwa mpaka sasa hivi, ni 390,466.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyama vya Ushirika ambavyo, vimelipa ni 605 kati ya vyama 606,

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hasunga.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Hasunga, Mheshimiwa Dkt. Kijaji.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana, kwa kunipa nafasi hii, naomba nichangie Taarifa ya Kamati ya *PIC* kwa machache yaliyosemwa. Lakini naomba nianze hapa alikoishia Mheshimiwa Hasunga, ndugu zangu Katiba, Sheria wala Kanuni yoyote ndani ya Taifa hili, haipo iliyozuia Taifa hili kufanya biashara ndio maana *PIC* Mwenyekiti wake anatueleza Serikali kwamba tuendelee kusimamia mashirika yetu ili yaendelee kufanya vizuri. Sasa hiki mnachokisema kwamba Serikali ilinunua korosho elfu tatu na mia ngapi, imeuza bei hii halafu yote ipelekwe kwa mwananchi *that is not a business analysis*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hilo, nilitaka nianze kulisema hivyo, naomba tu tulie ili tuweze kusikilizana na na tuelewe nini Serikali inafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na jambo moja muhimu ndani ya Kamati yetu ya *PIC* na niishukuru sana Kamati ya *PIC* kwa kuendelea kutoa ushirikiano/kutoa ushauri na hata nilipopitia kitabu chenu, maazimio yote, mmeshauri Serikali iwe iendelee kufanya *improvement* katika maeneo mbalimbali, nakushukuru sana kwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika tangu nimeingia ndani ya Bunge hili, na ndani ya Wizara ya Fedha, jambo kubwa ambalo Kamati hii ilikuwa inaongelea ilikuwa ni kuimarisha na kuboresha ofisi ya Msajili wa Hazina. Kama Serikali tulilipokea kwa mikono miwili, tukafanyia kazi Maazimio haya ya Bunge na leo hii napenda kumpongeza Msajili wa Hazina na watu wake, wanafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema hayo wanafanya kazi nzuri kwa sababu gawio lililotolewa na Taasisi haijawahi kutokea katika historia ya Taifa hili, tuliona wenyewe Taasisi zimetoa gawio kwa sababu ya uimara wa Ofisi ya Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la TEHAMA ambalo Kamati imesema napenda kusema kwamba tayari tumeanza na sasa hivi mfumo, wa TEHAMA wa Ofisi ya Msajili wa Hazina upo katika kufanyiwa majaribio na kati ya taasisi za Serikali, taasisi 27 tayari zimeshafanyiwa majaribio na tayari zimeshazipata mafunzo ya jinsi ya kutumia mfumo huo, mfumo wenyewe unaitwa *Financial Analysis Reporting System* ambayo ndiyo kazi kubwa ya Ofisi ya Msajili wa Hazina. Kwa hiyo, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamependekeza, kama ambavyo Kamati imependekeza tumesikia kama Serikali na sasa tunaifanyia kazi hii sasa itatupa nafasi popote pale alipo Msajili wa Hazina popote pale alipo Katibu Mkuu wa Hazina ataweza kuona Taasisi zote za Serikali zinafanyaje kazi. Hili ni azimio lilikuwa la Bunge na sisi kama Serikali tunaanza kufanyika kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utendaji wa Ofisi ya Msajili wa Hazina na hii ndiyo maana siku zote tunapenda kusema, lazima tuwe na hofu ya Mungu, tunapoongea ndani ya Bunge hili lazima tuwe na hofu ya Mungu. Ndugu yangu, rafiki yangu Mheshimiwa Ester Bulaya uliposema kwamba Ofisi ya Msajili wa Hazina haijawahi kuwasilisha taarifa kwenye Kamati hii, hakuna aliyekataa, ni maoni ya Kamati lakini wewe, kipo ulichokiongezea kwamba taarifa hii Wizara ya Fedha na Mipango ndio inaishikilia taarifa ya Msajili wa Hazina na kuizuia kwamba isiletwe katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme hapana, Maazimio ya Kamati ambayo yaliletwa na sasa, tunayafanyia kazi ilikuwa ni kuhakikisha Ofisi ya Msajili wa Hazina inaongezewa Bajeti na ndicho ambacho Wizara ya Fedha na Serikali imefanya na sasa hivi ndicho walichokisema Msajili wa Hazina kwenye Kamati, wameongea na Ofisi ya Bunge kuona utaratibu na ni lini wawasilishe taarifa yao kwenye Bunge letu tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa ratiba waliyopewa kufika Aprili, 29 taarifa ya Msajili wa Hazina, itakuwa imewasilishwa katika Bunge lako tukufu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii na naunga mkono hoja za Kamati zote mbili, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namkaribisha Mheshimiwa Waziri Dkt. Philip Mpango.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana, kwa kunipa hii fursa niweze kuchangia kwenye hoja zilizotolewa, lakini nitangulize pongezi zangu za dhati kabisa kwa Kamati ya Bajeti na Mwenyekiti wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia *PAC* na Mwenyekiti wake, kwa kweli taarifa ni nzuri zina afya, na naamini kabisa zitatusaidia kuendelea na juhudi za kuboresha uchumi wa Taifa, lakini pia zitatuwezesha, kuimarisha utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha mwaka kilichobaki. Na naamini pia kwa upande wa *PAC* ushauri wao utatusaidia kusimamia utendaji wa Mashirika yetu na yale ambayo yametolewa kama ushauri na Waheshimiwa Wabunge waliochangia niwaahidi kwamba tutayafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya maneno hayo ya utangulizi, niseme kidogo, nikianza na lile ambalo alilieleza Mheshimiwa Balozi Kamala. Ni kweli kabisa kabisa, naungana naye, uchumi wetu umekuwa unakuwa kwa kasi na dunia yote inajua hivyo, sio tu kwamba ni jambo jema, lakini ni lazima tuhakikishe kwamba uchumi wa Taifa unaendelea kukuwa kwa kasi kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naungana naye pia kusema ni muhimu tuelekeze pia nguvu kukuza sasa *size* ya keki yenyewe, ametoa takwimu nzuri. Lakini ni vyema tukumbushane tunakotoka nchi yetu tunatoka kwenye kauchumi kadogo sana, kwa mfano mwaka 2000 *GDP* ya Tanzania ilikuwa ni dola bilioni 10.1 tu, sasa ndani ya miaka

15 kufikia 2017 uchumi wa Taifa umefikia dola bilioni 52. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo unakuwa haitoshi kwa hakika, ukilinganisha na takwimu na zile alizokuwa anasema kwa nchi kadogo kama Ubelgiji ni kweli, lakini msingi wake ni lazima tubadilishe sasa *structure* ya uchumi wetu, ili twende zaidi kwenye viwanda, twende zaidi kupanua pia huduma ambazo kama Taifa tuna fursa kubwa au *comparative and competitive advantages.* Kwa hiyo, nilitaka tu niungane na Mheshimiwa Dkt. Kamala na njia aliyosema ni sahihi, sio tu tuwekeze kama tunavyofanya kwenye *Standard Gauge Railway* tuwekeze kwenye umeme mkubwa ambao ndio msingi wa kujenga viwanda, tuwekeze kwenye *skills* za Taifa letu, lakini pia twende kwenye maeneo kama *tourism* ambayo itatupatia nguvu zaidi ya kuendelea mbele kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo ningependa kulisemea kidogo ni baadhi ya maeneo ambayo aliyasema Mheshimiwa Silinde, nilidhani ametoka sasa namuona, kwanza tu nisisitize wazee wetu walitufundisha mtegemea cha nduguye anakufa fukara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni muhimu sana kama Taifa, na hapa huwa siendi kwenye siasa za vyama, *very seriously* kama Taifa tusipofika mahali tukasimama, tukajitegemea, tukaendelea kutegemea hawa wajomba wa enzi zile, hatutakwenda, hatutakwenda kabisa. Kwa hiyo, kwa hili ningeomba sana Waheshimiwa Wabunge, tuungane kuhakikisha kwamba hatua zote ambazo Serikali inachukua hivi sasa, ili tujitegemee, kweli tunashikamana ili twende mbele kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui nisemeje, mimi ambaye nakwenda kuomba kwa niaba ya Taifa ninadhalilika mno, ninadhalilika mno, tumekaa na mradi wa *Stiegler's* ili tupate umeme wa kutosha kwa muda mrefu mno. Lakini hivi sasa, wao ndio wanataka watufundishe darasa kwamba sisi ndio

hatujui maana ya mradi ule, haiwezekani, haiwezekani hata kidogo, wala hatutakubali na wala hatutakubali,. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Silinde kupitia meza yako nataka tu nimkumbushe kwamba uandaaji wa takwimu za Pato la Taifa na ukuaji wake, unaenda kwa ngazi na inanishangaza kidogo kwa sababu Mtakwimu Mkuu wa Serikali alitoa mada kwa Kamati ya Bajeti namna ya kukokotoa takwimu za Pato la Taifa na mimi nilidhani si tulikuwa tumejitahidi kumuelewesha namna ambavyo tunafanya. Zipo zile za robo mwaka lakini, takwimu za robo mwaka zinakuwa zile ambazo baadhi ya vitu, havijapatikana sawasawa. Kwa hiyo, kwenye robo ya pili inayofuata unakuwa una takwimu nzuri zaidi, za robo iliyotangulia. Kwa hiyo, inawezekana kabisa kwamba takwimu ambazo tumetoa robo iiyotangulia tunapokuja robo ya pili, tukawa tumepata taarifa nzuri na kuzipitia zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sio kitu cha ajabu kabisa ukokotoaji wa pato Taifa, na kama utapenda tena turudie tuko tayari kurudie tukupeleke polepole polepole ili uweze kuelewa pato la Taifa linavyokokotolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila alinishangaza kidogo kama mwanafunzi wangu wa uchumi aliposema kwamba kama mfumuko wa bei, unateremka kwa nini bei hazipandi, ilinishangaza kidogo, sijui labda nikirudia kwa lugha nyepesi, mfumuko wa bei, ni kama gari linalotembea unaweza ukaamua kutembea kwa *speed* 100, unaweza ukaamua kutembea kwa *speed* 40 kwa hiyo tunaposema mfumuko wa bei, umeteremka, hatusemi kwamba bei nazo zimeshuka, tunachosema ni kwamba kasi ya ongezeko la bei limepungua, ndio maana yake, sasa sijui nitalieleza kwa lugha ipi zaidi ili lieleweke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kidogo juu ya mchango wa Mheshimiwa Bashe, nafikiri saa nyingine anakuwa anatumia macho ambayo ni-*bit pessimistic*. Kwa sababu ni kweli, ukiziangalia zile takwimu, kwa nusu mwaka ambao tulikuwa tumetazama, *export* nyingi hasa zile za

*tradition* zimepungua. Lakini sababu moja kubwa kwa mwaka huu ni kwa sababu ya tatizo la korosho tulilokuwa nalo na mimi naamini kabisa kwamba tutapata matokeo chanya baada ya muda si mrefu, kutokana na hatua ambazo zinaenda kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini namshangaa pia kwamba baadhi ya mauzo yetu nje kuna *component* zinaongezeka upande wa bidhaa za viwandani ni wazi kabisa zimeongezeka. Lakini pia baadhi ya bidhaa ambazo sizo za mauzo yetu ya asili nazo zimeongezeka, lakini la msingi ambalo nilitaka kusisitiza hapa, tumefanya mabadiliko makubwa katika uendeshaji wa biashara nchini ili kuirejesha nchi kwenye misingi halali na ya haki ya kufanya biashara. Sasa ni lazim utarajie kwa sababu biashara ni *cyclical* biashara sio kwamba kila saa, basi wewe utakwenda tu biashara mauzo yanaongezeka hayapungui hata kidogo, haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo pamoja na kuwa tunaendelea kulitazama, niliiambia Kamati ya Bajeti kwamba tayari tumeunda timu pale Wizarani ili tuangalie mwenendo wa mauzo yetu nje kwa kipindi kirefu zaidi ili pale ambapo kama kuna *structural problems* tuweze kuzishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulitolewa ushauri kwamba Kariakoo ilikuwa ndicho kituo kikubwa cha biashara na hususan tumeshauriwa tutazame sana soko la Congo na Zambia. Ni kweli kabisa na pengine labda hoja iwe kwamba tuongeze kasi katika kulitazama. Lakini kwa mfano dhamira ya Serikali ya kujenga Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Songwe maana yake ilikuwa ni hiyo, kwamba tuweze kupata wasafiri kutoka Congo, Zambia, Malawi na nchi nyingine zinazozunguka mpaka Zimbabwe, kwa hiyo sio kwamba tumefumbia macho soko hili hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada ambazo zinafanyika kujenga Bandari ya Karema zinaelekea huko huko, lakini pia hata hatua ambazo tumefanya kujaribu kuimarisha *management* ya *TAZARA,* lakini pia *TRA* na bandari

wamekuwa wanafanya ziara Congo na Zambia ili kuweza kuhakikisha kwamba tunashughulikia zile changamoto ambazo wafanyabiashara kutoka nchi hizo wanakumbana nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bashe pia nadhani nilimsikia akisema ni muhimu kwamba hatua zetu za kibajeti zijielekeze pia kwenye uzalishaji. Nakubaliana naye na nafikiri ndiyo sababu tumekuwa tunaelekeza zaidi fedha kwenye miundombinu ambayo itatuwezesha kuchangamsha uchumi wa Taifa zaidi kuliko ilivyokuwa hapo nyuma. Lakini hata kwa upande wa mabadiliko ya Sheria za Kodi ni wazi kabisa kwamba kupitia bajeti iliyopita, ndiko tulipojielekeza huko kuhakikisha kwa mfano kwamba tunapunguza kodi ya mapato *(income tax)* kwa ajili ya viwanda vipya mfano upande wa ngozi, lakini pia kupunguza ushuru wa bidhaa kwenye baadhi ya viwanda ambavyo vinazalisha kwa kutumia *raw materials* za hapa ndani. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge sasa nitawaita watoa hoja mmoja baada ya mwingine ili waweze kuhitimisha hoja zao kwa muda wa dakika kumi kumi. Nitaanza na Mwenyekiti wa Kamati Bajeti. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa na kwa niaba ya Kamati napenda niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge ambao wamepata fursa ya kuchangia hoja ya Kamati ya Bajeti kutoka pande mbili zote za Bunge, nawashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Aidha, pia napenda niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri ambao pia kwa namna fulani wamechangia lakini kwa kujaribu kufafanua baadhi ya maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge walihoji au wali-*criticize.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe waliozungumzia na kugusa ripoti ya Kamati ya Bajeti ni 17 na kwa sababu ya muda naomba nisiwataje majina yao. Hata hivyo si rahisi sana kwa muda nilionao kuweza kujibu hoja moja baada ya nyingine na kwa sababu hiyo nitajaribu kuchukua yale ya jumla jumla tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumziwa suala la ukuaji wa uchumi, lakini pia pongezi zimetolewa na wengine wame-*criticize* na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango amejaribu kufafanua kwamba hakuna ubishi kwamba uchumi wetu unakua kwa kasi nzuri na kwa Afrika sisi ni miongoni mwa nchi tano yaani tupo kati ya kumi ambazo uchumi wake unakua kwa kasi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo tunaweza tukajidharau lakini tunapojidharau katika mambo ya msingi yanayotupa heshima ni kama vile hatuitaki heshima. Kwa hiyo ni vizuri mimi niwasihi Waheshimiwa Wabunge kwenye mambo ambayo kama Taifa tunafanya vizuri ni vizuri tukasema tunafanya vizuri, lakini tukaboresha kwa maneno mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa hapa jambo la misaada na mikopo na msemaji aliyesema na wengine wamesema, lakini nimtaje Mheshimiwa Msigwa ambaye amesema bajeti yetu inategemea asilimia 40 kutoka kwenye misaada na mikopo, sijui hizi takwimu zinatoka wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikusihi Bunge lako liangalie matumizi ya takwimu ndani ya Bunge, kwa sababu sisi ni viongozi lakini Bunge hili limejaa wasomi watupu. Matumizi ya takwimu yaangaliwe, tusitajetaje tu na kuzungumza zaungumza tu. Ni vizuri tukazisema za kweli na

zilizopo kwa sababu takwimu ni tafiti na kama hujafanya utafiti huna haki ya kuzungumza. Sasa kama unatumia takwimu zisizo halali maana yake hukuwa na haki wala usahihi wa kusema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bajeti ya mwaka 2018/2019 mchango wa misaada na mikopo tulioutegemea kwa bajeti ya mwaka 2017/2018 fedha zenyewe tulizozihitaji ni trilioni 2.13 ambayo kwa bajeti yetu ya trilioni 32.475 kiwango hiki cha misaada na mikopo tulichokihitaji ni asilimia 6.55 tu. Kwa bajeti ya mwaka 2019/2020 ambayo tunaindaa sasa na tupo katika mchakato, kiwango tunachokihitaji kutoka kwenye misaada na mikopo its only 3.38 trilioni ambapo bajeti yake inatarajiwa kuwa trilioni 33.5; kiwango hiki ni sawasawa na asilimia 10.005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake kama Taifa tumebadilika, hiyo asilimia 40 ilikuwa ni zamani sana, tunakwenda kwenye kujitegemea na kwa hiyo kuzungumzia suala la misaada na mikopo kama ndio mwarubaini wa kuondoka kwenye umaskini wa nchi yetu sio sahihi ni kujidhalilisha kwa sababu tumejenga uwezo wa kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa suala la kama vile nchi kama nchi tunadharau, hatuheshimu, hatuthamini *private sector* katika kujenga uchumi. Hakuna nchi duniani ambayo leo hii inaweza kujenga uchumi wake bila *private sector* na Tanzania tunaheshimu sana *private sector* na ndio maana Serikali imetengeneza *blue print,* tumeripoti kwenye taarifa yetu. Serikali imeleta hapa sheria ambayo tumeifanyia kazi na kwenye ripoti ya Kamati imeelezea kwenye ukurasa wa 9 na 10. Kwenye ripoti ya Kamati tumeelezea kwamba tumetengeneza Sheria ya *PPP, PPP* maana yake ni nini, ni *Public Private Partnership.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumeelezea kwamba pia Serikali imeongeza diplomasia ya uchumi, mabalozi wote wameagizwa kwa ajili ya kuhamsisha wawekezaji mbalimbali kuingia nchini. Hata hivyo mafanikio yamejionesha na kwenye ripoti yetu tumesema kwenye ukurasa wa 10 kwamba hata

kwa kipindi hiki kifupi cha mwaka huu tu viwanda vitano vya dawa vinajengwa, kwenye ripoti yetu tumeonesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inaposemekana kama Serikali au nchi yetu hatuthamini wawekezaji mimi nashangaa na hii taarifa mmeitoa wapi kwa sababu kwenye ripoti yangu niliyoleta nimesema na namna tulivyofanya na Serikali ambavyo inafanya. Mimi nadhani mambo mengine tuyaseme lakini tuwe na kiasi katika kuyasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji mmoja mmoja wamesema na wamechangia mambo mengi ya msingi ambayo Serikali imeyachukua na sisi kamati tumeyasema kwenye taarifa yetu. yale ambayo Waheshimiwa Wabunge wame-*criticize* ni vizuri Serikali nayo ikayachukua; lakini unapo-*criticize* kwa jambo ambalo si sahihi, kwa mfano nimpongeze Mheshimiwa Silinde mara ya pili aliposimama kutoa taarifa amefafanua vizuri sasa kwamba fedha ya maji aliyokuwa anaisema si ya Mfuko wa Maji peke yake, ya Mfuko wa Maji yote ilipelekwa kama ilivyo isipokuwa Serikali haijapeleka fedha ya maendeleo kutoka Hazina. Kwa hiyo Mheshimiwa Silinde umefanya vizuri lakini mwanzo ulizungumza kwa ujumla kwamba hakujapelekwa fedha ya maendeleo ya maji. Kwa hiyo, kwa taarifa yetu umetutendea haki maana tulianza kushangaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine ambayo yamechangiwa sana na mimi niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge ni juu ya Serikali kuwa makini na ahadi ilizoziahidi na utekelezaji wake. Yapo yale maeneo ambayo Serikali tunakubaliana kabisa kwenye kamati, rai yangu kwa Serikali ni kwamba muhakikishe kwamba mnayatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, eneo la maboma ambayo tulikubaliana kwenye afya mmepeleka fedha vizuri lakini kwenye eneo la elimu hamjapeleka fedha vizuri kama tulivyokubaliana. Kwa hiyo, kwenye hili na Waheshimiwa Wajumbe wengi niwapongeze mmelisemea na Serikali wamesikia.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** *(Hapa alizungumza bila kutumia kipaza sauti).*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Tatizo lenu mnajua ku-criticize ndio kusema.

**MBUNGE FULANI:** Endelea Mheshimiwa.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Msigwa amelinganisha ukuaji wa uchumi na hali ya utoaji wa huduma. Huduma hizi haziwezi kuimarika kama misingi muhimu kama ambavyo Mheshimiwa Dkt. Mpango amezungumza, lakini kama pia alivyozungumza mjumbe wangu wa Kamati, Balozi. Amesema kwamba ni lazima tuimarishe kujenga ukubwa wa uchumi. Tunaweza tukawa na uchumi unaokuwa lakini uchumi huo ukawa mdogo, *we have to strengthen the economy, so how do we strengthen the economy* ni kuhakikisha kwamba miundombinu muhimu inayojenga uchumi inashughulikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kunahitaji maamuzi ya makusudi kujenga reli, ukijenga reli uchumi wako lazima utaimarika. Tukiwa na umeme wa kutosha kama tunavyojenga *Stiegler's Gorge* ni maamuzi ambayo unayafanya leo lakini yatautunza uchumi kwa muda mrefu. Kama tunavyojenga miundombinu ya barabara, kama tunavyojenga miundombinu na kuhakikisha kwamba watoto wetu wanasoma vizuri; una-*invest* kwa watu, huko ndiko kuimarisha uchumi utakaokuwa na uimara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Serikali iangalie pia namna ya kuimarisha katika eneo la *ICT*. Duniani sasa na nchi matajiri duniani wame-*invest* zaidi kwenye *ICT* na makampuni matajiri sana duniani ni wale wanaofanya biashara ya *ICT.* Kama Taifa ni vizuri na sisi tukaona tu-*invest* zaidi katika eneo hili kwa sababu hili eneo nalo tukifanya masihara nalo lina *connection* kubwa na uchumi wa kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tuna Mkongo wa Taifa ambao Serikali imewekeza hela nyingi sana, lakini utasikia *internet low,* malipo yanachelewa, *efficiency* inapungua. Sasa kwa nini tuwekeze fedha nyingi halafu tusipate faida ya jambo hilo? *(Makofi)*

Kwa hiyo rai yangu kwa Serikali ni kwamba *ICT area* ni muhimu sana iwe kwenye *perfection* na iwe kwenye *precision* kwa sababu bila kuwa na uhalisi na usahihi hatuwezi kupata tija na *payback* ya uwekezaji tulioufanya. Sasa tatizo hapa tatizo ni nini ni watu, *software ama ni hardware?* Hapa kama taifa tujaribu kutoka na wale ambao wanajua katika eneo hili wasitubabaishe zaidi tusiojua. Mimi naamini kama Serikali ime-*invest* lazima itulipe na malipo yake ni sasa wakati dunia inaishi kwenye maisha ya *ICT. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu michango ilikuwa mingi lakini kwa sababu ya muda nipende kurudia tena kuwashukuru wote kabisa ambao mmechangia maoni ya kamati yetu. Sisi kama kamati tunapongeza sana aina ya michango iliyotolewa inaweza ikawa mingine ilikuwa inakwenda kinyume lakini ukinyume huo ndio unaohitajika ili kufanya tufikiri zaidi. Kwa hiyo kimsingi yote yanahitajika katika muktadha wa kuchambua unachokifanya hasa katika utekelezaji wa bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya kwa niaba ya Kamati ya Bajeti naomba kutoa hoja.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti, hoja imeungwa mkono sasa nitalihoji moja kwa moja Bunge.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*
*(Taarifa pamoja na Mapendekezo na Maazimio ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2018 Ilipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Namkaribisha sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ili na yeye aweze kuhitimisha hoja yake kwa dakika kumi.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi napenda sana niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango mizuri ambayo kwa kweli imetupa afya njema sisi Wanakamati wa Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na hoja mbalimbali, na taarifa yetu ya kamati imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge 21. Sina haja ya kuwataja wote lakini niwashukuru wale wote ambao wamepata nafasi ya kuzungumza na hata mlitoa kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati hii ukiangalia msingi wake mkubwa ni kuangalia mapato ambayo hayatokani na kodi *(no-ntax revenue)* na ndio kigezo kikubwa sana cha uhai wa ufanisi wa Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii imejikita kuelezea ni mambo gani ya msingi ili Serikali iweze kuyazingatia. Kama itafanya vile maana yake tutapunguza ile nakisi ya bajeti kupitia mapato ambayo hayatokani na kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji wengi wamezungumza lakini ningependa nianze na jambo moja kidogo hapa la kufanya *clarification.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa ambazo Kamati inazo, Serikali ina taasisi 11 ambazo ina ubia wa kuanzia asilimia 50 na chini ya asilimia 50. Moja ya taasisi hizo zimechangia sana kupata mapato ya zaidi ya shilingi bilioni 35.9. Katika taasisi zile tatu zinazoongoza kuna Benki ya *NMB* iliyotoa shilingi bilioni 10 kama gawio, *PUMA Energy* ambayo Serikali ina asilimia 50 na ninaomba nirudie kwamba Serikali tuna ubia wa asilimia 50 kwenye Shirika la *PUMA Energy.* Sasa

nasikitika sana kama kuna watu ndani ya Bunge au ndani ya Serikali hawa-*acknowledge* hiyo, huyu ni mtoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna asilimia 31.8 kwenye Benki ya *NMB,* huyu ni mtoto wetu, tuna asilimia 30 kwenye Benki ya *NBC,* huyu ni mtoto wetu. Tuna asilimia 25 kwenye *Tanzania Planting Company Ltd.*, huyu ni mtoto wetu na ametoa gawio kubwa kuliko wote la shilingi bilioni 13.4. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri sana na naamini kwamba kama una mtoto msaidie na kama ana mapungufu mrekebishe lakini ningeona kwamba ni fahari tuone kwamba taasisi hizi tuzibebe vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inawekeza kwenye Shirika la Ndege - *ATCL* na Mheshimiwa Rais alikuwa *very clear* na akasema kwamba Serikali imewekeza pesa nyingi, tunawakabidhi *ATCL* muendeshe shirika hili, mkishindwa nawanyang'anya nawapa hata *Precision.* Maana yake ni kwamba tunataka uwekezaji huu uwe na tija kwa Watanzania na tunadhani ni fahari kwa wewe Mtanzania kutumia mali ya kwako, *brand* ya kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa sana kwamba Watanzania tujawe na uzalendo; na hata wenzangu waliochangia akiwemo dada yangu Mheshimiwa Ester Bulaya, amezunguma vizuri, lakini hoja ni kwamba uwekezaji kwenye ndege huwezi ukapata faida leo au kesho. Mashirika yote ya ndege hapa duniani hayapati faida peke yake, isipokuwa yanachochea kukuza uchumi kwenye sekta zote za uchumi wa nchi hiyo. Kwa hiyo, uwekezaji huu tusiuangalie kwa kuangalia faida, tuangalie una *multiply effect* gani kwenye uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya kuna suala la kujua kwamba *TRA* wanakusanya kodi, Msajili wa Hazina *(Treasury Registrar)* yeye anakusanya mapato yasiyotokana na kodi. Mapato yapo ya aina tatu makubwa; kuna gawio, *redemption of excess capital* au mtaji uliozidi na kuna asilimia

15 ya mapato ghafi, haya ndiyo makusanyo yanayopitia katika Ofisi ya *TR.* Ninachoomba Serikali huyu mtu awezeshwe, kwa maana ya *staffing, technology* lakini vilevile na namna ya kupata wataalam wenye weledi kuendesha Ofisi ya Msajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiyafanya haya na kwa bahati nzuri nimeshafanya *consultation* na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mawaziri husika wameona umuhimu huu kwamba Ofisi ya *TR* lazima tuiwezeshe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine cha msingi katika hili ni suala la Seikali kutokulipa madeni...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti naomba utoe hoja muda umeisha.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika kumi tayari?

**MWENYEKITI:** Ndiyo, naomba utoe hoja.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naomba basi niwashukuru wale wote waliochangia ukiwepo wewe mwenyewe kwa kuweza kutupa fursa hii; na basi naomba nitoe hoja kwamba lipokee maoni na mapendekezo ya kamati yetu, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, hoja imeungwa mkono. Waheshimiwa sasa ninawahoji.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa pamoja na Mapendekezo na Maazimio ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2018 Ilipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge nawashukuru na kuwatangazia rasmi kwamba sasa taarifa zote hizi za kamati hizi mbili zimeshakuwa ni maazimio ya Bunge kwa hiyo sasa ni jukumu la Serikali kwenda kushughulikia yale ambayo yameshauriwa katika Kamati zetu.

Waheshimiwa Wabunge, natumia fursa hii kuwashukuru wote kwa kazi nzuri ambayo tumeifanya siku ya leo na naomba Mwenyezi Mungu awabariki sana.

Kabla ya kuahirisha shughuli za Bunge kuna tangazo moja kubwa hapa linatoka kwa Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mwenyekiti wa tawi wa timu ya Yanga anawatangazia Wabunge wote wapenzi wa Yanga wakutane katika Ukumbi wa Msekwa mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge muda huu. (*Makofi)*

Baada ya kusema hayo nawatakiwa kila la kheri na nahairisha shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatatu tarehe 4 Februari, 2019 saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 8.00 Mchana Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatatu, Tarehe 4 Februari, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*